ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1. Mhe. Ali Abdalla Ali	Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini
2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni
3. Mhe. Mgeni Hassan Juma	Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais
5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani
6. Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais
7. Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/Jimbo la Tumbatu
8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais
9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais
10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni
11. Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani
12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais
13.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais
14.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais
15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
17.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/\Jimbo la Jang'ombe
18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara,

	Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
19.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
20.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi
21.Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
22.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni
23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole
24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
25. Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais.
27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
28.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi
29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
30.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae
31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake
32.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
35.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
36.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais

37.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
40.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
44.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
45.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
46.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
47.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
48.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
49.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
53.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
54.Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Jimbo la Kiembesamaki
55.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
56.Mhe. Marina Joel Thomas	Kuteuliwa na Rais
57.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando)	Jimbo la Mkwajuni
58.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	Jimbo la Bumbwini
59.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
60.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini
61.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi	Jimbo la Chambani
62.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
66.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
67.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
68.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
69.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
70.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
71.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
72.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
77.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Nne - Tarehe 21 Mei, 2014

(Kikao kilianza saa 3.00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHWA MEZANI

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kuwasilisha mezani hotuba ya kuwasilisha Mswada wa Sheria ya Kutoza Kodi na Kubadilisha baadhi ya Sheria za Fedha na Kodi kuhusiana na Ukusanyaji na Udhibiti wa Mapato ya Serikali na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Naomba kuwasilisha.(*Makofi*)

Mhe. Hamza Hassan Juma(Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti wa Kamati ya Baraza): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Wenyeviti wa Kamati zako za Baraza, naomba kuwasilisha mapendekezo ya Kamati ya Kadumu ya Baraza la Wawakilishi la Zanzibar kuhusu Mswada wa Sheria ya Kutoza Kodi na Kubadilisha baadhi ya Sheria za Fedha na Kodi kuhusiana na Ukusanyaji na Udhibiti wa Mapato ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.(*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa mwaka 2014/2015. Naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

Mhe. Hamza Hassan Juma (Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa): Mhe. Spika, kwanza nashukuru kwa kunipa vyeo vingi, lakini pia, napenda kuwasilisha hotuba ya maoni ya Kamati ya kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa mwaka 2014/2015.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 86

Sensa ya Watu Wenye Ulemavu

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Mhe. Spika, kabla ya kumuuliza swali langu Nam. 86 naomba nitoe utangulizi ufuatao. Wajumbe wa Baraza lako humu tumo ndani kwa nia njema kabisa ya kusaidiana na Mawaziri na wasituelewe Mawaziri kuwa tunakomoana humu ndani, nia yetu ni kupeleka nchi yetu mbele na kutumia wananchi, tofauti yetu ni milango tu humu.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba swali langu Nam. 86 lipate jawabu.

Je, serikali inaweza kulifahamisha Baraza hili kuwa watu wenye ulemavu wapo wangapi kote Unguja na Pemba kwa mgawanyo ufuatao:-

a) Walemavu wa viungo *(The physical impaired)*
b) Wasiona *(The visual impaired)*
c) Walemavu wa ngozi *(The Albinous)*
d) Viziwi (*The hearing impaired and cerebral porsy)*

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 86 lenye vifungu (a), (b), (c) na (d) kama ifuatavyo:-

Naomba Mhe. Mwakilishi na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu wakumbuke kwamba Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ilifanya usajili wa watu wenye ulemavu kwa Unguja na Pemba. Kutokana na usajili huo wa Idara ya Watu Wenye Ulemavu, imegundulika kuwa aina zifuatazo za watu wenye ulemavu kama ambavyo Mhe. Mwakilishi ameomba zimepatikana.

Mhe. Spika, taarifa hii imeletwa kwa njia ya jadweli linaloonesha jadweli la Unguja. Kwa upande wa Unguja aina ya watu wenye ulemavu wa ngozi idadi yao ni 192, aina ya watu wenye ulemavu wa uoni ni 903, aina ya watu wenye ulemavu wenye aina ya uziwi ni 1,146 na watu wenye ulemavu wa viungo 2,832. Jumla kwa aina hizo nne 5,073.

Mhe. Spika, jadweli la pili linaonesha kwa upande wa Pemba. Aina ya watu wenye ulemavu wa ngozi ni 171, aina ya watu wenye ulemavu wa uoni ni 759, aina ya watu wenye ulemavu ya uziwi 1352 na aina ya watu wenye ulemavu wa viungo 2149.

Mhe. Spika, hilo ndio jibu kwa swali la Mhe. Mwakilishi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri na ya kutia moyo na niendelee kumpongeza tena kama nilivyompongeza jana kuwa ni mwanamke jasiri na Marekani hawakukosea kumpa Shahada hiyo, naomba kumuuliza swali dogo tu la nyongeza.

Mhe. Spika, walemavu wa viungo wamekuwa na wakati mgumu sana wa kufika katika maeneo hasa ya skuli na wengine familia hutoka katika hali nzito kukosekana kwa baiskeli ya maringi matatu. Je, kwa nini serikali haiandai taratibu kila mwaka kununua baiskeli hizo na kusubiri wafadhili, kwa mfano mtoto Maryam aliyeepo Machui hana miguu ameonesha uwezo mzuri sana wa kusoma. Je, serikali inatoa kauli gani?

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, ahsante sana naomba kujibu swali la nyongeza la Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-
Mhe. Spika, ni kweli watu wenye ulemavu wa viungo hasa watoto wadogo wengi wanashindwa kuanza masomo yao kutokana na kuweza kufikia maeneo ambao skuli ambazo zipo. Katika vipaumbele vya Idara ya Watu Wenye Ulemavu mapema kabisa serikali imeanza kutenga bajeti kwa ajili ya kununua vifaa vya watu wenye ulemavu.(*Makofi*)

Mhe. Spika, mwaka 2012/2013 serikali ilitenga bajeti ya shilingi milioni mia tatu kwa ajili ya ununuzi wa vifaa hivyo, mwaka 2013/2014 nako zaidi ya shilingi milioni 200 zilitengwa kwa ajili hiyo na kwa kipindi hichi kidogo fedha itapungua ni kama shilingi milioni thamanini kwa ajili ya ununuzi huo na kwa kweli idara inajitahidi sana kuwaomba wazazi ambao wana watoto wenye ulemavu ambao wanahitaji vifaa hivi kufika katika Idara ya Watu Wenye Ulemavu ili kuweza kusaidiwa na yenyewe wizara inafanya *outreach programme* kuweza kwenda katika maeneo yote, kwa sababu walipofanya usajili walikuwa wamekwenda katika ngazi ya shehia na walikuwa wanakwenda nyumba hadi nyumba.

Mhe. Spika, nimuombe basi Mhe. Mwakilishi atuletee taarifa zaidi za mtoto wetu huyu Maryam ili tuweze kumsaidia, lakini niiombe jamii kwa ujumla kwamba pamoja na jitihada za serikali yetu za kuweza kusaidia katika ununuzi wa vifaa hivyo, tukumbuke kwamba watu wenye ulemavu na hasa watoto, ulemavu upo wa aina nyingi na vifaa vinavyohitajika ni vingi mno kuliko fedha ambazo zinatolewa katika bajeti yetu. Kwa hivyo, wito wangu kwa jamii ni kwamba sisi wenyewe pia tujitokeze kwa kadiri tunavyoweza kuweza kusaidia hali hii ya kuwasaidia ndugu zetu na watoto wetu ambao wapo katika hali ya ulemavu.(*Makofi*)

Mhe. Raya Suleiman Hamad: Mhe. Spika, ahsante sana na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, kwa vile watu wenye ulemavu wanakabiliwa na matatizo mengi ya vifaa mbali mbali vikiwemo vya watu wale wasiosikia na hivi viti vilivyoambiwa vipo, lakini viti hivi vipo katika Ofisi ya Watu Wenye Ulemavu zina michango mikubwa, watu hawa watazipata wapi pesa za kwenda kutoa michango?

Je, Mhe. Waziri. utatufanyia mpango gani wa kuwa viti hivi serikali ikivileta wapewe bure watoto wenye ulemavu viweze kuwasaidia.(*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, ahsante sana ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mhe. Raya Suleiman Hamad kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwa kadiri ya uelewa wangu na Idara ya Watu Wenye Ulemavu ambao ndio inayoratibu shughuli hizi, serikali haijauza na haitouza wala kutaka mchango wa wazee katika kuwasaidia vifaa hivi na ninafikiria Mhe. Raya Suleiman Hamad anazungumzia *NGO* ya watu wenye ulemavu, Umoja wa Watu Wenye Ulemavu, hiyo ni *NGO* na ina taratibu zake, pengine *NGO* inasaidia pesa kidogo na inakuwa na vifaa hivyo kwa wazee pia kuweza kuchangia kupata vifaa hivyo.

Mhe. Spika, lakini kwa kadiri ninavyoelewa mimi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haitouza, vifaa hivi vitatolewa kama visaidizi vikuu.(*Makofi*)

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunisaidia kupata nafasi kuuliza swali dogo la nyongeza.
Mhe. Spika, Mhe. Waziri, hapa ametoa takwimu kwamba mpaka muda huu tuna walemavu 5073. Katika takwimu hizi ulemavu huu umechangiwa na maumbile au ni jambo gani limesababisha mpaka kusababisha watu kufikia asilimia hii ya ulemavu huu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, ahsante sana naomba kujibu swali la nyongeza la Mhe. Rufai Said Rufai kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza nimkumbushe tu kwamba idadi hii aliyoitaja ni ya watu wenye ulemavu Unguja na kwa zile aina nne ambazo Mhe. Jaku Hashim Ayoub ameuliza, lakini idadi ya watu wenye ulemavu wa aina nyengine nayo ipo na idadi ni kubwa zaidi.

Mhe. Spika, naomba nikiri kwamba kwa sasa serikali bado haijafanya utafiti kuweza kubaini ulemavu huu hasa unasababishwa na nini, lakini ni imani yangu ni kwamba baadhi ya watu wenye ulemavu hawa wanazaliwa wakiwa na ulemavu, wengine hupata ajali wakati wa maisha yao na wengine hupata maradhi ambayo nayo husababisha ulemavu, lakini kwa kweli serikali bado haijafanya utafiti kuweza kubainisha kwa kina sababu za ulemavu huu.

Nam. 24

Sheria ya Kudhibiti Vitendo Vinavyodhalilisha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Mhe. Spika, tokea enzi za enzi Zanzibar imekuwa na utamaduni wa kuheshimu Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, serikali zote tokea ukoloni na baada ya kujitawala zimekuwa zikilinda heshima hiyo bila ya kutetereka. Hali hiyo imeanza kugeuka katika zama hizi ambapo ikifika mwezi mtukufu wa Ramadhani kunakuwa na vitendo vinavyokwenda kinyume na utamaduni wetu wa heshima ya mwezi mtukufu, kama vile vibanda vya hoteli kuwa wazi wakati wa mchana, wanawake kuvaa nguo zisizokuwa na heshima, baadhi ya *bars* za ulevi kuwa wazi nakadhalika, haya yote yanashusha hadhi ya utamaduni wa Ramadhani kuwa ni mwezi wa ibada ambao utamaduni wa kuheshimu tumerithi kutoka kwa wazee tangu dahari.

a) Serikali inatoa kauli gani unapofika mwezi wa Ramadhani kuhusu vitendo hivyo.
b) Serikali haioni haja ya kutunga sheria ya kulinda utamaduni huu mzuri wa kuheshimu mwezi mtukufu kwa wale wanaovunja kwa makusudi.
c) Serikali kuchelewa kuleta mswada huo, haioni kuwa inawanyima haki wananchi wa Zanzibar ambao zaidi ya asilimia 99 ni waumini wa dini ya Kiislamu na wana haki ya kulindwa utamaduni wao kwa sheria.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo (Kny: Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria) - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 24 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli kwamba tokea enzi zilizopita na hadi hii leo, kila unapowadia mwezi mtukufu wa Ramadhani, basi serikali hutoa kauli ya kuheshimu mwezi huu.

Mhe. Spika, kauli ya kwanza hutoka katika hotuba anayotoa Mhe. Rais wa Zanzibar katika mwisho wa mwezi wa Shaaban. Kauli ya pili huitoa Mhe. Waziri wa Katiba ya Sheria, takriban wakati huo huo. Mbali na hayo Mufti na Mashehe nao huelimisha jamii kuhusu utukufu wa mwezi huo na vipi Wazanzibari tunatakiwa kuuheshimu.

Mhe. Spika, katika kauli hizo hutaka hoteli zote zifungwe wakati wa mchana, watu wavae nguo zenye stara, watu wasile ovyo, wasilewe, wasaidiane na waoneane huruma na kuheshimiana.

Mhe. Spika, maagizo hayo kwa kiwango kikubwa sana yanatekelezwa. Sisi Wazanzibari ni wajibu wetu nasi kuyaripoti matokeo ya aina mbali mbali yatakayovunja heshima ya mwezi mtukufu wa Ramadhani. Kutokana na sababu hizo bado ninahisi hakuna sababu yoyote nzito ya kutufanya kutunga sheria juu ya mambo hayo, ila ni wajibu wetu kuelimishana mara kwa mara ili wananchi waelewe zaidi wao katika mwezi huo wa Ramadhani na miezi mengine.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, ahsante sana pamoja na majibu ya Mhe. Waziri kutokufanana na swali la msingi nilivyoliuliza. Hivi karibuni au siku za nyuma Uganda ni nchi yenye wakristo wengi, lakini imefanikiwa kupiga marufuku nguo za mavazi mafupi au maarufu vinaitwa vimini.

a) Je, kwa nini serikali inashindwa kuchukua hatua wakati mavazi hayo pamoja na suruali za modo zinaendelea kuvuruga silka na utamaduni na kuwarusha roho vijana wetu. Hilo moja.

b) Utekelezaji wa maagizo hayo hayafanyiwi kazi na vyombo husika, kwa nini asubiriwe raia ili aje kushtaki na kuchukuliwa hatua, wakati mambo yako hadharani. Wavuta unga wanatafutwa na wavuta bangi wanakamatwa, huoni serikali imeshindwa kutumia wajibu wake hapa.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo (Kny: Waziri wa Katiba na Sheria): Mhe. Spika, kama nilivyosema awali kwamba asilimia karibu 98 ya Wazanzibari ni Waislamu na tunapaswa wakati wote kuhakikisha kwamba tunakwenda sambamba na mafundisho ya dini yetu, hasa katika Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, ili kuhakikisha kwamba tunapata tija kutokana na mafundisho hayo ya Mwezi Mtukufu huu.

Mhe. Spika, sasa ni kweli kwamba yapo mambo ambayo yanafanyika na jambo ambalo linafanyika hivi sasa ni kuhakikisha kwamba tunatoa taaluma ya mara kwa mara katika jambo hilo, ili kuhakikisha kwamba jamii yetu inakuwa na ule utaratibu wa kutii sheria bila ya kushurutishwa na hilo ndio jambo la msingi la kujenga jamii iliyo nzuri zaidi, kuliko kujenga tabia ya kuwafanya wananchi watii sheria kwa kushurutishwa na kwa nguvu.

Mhe. Spika, kwa hivyo, bado naona kwamba ipo nafasi ya kuendelea kuelimishana na wananchi na tunashukuru sana kwamba Wazanzibari wengi hivi wamejitokeza katika makundi mbali mbali ya kijamii na hasa vikundi vya kidini tunavishukuru sana kwa namna ambavyo vinaendelea kutoa taaluma na kuwaelimusha wananchi wetu, kuhusu namna ya kuheshimu silka na utamaduni wetu ambao kwa kiwango kikubwa ni utamaduni ambao unalingana na dini yetu, kwa sababu asilimia kubwa ya wananchi wetu ni wale ambao tunafuata dini yetu ya Kiislamu.

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kuwa tatizo la kupuuza sheria ya mavazi ya mwaka 1970 limekuwa likilalamikiwa hapa Baraza, kwamba limemomonyoa utamaduni na heshima ya Mzanzibari. Kwa kuwa katika majibu ya Mhe. Waziri kakiri kwamba tatizo hilo limekuwa likiathiri hata heshima ya Mwezi wa Ramadhani.

Mhe. Spika, naomba nimuulize Mhe. Waziri, je, wizara yako ina mpango gani wa kuondokana na tatizo hilo?

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo (Kny: Waziri wa Katiba na Sheria): Mhe. Spika, sisi katika Wizara ya Katiba na Sheria jukumu letu kubwa ni kusaidia utungaji wa sheria mbali mbali katika nchi kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, lakini pia, kwa msaada wa Baraza lako tukufu na kwa idhini ya Mhe. Rais, pale ambapo sheria imeshatungwa ni jukumu la wizara husika kulisimamia.

Mhe. Spika, sasa katika hili la sheria ya mavazi, nadhani wizara inayohusika ni Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo. Sasa katika ile dhana ya kufanya kazi kwa pamoja ya *Cabinet*, yaani *Collective Responsibility*, labda nimjibu Mhe. Mwakilishi kwamba ninavyoelewa ni kuwa Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo tayari imeshamuandikia Mwanasheria Mkuu ili kuona kwamba Tume ya Kurekebisha Katiba ikae iangalie namna gani ya kuitazama sheria kongwe ile ya mavazi kwa minajili ya kuangalia utaratibu wa kuirekebisha, ili kuondoa kasoro ambazo zipo.

Mhe. Saler Nassor Juma: Mhe. Spika, kabla ya kuuliza swali la nyongeza, naomba uniruhusa kwa niaba yangu na kwa niaba ya Mamake Cholo, yaani mke wangu, pamoja na familia yangu kukupongeza wewe kwa umakini wako na umahiri wako uliouchota mara baada ya kuongoza lile Bunge la Katiba pale kama Mwenyekiti wa Muda, kwa kweli uzoefu wako umetusaidia mpaka sasa hivi.

Mhe. Spika, baada ya pongezi hizo, naomba niulize swali moja dogo kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kama swali la msingi lilivyoulizwa karibu asilimia 95 ya Wazanzibari ni Waislamu na tunawajibika kufunga na kuwacha mambo yote yanayoondoa funga katika Mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Kwa kuwa mbali na mahoteli aliyoyasema Mhe. Jaku Hashim, lakini kuna wanawake hoteli hawatembei, lakini kuna wale akina mama wao wanatembea, japo umekaa barazani kwako wewe, basi watakuwa wanatembea huku wamevaa vimini na kukupitia katika mbele ya macho yako, jambo ambalo linaweza kuondosha swaumu yako.

Mhe. Spika, kwa kuwa serikali yetu iko makini sana katika kutaka kulinda amani na utulivu katika nchi, kwa mfano pale ilipowakamata Masheikh na kuwaweka ndani katika kuimarisha dini ya Kiislamu ikaweka Masheikh wale katika kipindi kirefu sana. Swali sasa.

a) Je, utaratibu ule ule walioutumia kuwaweka Masheikh ndani kipindi kile mpaka wakawatoa juzi juzi tu, hawawezi kuutumia utaratibu ule kuwakamata na kuwatia ndani na kuwasweta na kuwatesa hawa akina mama wanaovaa vimini katika Mwezi Mtukufu wa Ramadhani. *That is (a).*
b) Kwa kuwa katika kipindi kile cha miaka ya 1970, ilitoka *Presidential decree* ya kuwapiga bakora na kuwaweka jela watu wote wanaovaa nguo fupi, pamoja na kunywa tembo na mnazi. Kipindi kile ilikuwa hakuna bia, walikuwa wanakunywa pombe za mnazi, sio tembo jamani nafuta neno "tembo" kwa sababu katika maeneo ya Kusini ni tatizo. Kwa hivyo, nafuta hapo nasema "pombe za mnazi".

Mhe. Spika, Marehemu Mzee Karume aliweka *Presidential decree* katika miaka ile ya 1969/70 na watu wengi wakaacha kunywa pombe na watu wengi wakaacha kuvaa nguo za kubana, kwa maana suruali za chupa.

Je, kwa nini hatumshauri Rais wetu mpendwa Dkt. Ali Mohammed Shein akaleta *Presidential decree* ya kuwachapa viboko na kuwaweka ndani hawa wanaovaa vimini katika Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, kwa dhamira ya kutufungulia swaumu zetu au ikaleta sheria itakayo-*base* zaidi katika Mwezi wa Ramadhani ya kuwasweka na kuwaweka ndani kwa muda wa siku aliyokamatwa mpaka Ramadhani nyengine ya siku kama ile aliyokamatwa, kwa watu wote wanaovaa vimini na kunywa pombe katika Mwezi huu wa Ramadhani?

Mhe. Spika: Mhe. Waziri, majibu kwa maswali marefu sana ya Mhe. Mjumbe.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo (Kny: Waziri wa Katiba na Sheria): Mhe. Spika, nchi yetu inafuata dhana ya utawala bora na kwamba ni vizuri wakati wote kuhakikisha kwamba dhana hii ya utawala bora inatumika katika kuendesha mambo yetu. Sasa rai kwamba tupite katika kila mitaa ya Unguja na Pemba, kuwatafuta wanawake wanaotembea na vimini kuwakamata na kuwasweka ndani. Kwanza itakuwa tatizo ni utaratibu mgumu sana, kama wanavyosema wenyewe kama wako wengi, basi nadhani mambo mawili ni muhimu.

Mhe. Spika, la kwanza tuendelee kuelimishana, kama nilivyosema awali kwamba ni vizuri tuandae utaratibu wa kutii sheria bila kushurutishwa ni jambo muhimu sana katika nchi ambayo inataka kujenga utawala bora na utawala wa kistaarabu katika nchi, ni lazima tufike hapo, lakini la pili, suala la kutoa taaluma liendelezwe na kuiangalia sheria iliopo. Sasa suala la kumuambia Dkt. Shein aweke *Presidential decree.*

Mhe. Spika, wakati Mzee wetu Marehemu Abeid Aman Karume alipotoa *Presidential decree*, siku zile kulikuwa hakuna Baraza la Wawakilishi. Kwa hivyo, hivi sasa chombo ambacho kinatumika kutunga sheria zetu ni Baraza

lako tukufu. Kwa hivyo, njia ambayo tumetumia hivi sasa kama nilipokuwa najibu swali la Mhe. Salma Mohammed ni kwamba Tume ya Kurekebisha Sheria, tumeipa kazi ya kuiangalia sheria ile ina mapungufu wapi, ili wakishafika pahala sisi Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo tutaileta katika chombo chako tukufu na tutaiangalia vizuri na Waheshimiwa Wajumbe watairekebisha kwa mujibu wa hali ilivyo na kwa mujibu wa mazingira yalivyo sasa. Hatuwezi kutumia mazingira ya *Presidential decree* ya mwaka 1970 tukaweza kuya-*impulse* hivi sasa, kwa kweli mambo mengi yamebadilika sana.

Mhe. Spika, kwa hivyo, nadhani tutakapokuwa tayari kupitia na msaada wa Tume ya Kurekebisha Sheria iliokatika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu chini ya Wizara ya Katiba na Sheria, tutaileta hapa sisi Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, ili kuona kwamba ni namna gani tunaweza kurekebisha vizuri kulingana na mazingira yaliopo sasa, kuhakikisha kwamba watu wetu sasa wanafuata sheria ambayo itatungwa na Baraza lako tukufu, badala ya *Presidential decree* ya Mhe. Rais.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri tunakushukuru na tunaendelea.

Nam. 20

Zanzibar Kutopiga Hatua Katika Michezo na Sanaa

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Mhe. Spika, ahsante sana kabla ya kujibiwa swali langu namba 20. Nataka kwanza nitowe pongezi kwa Mhe. Waziri kwa kuufanyia matengenezo au baada ya kusaini mkataba wa Uwanja wa Mau, kwa niaba ya baadhi ya wananchi wa Kikwajuni wamekupongeza sana kwa suala hili ambalo litaleta changamoto, ukizingatia Kikwajuni ni kituo kikuu cha wachezaji wa Timu ya Taifa ya Zanzibar na ya Tanzania Bara.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, naomba swali namba 20 lipate jawabu.

Mhe. Spika, kwenye miaka ya nyuma Zanzibar imekuwa ikisifika sana katika tasnia ya michezo na sanaa mbali mbali katika ukanda huu wa Afrika Mashariki na Kati, kiasi ya kuzalisha vipaji vingi vya michezo na sanaa mbali mbali vilivyosaidia kuitangaza Zanzibar katika ulimwengu wa michezo na sanaa. Nchi nyingi zimekuwa zikitumia vipaji vya wanamichezo na wasanii katika kujitangaza na kukuza utalii wao Kimataifa.

(a) Kwa nini Zanzibar imerudi nyuma katika tasnia ya michezo na sanaa, na
(b) Je, mikakati gani ya kutekelezeka inafanyika kuirudisha Zanzibar katika medani ya michezo na sanaa kama ilivyokuwa zama hizo, ili iweze kusaidia kuutangaza utalii wa Zanzibar Kimataifa kama nchi za wenzetu wanavyofanya, mfano Kenya.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 20 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli Zanzibar imekuwa ikisifika sana katika tasnia ya michezo na sanaa mbali mbali katika ukanda huu wa Afrika Mashariki na Kati, kiasi ya kuzalisha vipaji vingi vya wanamichezo na wasanii vilivyosaidia kuitangaza Zanzibar katika ulimwengu wa michezo na sanaa. Ni kweli nchi nyingi zimekuwa zikitumia vipaji vya wanamichezo na wasanii katika kujitangaza na kukuza utalii wa Kimataifa.

Mhe. Spika, baada ya kutoa maelezo hayo yanayokubaliana na Mhe. Mwakilishi. Sasa naomba kumjibu swali lake kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, naomba nitafautiane na Mhe. Mwakilishi kwamba Zanzibar imerudi nyuma katika tasnia ya michezo na sanaa, kwani pamoja na uhaba wa bajeti inayopatikana, tasnia hizo zimekuwa zikisonga mbele hatua kwa hatua, kwa mfano hivi sasa katika ukanda wa Afrika ya Mashariki na Kati Zanzibar ndio inayoongoza kwa umahiri wa kuendeleza sanaa ya taarab na uchongaji wa milango na makasha.

Mhe. Spika, kwa upande wa michezo, Zanzibar hatufanyi vibaya katika ukanda huu kwa michezo kadhaa ikiwemo ya soka, judo, karati, riadha, karata na michezo ya kiasili kama vile bao, dhumna, karata na mengineyo.

(b) Mhe. Spika, ipo mikakati inayochukuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, mikakati hiyo si ya kuirudishia hadhi Zanzibar, lakini ni ya kuendeleza tasnia ya michezo na sanaa kwa lengo la kusaidia kuutangaza utalii wa Zanzibar Kimataifa kama nchi za wenzetu wanavyofanya.

Mhe. Spika, mikakati hiyo ni pamoja na kujenga miundombinu bora ya michezo na sanaa. Miundombinu hiyo ni pamoja na viwanja vya michezo vyenye hadhi ya Kimataifa na studio za kurekodia muziki. Aidha, kumekuwa na juhudi zinazochukuliwa na serikali za kuwasaidia wanamichezo na wasanii, kuweza kushiriki katika mashindano na maonesho mbali mbali ya Kitaifa na Kimataifa, kwa lengo la kuwaongezea ujuzi na maarifa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, ahsante sana pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri. Mimi ningemuomba tu tusitofautiane. Hivi sasa watu wanafuatilia *league* ya Ulaya zaidi kuliko ya Zanzibar, utafikiri wanaishi Ulaya.

a) Je, ni lini *ZFA* na *TFF* zitakutana pamoja ili zirudishe *league* ya Muungano kwa vile *league* hiyo ilisaidia sana kukuza mchezo huu wa soka.
b) Ni lini serikali itafikiria mpango wa kurudisha mchezo katika Maskuli ya Sekondari na *Primary.*

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, kwanza suala la wananchi kuangalia mipira ya Ulaya ni suala la Utandawazi ambalo limeingia na hili halipo hapa Zanzibar tu, ukienda Bara na Kenye liko hivyo hivyo na jumla nchi zote za dunia ya tatu wanafuata utaratibu huo. Kwa hivyo, hilo sio la msingi.

Mhe. Spika, la msingi ni kwamba sisi kama wizara tunashirikiana na Baraza la Michezo ili kuona michezo yetu inaimarika, wazo lake la kwamba tukae na *ZFA* na *TFF* kurudisha *League* ya Muungano. Tunalichukua na tutalifanyia kazi.

Mhe. Spika, suala la kurudisha na kuamsha hisia zaidi ya michezo Maskulini, serikali imeanza kulifanyia kazi. Mimi na mwenzangu hapa Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, tumeshakaa kuliangalia hilo na tumeunda Kamati maalum ya kuhakikisha kwamba michezo Maskulini inapata hamasa kubwa na inarudisha hadhi ya kuibua vipaji katika nchi yetu.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza lenye sehemu (a) na (b).

Mhe. Spika, Mhe. Waziri, wakati anajibu swali lake alikiri kwamba Zanzibar au Wazanzibari wanapenda sana michezo ya sanaa. Hivi karibuni kikundi cha sanaa kutoka Egypt kilikuwepo hapa Zanzibar na kilifanya maonesho yake katika maeneo mbali mbali ili kuendeleza udugu na mshikamano na upendo kati ya Misry na Zanzibar, kama vile ambavyo wizara yetu imekuwa ikishirikiana katika kubadilishana mawazo katika mpira wa miguu kati ya Zanzibar na Egypt.

a) Je, kuna mipango gani ya kuwachukua au ya kuwapeleka vijana wetu wasanii wa Zanzibar Egypt kwenda kujifunza zaidi kwenye nyanja za sanaa.
b) Hivi karibuni kutakuwa na mashindano ya mpira wa miguu ya dunia, yaani *World Cup* na mchezo huu ambao unapendwa ulimwenguni kote na Zanzibar ni washabiki sana wa mchezo wa mpira huu wa miguu. Je, Wizara yake ina mpango gani na mikakati gani ya kuhakikisha kwamba michezo hii ya *World Cup* ambayo inakuja mwezi unaokuja itaonyeshwa *live* na *ZBC* ili Wazanzibari waone michezo hii ya *World Cup*.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, ni kweli kwamba juzi tulikuwa na kikundi cha utamaduni kutoka Misri ninafurahi kwamba Mheshimiwa Salim Ali Nassor (Aljazira) alikuwa mwenyeji wetu

katika jimbo lake katika burudani ile tunamshukuru sana sisi kama Wizara ya Habari, alitupokea vizuri na tulishirikiana nae hadi mwisho kuhusu kupeleka vijana au vikundi vya utamaduni Misri hilo tumelianza na kikundi cha Tauzi kimeshawahi kwenda Misri katika utaratibu huu. Kwa hivyo, wao ndio maana wakafanya ziara wakaja na wao kuitikia wito wetu, sasa utaratibu huu utakuwa unaendelea mwakani tutakwenda kwao kama hali itaruhusu na sisi mwaka unaokuja watakuja wao.

Mhe. Spika, kwa hivyo, ni jambo ambalo tumekubaliana ni suala la kubadilishana mara hii wanakuja wao mara nyengine tunakwenda sisi. Kwa hivyo, tuliwahi kwenda mara hii wamekuja wao na kwamba hali yao pale ndani itakuwa nzuri, basi kuhakikisha kwamba na sisi mwakani tutakwenda.

Mhe. Spika, suala lake la pili, ni kuhusu kombe la dunia na kuonyesha katika *ZBC. ZBC* siku hizi inaonekana zaidi katika king'amuzi cha *ZEDMUK* mipango inafanywa na uongozi wa taasisi ile kuhakikisha kwamba Wazanzibari watapata *live* michezo ya kombe la dunia, taratibu za mwisho zinakamilika hadi jana kuona kwamba mambo haya yanakamilishwa na tunaamini kwamba wale wote watakaokuwa na ving'amuzi, basi wataweza kuona michezo hii, taratibu zinafanywa pia kuona wale waliokuwa hawana ving'amuzi, basi ikiwezekana pia kuona, lakini hilo bado lipo katika hatua za awali.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, nashukuru kunipa nafasi nimuulize Mhe. Waziri suala moja la nyongeza, kwa kipindi kirefu kumekuwa na dhana kwamba michezo na burudani na sanaa ni dhana ya kwamba ni vitu vya burudani tu, lakini ulimwengu wa sasa umeigeuza dhana hii kutoka kwenye burudani na kuifanya kuwa ni sehemu ya uchumi. Je, Zanzibar inaitekelezaje dhana hii kufanya michezo na sanaa kuwa sehemu kuu ya burudani bali ni sehemu ya uchumi.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, ni kweli kwamba siku hizi sanaa na burudani ni dhana zaidi ya kiuchumi kuliko burudani, serikali katika hilo inafanya mambo mawili, la kwanza sera ndivyo inavyoagiza. Kwa hivyo, mikakati ya kisera, serikali ambayo tunasimamia wizara inaelekeza huko kwamba mbali ya kuwa burudani, basi sanaa na michezo ni suala la uchumi, katika utekelezaji huo tunaelekeza vyama mbali mbali vya michezo chini ya Baraza la Michezo kuelekeza nguvu zao katika huko na tunafurahi kwamba katika kiwango kikubwa baadhi ya vyama vya michezo vimeanza kutekeleza suala hilo na ndio maana ukaona vijana sasa wengine wanatafuta kucheza michezo nje ya nchi yetu.

Mhe. Spika, kwa hivyo, hiyo ni dhana hiyo, lakini mbali ya hilo tumewaelekeza kwamba wale ambao watafanya sanaa zao na michezo yao mbali mbali wanaweza kuisajili katika hati miliki ili kuona kwamba wanapata faida kiuchumi kotokana na sanaa zao na siyo iwe burudani peke yake.

Nam. 12

Tatizo la Maji na Umeme Mtambwe Kaskazini na Kusini

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuuliza suali langu nambari 12, suala ambalo ni la zamani sana. Kwa hivyo, kabla ya kuomba kupata majibu kwa ruhusa yako naomba kufanya marekebisho yafuatayo:-

Mhe. Spika, kwanza baada ya neno "Mtambwe Mkuu" paongezwe neno "Chanjaani", neno "Kidindo" lirekebishwe na liwe "Kidundo", neno "Cheke" lirekebishwe na kusomeka "Chekea" na neno "Kivukoni" lirekebishwe na lisomeke "Kivumoni" hilo la mwanzo.

Mhe. Spika, marekebisho ya pili, ni kuwa kwa sababu suala hili ni la zamani sana na tulikuwa tukiendelea na mchakato wa kuwatetea wananchi wetu kuna marekebisho yamefanyika, sasa ili Mhe.Waziri aweze kulijibu vizuri, naomba kufanya marekebisho namba mbili. Kwanza Mtambwe Mkuu badala ya kuwa hakuna maji na umeme, sasa hivi maji yapo tayari na yamepelekwa kutokana na mfuko wa maendeleo wa jimbo, Kidundo tayari kumeshakuwa na umeme, lakini maji hakuna, tokea hali ya kawaida hakuna maji wala umeme, Kivumoni maji yameshakuwapo linalohitajika ni umeme, Makongeni umeme tayari yanayohitajika ni maji na vijiji vingine Utaani, Tondooni, Mitambuni na Kinazini wanakabiliwa na tatizo la umeme na maji kwa marekebisho hayo kama yamefahamika, naomba suala langu namba kumi na mbili lijibiwe.

Mhe. Spika: Hili suala linaonekana kwa upevu wake lina ugumu kupata majibu yaliyo sahihi sina hakika, lakini mimi ningekushauri hili suala ukaliandika upya ukaliuliza. *(Makofi)*

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nakubali.

Mhe. Spika: Hebu niwache kidogo, inaonekana hata hayo majina sijui mengine yamefutwa yale majina ya mitaa na maeneo, lakini hebu liandike upya ili litokeze vizuri.

Nam. 25

Baraza la Manispaa Kukiuka Haki za Raia kwa Kukamata Mali Zao Kinyume na Utaratibu

(Suala hili liliondoshwa na Mheshimiwa aliyeliuliza.)

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2014/2015
ya Wizara ya Feddha

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nitoe ufafanuzi kwa hoja ambazo zimechangiwa na Waheshimiwa Wajumbe kwenye bajeti ya Taifa kwa kipindi cha siku mbili zilizopita, kabla sijaanza na kujibu hoja mbali mbali, naomba kwanza niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote kwa michango yao hii, ni bajeti yangu ya nne, kwa kweli nataka nikiri kuwa michango ya mara hii ilikuwa ni michangoa ambayo imeielekeza zaidi serikali katika kutekeleza majukumu yake.

Mhe. Spika, lakini la pili, michango ya mara hii imenifurahisha hakukuwa na marejeo rejeo. Kwa hivyo, kila hoja ambayo ilikuwa inachangiwa kwa kweli ilikuwa na umuhimu mkubwa sana katika kujenga na kuendeleza majukumu ndani ya serikali yetu.

Mhe. Spika, naomba basi kwa ruhusa yako hoja zilizoulizwa na zilizochangiwa ni nyingi, nataka niwaambie tu Waheshimiwa Wajumbe kwamba hoja zote tutazifanyia kazi, lakini kuzijibu hoja zote hapa nitachukua muda mkubwa sana.Kwa hivyo, hoja ambazo nitazijibu ni zile ambazo Wajumbe wamezichangia na wengine wamezisisitiza zaidi, naomba basi sasa kwa idhini yako niwataje wale wote waliochangia.

Mhe. Spika, Wajumbe waliochangia bajeti hii kwa kuongea walikuwa ni thalathini na sita (36) na wale waliochangia kwa maandishi walikuwa ni wanne, naomba niwataje. Wakwanza aliyeongea Mhe. Hamza Hassan Juma, Mwenyekiti wa Wenyeviti na Mwakilishi wa wananchi jimbo la Kwamtipura, Mhe. Mohammed Raza wa Uzini, Mhe. Ashura Sharif wa viti maalum vya wanawake, Mhe. Ali Salim Ali wa Kwahani, Mhe. Abdala Juma Abdalla wa Chonga, Mhe. Jaku Hashim wa Muyuni, Mhe. Hassan Hamad Omar wa Kojani, Mhe. Hussein Ibrahim Makungu wa Bububu, Mhe. Makame Mshimba wa Kitope, Mhe. Mussa Mohammed Mbwana wa Chambani, Mhe. Mwanaidi Kassim Issa wa viti maalum wanawake, Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi wa viti maalum wanawake, Mhe. Moh'd Haji Khalid wa Mtambile, Mhe. Marina Thomas mteuliwa wa Rais, Mhe. Saleh Nassor Juma wa Wawi, Mhe. Mohammed Mahamoud Mussa wa Kikwajuni, Mhe. Salma Moh'd Ali wa viti maalum wanawake, Mhe. Abdi Mossi Kombo wa Matemwe, Mhe. Abdalla Mohammed Ali wa Mkoani, Mhe. Abdu Haji wa viti maalum wanawake, Mhe. Suleiman Hemed wa Konde, Mhe. Hija Hassan Hija wa Kiwani, Mhe. Farida Amour wa viti maalum wanawake, Mhe. Rifai Said Rifai wa Tumbe, Mhe. Omar Ali Shehe wa Chake Chake, Mhe. Shadya Moh'd Suleiman wa viti maalum wanawake, Mhe. Salim Abdalla Hamad wa Mtambwe, Mhe. Hamad Masoud Hamad wa Ole, Mhe. Asha Bakari Makame wa viti maalum wanawake, Mhe. Mohammed Said Mohammed wa Mpendae, Mhe. Mussa Ali Mussa wa Koani. Mhe. Spika, na wengine ni Mhe. Bikame Yussuf Hamad wa viti maalum wanawake, Mhe. Asaa Othman Hamad wa Wete, Mhe. Shamsi Vuai Nahodha wa Mwanakwerekwe, Mhe. Mtumwa Kheri Mbarak wa viti maalum wanawake, Mhe. Mwinyihaji Waziri wa Nchi Ikulu na Utawala Bora pia ni Mwakilishi wa wananchi jimbo la Dimani.

Mhe. Spika, Wajumbe waliochangia kwa maandishi wa kwanza alikuwa ni Mhe. Ali Abdalla Ali Naibu Spika na Mwakilishi wa Mfenesini, Mhe. Panya Ali wa viti maalum wanawake, Mhe. Mahamoud Thabit Kombo wa Kiembesamaki, Mhe. Thuwaibah Edington Kisasi wa Fuoni.

Mhe. Spika, kabla ya kuanza michango, naomba kidogo nitoe nukuu mbili ambazo zimeibuliwa na Waheshimiwa Wajumbe kwa mnasaba wa bajeti yetu na michango na ufafanuzi nitakaoutoa, nimeona nukuu hizi ni muhimu kuzitaja, ya kwanza na nitaifafanua wakati ninapoendelea kutoa ufafanuzi wa michango, ni ile nukuu inayosema "afya ya binaadamu ni muhimu katika kujenga uchumi" ambayo imetolewa na Mheshimiwa Asaa Othman Hamad.

Mhe. Spika, lakini ya pili, ni ile inayosema kwamba "tutumie utulivu na amani iliyopo katika kuimarisha uchumi wetu" ni ile nukuu iliyotolewa na Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, nitazingumza nukuu hizi wakati ninatoa ufafanuzi.

Mhe. Spika, kuna hoja tatu nzito sana zimeelezwa na Waheshimiwa wengi, Mheshimiwa Dkt. Mwinyihaji amezitolea ufafanuzi, lakini na mimi naona kwamba ni vyema nikajaza nyama kwa mnasaba wa ufahamu wetu na faida ya wananchi wetu, la kwanza ni ile hoja ambayo ya kuifananisha Zanzibar na Mauritius, Mheshimiwa Dkt. Mwinyihaji ameieleza na mimi naomba nijalize, Wazanzibari tuna fursa kubwa sana katika kuekeza, sio Zanzibar tu ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Spika, kwa hivyo, Wazanzibari wengi tumeekeza Tanzania Bara ukilinganisha na wenzetu wa Mauritius ambao wao fursa zao kuwekeza zimo ndani ya Mauritius au kwenda nje ya nchi ambayo siyo yao kwa mnasaba huu tunao ndugu zatu wa Kizanzibari ambao laiti ingekuwa uwekezaji wao walioufanya Tanzania Bara wangeufanya Zanzibar, ni dhahiri kwamba uchumi wa Zanzibar ungepiga hatua zaidi na hata zile *investment* zao zingeweza kutoa ajira kwa vijana wetu, sitaki niwataje Wazanzibari gani, lakini tunawaelewa. Kwa hivyo, unapolinganisha Mauritius na Zanzibar, sisi tuna upande mkubwa zaidi wa kuwekeza na maeneo makubwa zaidi ya uwekezaji hilo la kwanza.

Mhe. Spika, lakini la pili, wenzetu wa Mauritius wameanza muda mrefu sana kuwa na *Air line* yao, watalii wanaowachukua kutoka nje wanakuja moja kwa moja pale Mauritius, kwa mnasaba huo, mchango wa ile *Air line* ni mkubwa zaidi katika uchumi wa Mauritius, sisi Zanzibar hatujawa na *Air line* yetu, tunagemea *Air line* za nchi nyengine kuleta watalii wale ambao tumewataja. Kwa hivyo, mchango wa *Air line* katika uchumi wetu ni ile *landing fee* tu hilo nalo vile vile tuliangalieni.

Mhe. Spika, lakini la mwisho katika eneo hili, wenzetu tokea walipopata uhuru walifungua milango kukarikaribisha wawekezaji kutoka nje. Sisi tumefungua milango katika miaka ya mwishoni mwa 1980. Kwa hivyo, utaona tofauti tuliyonayo katika uekezaji. Kwa hivyo, hata uchumi baina ya sisi na Mauritius utakwenda tofauti, lakini tusikate tamaa, tusikate tamaa muda na uwezo upo, tunachohitajia ni nini? Ni yale ambayo aliyosema Mhe. Shamsi amani na utulivu ndani ya nchi yetu. Tutumie fursa ya amani na utulivu ndani ya nchi yetu ili kujenga uchumi wetu, tutumie umoja tulionao ndani ya nchi yetu kujenga uchumi wetu, haya ndio ambayo nilitaka niyaseme katika eneo lile.

Mhe. Spika, eneo la pili, Mhe. Dr. Mwinyihaji, amezungumza, lakini na mimi naomba niongezee nyama kidogo, wengi tulihoji tukauliza ni kwa kiasi gani huu ukuaji wa uchumi unamsaidia mwananchi wa kawaida. Tukapeleka mkulima, mvuvi, wananchi wa kawaida wapo wengi, wengi sana. Nataka niseme tu ndugu zanguni, kuna maneno ambayo haya ni vyema tukawa nayo na tukayafahamu. Ukuaji wa uchumi ndio unaopelekea ukuaji wa maendeleo ya nchi, unapoona nchi ina maendeleo, basi uchumi wake umekuwa *source of economic development, it is economic growth.*

Mhe. Spika, hebu tujiulizeni, tulipokuwa na barabara 1970's na 1980's ndio leo? Tulivyokuwa na idadi ya shule 1970's na 1980's ndio leo? Tulipokuwa na idadi ya Vituo vya Afya na Hospitali 1970's na 1980's ndio leo? Haya yote sasa ukiyatazama kwa umoja wake tunafaidika sote. Shule zile tunapeleka watoto wetu wote, Vituo vya Afya na Hospitali tunatumia sote, barabara tunazitumia sote na zaidi mkulima anafaidika zaidi na utumiaji wa barabara, wa sababu ana *excess* ya soko, sasa hivi kutoka katika sehemu yake ya kilimo mpaka kwenye soko, cha msingi ni kuhamasishana na kuzitumia zile fursa ambazo zimeibuliwa kutokana na kukua kwa uchumi wetu.

Mhe. Spika, lakini la tatu, ambalo limezungumzwa vile vile sana ni suala zima la ukusanyaji wa mapato na kuibua vyanzo vipya, nataka niseme ndugu zangu Waheshimiwa Wawakilishi, juhudi za kukusanya mapato zinaendelea na kumbukeni tokea tumeingia mwaka 2010 Novemba, sio kodi nyingi zilizoongezwa.

Mhe. Spika, lakini kiwango cha mapato kinachoongezeka ni kikubwa sana. Kwa hivyo, ukusanyaji wa mapato lazima uendane na udhibiti wa mapato, sio lazima uendane na kupandisha kwa kodi. Tunachokihamasisha kwanza ni udhibiti wa mapato, hatua za kupandisha kodi, sote tunaelewa ukipandisha kodi katika sekta yoyote ile mlipa kodi ni mwananchi, *time* nyengine tunakuwa tunajidanganya tunasema mfanyabiashara analipa kodi, mfanyabiashara kodi ile anaipeleka kwa mwananchi, mlipa kodi ni mwananchi. Kwa hivyo, kupandisha kodi, maana yake unamfanya mwananchi yule kila muda awe nakulipa wewe na yeye atahitajia matunda ya kodi yake.

Mhe. Spika, lakini ndugu zangu Waheshimiwa wengi tumehoji hapa vyanzo vipya vya kodi, sina tatizo la chanzo kipya cha kodi. Mwaka jana nilikuja na kianzo cha kodi ada ya bandari kutoka Zanzibar kwenda Pemba na kutoka Pemba kuja Zanzibar na kutoka Zanzibar kwenda Dar-es-Salaam kuja Zanzibar, nilizungumza Ada ya Bandari. Baraza hili hili ikakubali ada moja tukaikataa, si vibaya serikali kuwaonea huruma wananchi wake, si vibaya.

Mhe. Spika, kwa hivyo, vyanzo vya kodi sio *solution* ya haraka haraka katika kupata mapato, sote kwa umoja wetu lazima tusimamie vyanzo vilivyopo, kwanza tukiulizana hapa wangapi katika sisi mwezi huu wa Mei wamekwenda madukani kununua vitu, sisi humu ndani Wawakilishi, halafu tuulizane wangapi wameomba risiti. Sasa hizo ndio tunasema tuzisimamie ili sote tusimamie ukusanyaji wa kodi ili mapato yetu yaweze kupatikana kwa ukamilifu.

Mhe. Spika, sasa naomba nende hoja zilizoulizwa na Wawakilishi *specific*, zile zilikuwa ni za jumla, lakini naomba niende kwenye zile *specific*. Nikianza na Mwenyekiti Mhe. Hamza umezungumzia sana suala ya *Cristal Hotel* Paje na suala la muekezaji Maghembe Michamvi na umezungumza vizuri sana na mimi nataka nikupongeze kwamba utaondoa shilingi kwa Waziri wa Fedha na Waziri wa Ardhi ninakuomba shilingi usiondoe. Hiyo shilingi ndio mkate wa watoto wako nyumbani kule. Kule kuna Safia, kuna Amne kule wote hawa watoto wa Omar Yussuf wanataka mkate ndio hiyo shilingi.

Mhe. Spika, lakini ninachotaka kukuomba wacha sasa tushirikiane mimi, wewe, Waziri wa Ardhi kwa umoja wetu tukae na hawa wawekezaji. Suala hili nimelifuatilia kwa undani kabisa nimegundua kwamba kuna matatizo ya ardhi, lakini bado tunahitaji kushirikiana mimi, wewe na Waziri wa Ardhi. Kabla ya Waziri wa Ardhi hajaondoka nimeongea na akaniahidi tu akirejea suala hili tutashirikiana na tutalipatia ufumbuzi. Nakuomba shilingi hiyo tuachie na tutalifanyia kazi kwa pamoja.

Mhe. Spika, umezungumzia kwamba uwanja wa ndege wa *terminal* tumefikia wapi? Na kuna baadhi ya Wajumbe hapa wamezungumza. Mhe. Dr. Mwinyihaji na yeye ameligusia kidogo. Nataka niseme tu kwamba tuko katika hatua ya mwisho, ile michoro ya marekebisho imeshakamilika, maombi yetu ya kupata pesa za kuendelea tayari yapo China na sasa hivi nina imani kwamba ukenda pale *Airport* utaona kazi zinaendelea, tunataka fedha ili kazi ziweze kuendelea na matarajio yetu kwamba *terminal* hii tutakabidhiwa kati ya mwezi wa 9 na mwezi wa 10.

Mhe. Spika, Mhe. Hamza umezungumzia kwamba tuongee na mabenki juu ya riba wapunguze riba, wazo lako sio baya, lakini riba inaongozwa na soko na mabenki haya yanaongozwa na Benki Kuu. Sisi tutajaribu tukipata muda kupitia wale wenzetu wanaoingia kwenye bodi ya Benki Kuu tutawaomba basi watusaidie kuzungumza na Benki Kuu katika eneo hili.Pia, umezungumzia suala la kuanzisha benki ya wanawake, ni kipindi kirefu unalizungumzia hili na nimeeleza kuanzisha benki, sasa hivi zinahitajika bilioni kumi na tano ili kuanzisha benki, hiyo ni benki ya kawaida *Commercial Bank,* unahitajia *about* 20 *to* 22 *billion* kuanzishwa *Commercial Bank.*

Mhe. Spika, lakini tayari tumeshafanya mawasiliano na Wizara ya Wanawake, nia yetu sio kuanzisha benki ya wanawake peke yao, kwa sababu washirika wanataka benki, wanawake wana benki, wakulima wanataka benki,wanaume pia wanataka benki yao. Tumesema wacha tuanzishe benki ambayo itakayokuwa na muono wa kuwasaidia hawa wote ambao wanaotaka kuanzishwa kwa benki tutaona baadae kiasi gani serikali inaweza ika-*contribute* na kiasi gani tunaweza tukauza *shares* kwa wananchi ili benki hii ikawa zaidi ni ya wananchi kuliko kuwa. Serikali hatuwezi tukawa tuna benki zaidi ya moja kulingana na hali yetu ya kiuchumi. Umesema kwamba kuhamasisha wananchi kuweka fedha zao benki na hasa ndugu zangu Pemba baada ya kuvuna karafuu.

Mhe. Spika, tumeshawaomba mabenki yetu yalioko Pemba na hivi karibuni Benki ya Posta nao waanzishe utamaduni huo wa kutoa elimu kwa wananchi wetu ili itakapofika ule muda, basi pesa zile waweke katika benki zao.

Mhe. Spika, Mhe. Hamza ametaka kupata maelezo ya kina juu ya mradi wa *ZUSP*, Dr. Mwinyihaji jana ametoa maelezo ya kina, sina haja ya kuyarudia. Umetaka Wizara ya Fedha kulipa deni la vikosi, nataka niseme tu kwamba lazima kuwe na *Financial Management Descipline*. Lazima kuwe kuna heshima katika matumizi ya pesa za serikali, serikali ilikuwa na madeni changunzima kutoka mawizara mbali mbali na maidara mbali mbali, ikayalipa madeni yote na ikasema kuanzia sasa kila atakaetumia alipe mwenyewe deni na tumetoa maelekezo kwamba madeni haya kila mmoja aya-*portion* katika bajeti zake, waanze kuyalipa taratibu taratibu.

Mhe. Spika, lakini hili la vikosi, nataka nikuthibitishie kwamba tumelipokea na tutaliangalia jinsi ya kuweza kufanya kazi pamoja kupitia vikosi na Wizara yao Tawala za Mikoa. Umetutaka *PBZ* waanzishe huduma za *visa card*, nadhani katika mikutano yangu niliyokuwa na *PBZ* hivi karibuni kama mwezi unusu uliopita hatua sasa ziko mbali na wamenipa matumaini kabla ya mwisho wa mwaka huu watakuwa tayari na wao wana *visa card* kabla ya mwisho ya mwaka huu, ndio matumaini walionipa.

Mhe. Spika, lakini kila siku nitakuwa na mimi jukumu langu kuwashtua. Nimesema yapo mengi, lakini nimechukua yale ambayo yalokuwa kidogo yanahitaji ufafanuzi wa haraka haraka. Mhe. Raza, bahati mbaya Mhe. Raza hayupo, lakini jirani yake pale Mhe. Bi Raya ndio jirani yako hapa utamuwekea majibu akija utampa. Ameuliza pale Mhe. Raza bilioni 27.1 ni msaada? Swali hilo vile vile limeulizwa na Mhe. Saleh Nassor, Mhe. Salma Mohammed, Mhe. Hija Hassan, Mhe. Jaku, wote wameuliza swali hilo.

Mhe. Spika, nataka nijibu kwa ujumla. Hizi ni *GBS General Budget Support*, fedha hizi ndugu zetu wa washirika wa maendeleo huwa wanaisaidia Tanzania na wanapoisaidia Tanzania, sisi huwa tunapata asilimia 4.5. Kwa hivyo, fedha hizi ni msaada kutoka kwa washirika wa maendeleo, akauliza tena Mhe. Raza 15.75 bilioni pia hizi ni kodi zinazotokana na mapato ya wafanyakazi wa Muungano wanaofanya kazi Zanzibar. Kodi hii inatakiwa ilipwe pale ambapo mfanyakazi yule anapofanya kazi ili iweze kuhudumia katika maeneo yale. Kwa hivyo, hii ni kodi ya pili, hiyo ni kodi ambayo inakusanywa na Serikali ya Muungano halafu inarejeshwa Zanzibar kwa wale wafanyakazi wa Muungano waliopo Zanzibar.

Mhe. Spika, halafu kuna suala jengine nikaulizwa Muungano umesaidia nini kwenye bajeti ya Zanzibar. Nataka niseme kwamba kama kusaidia pesa taslim katika bajeti hii hatujapata msaada huo, lakini miaka ya nyuma tumewahi kusaidiwa ujenzi wa barabara ya Amani/Mtoni na Jumba namba 10 la Michenzani, lakini kimsingi bajeti hii ukiangalia ina mikopo, mikopo ile inadhaminiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ule ni msaada mkubwa kwetu kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hivyo, unaweza ukasema kwamba tunao msaada kwa sababu wamedhamini mkopo ambao unatumika katika miradi yetu mbali mbali.

Mhe. Spika, Mhe. Ashura, ameuliza matumizi yetu yaendane na mapato yetu, mimi nakubaliana na wewe sana Mheshimiwa. Huwezi ukakata kitambaa cha kushona shati, halafu ghafla ukageuka ukasema nishonee koti, hakitatosha na hili limeungwa mkono na Mhe. Jaku, Mhe. Mdachi, Mhe. Rifai na Mhe. Omar Ali Shehe wameunga mkono na ndio kwa maana pale tuliposema kwamba mwaka huu tunataka kuja na bajeti ya uhakiki, tunataka kutazama kipi tulichotegemea kukipata, tumepata kipi halafu tuanzie na pale tulipokipata tuone sasa matarajio ni nini? Sio tuanzie pale tulipopanga. Ukianzia ulipopanga hutakwenda.

Mhe. Spika, kwa hivyo, mimi ninakubaliana na wewe kabisa Mhe. Ashura katika kutushtua katika hili na ndio ambalo naomba sana tulisimamie na ndio ambalo katika vitabu vyetu vya mwaka huu mtaliona. Mnawezamkaona kwamba wizara mwaka jana *OC* tuliipangia kuipa bilioni mbili, lakini mwaka huu tunaipa bilioni moja, msije mkahoji kwa nini tumeipangia bilioni mbili mwaka jana, mwaka huu tumeipa bilioni moja, mmewapunguzia, hatujawapunguzia, pengine walichokipata ni milioni mia nane tu, hawakupata bilioni mbili. Kwa hivyo, huwezi kuanzia bilioni mbili wakati hawakuzipata bilioni mbili. Kwa hivyo, hapa ndio tunaposema kwamba tunapotaka kwenda.

Mhe. Spika, Mhe. Ashura vile vile, ulisema kwamba tufanye tathmini katika vyanzo vya mapato.Hiyo kazi inaendelea na tunaviangalia vyanzo vyetu vyote vya mapato na ndio kwa maana Mhe. Hija alihoji kwenye kodi za ardhi, kwenye ripoti ya mdhibiti, ile ni tathmini tulimtaka mdhibiti akaifanye atuletee tuone, kuna baadhi ya ardhi, wawekezaji wamezichukua wanasubiri mpaka wajenge, ndio walipe kodi nikawaambia sasa hapana. Ukipewa ardhi

unaanza kulipa kodi pale pale, ukikaa miaka 10 tunasema aa kumbe wewe huna maendelezo yoyote tunachukua ardhi yetu.

Mhe. Spika, kwa hivyo, ile ni tathmini ambayo imetusaidia sisi. Kwa hivyo, vyanzo vyetu hivi vyote tunavifanyia tathmini kuweza kujua ni kianzo gani ambacho kinahitajia kufanyiwa marekebisho ya kisheria au ya kikanuni. Tunakushukuru sana Mhe. Ashura kwa hilo na tunakupongeza sana.

Mhe. Spika, Mhe. Ali Salim, swali lake liliungwa mkono na Mhe. Mshimba, Mhe. Mohammed Mbwna, Mhe. Mwanaidi, Mwenyekiti wetu Mhe. Hamza, Mhe. Suleiman Hemed, Mhe. Omar Ali Shehe, Mhe. Shadya na Mhe. Panya wote waliliunga mkono swali hili kukusanya mapato zaidi na kubaini wakwepa kodi. Hili nimelitolea ufafanuzi pale mwanzo. Kwa hivyo, tunakupongezeni na tunakushukuruni sana.

Mhe. Spika, Mhe. Ali vile vile, alisema baadhi ya mawizara wananunua samani ambazo hazina viwango. Nataka niseme tu kwamba sasa hivi tumejipanga katika kui-*review* kuifanyia mapitio sheria yetu ya *Procurement*, sheria hii sasa itadhibiti hayo mambo. Tumezungumza vile vile vyanzo vipya vya kodi ambavyo nimeshavitolea maelezo, amezungumzia pia mashine za kutoza kodi gharama zisiwe kubwa. Sisi kwa upande wetu mashine hizi tutaziingiza nchini hazitalipiwa kodi na tutaziuza kwa wafanyabiashara kama mtu anazo *cash*, atalipa *cash*, kama hana tutamkopesha kwa kipindi maalum. Lengo letu tunataka wafanyabiashara wa-*comply* na matumizi ya mashine hizi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nataka niwaambie Waheshimiwa mashine hizi zitasimamiwa na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko na sio Wizara ya Fedha, kwa sababu wafanyabiashara wako chini ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko, hawako chini ya Wizara ya Fedha, kwangu mimi wako kwenye kodi tu basi.

Mhe. Spika, Mhe. Abdala Juma Abdalla naye vile vile, alizungumzia suala la Mauritius na Zanzibar, nimeshalitolea maelezo. Pia, alitaka kuelewa asilimia 4.5 ya msaada, hili liliulizwa vile vile na Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mhe. Saleh Nassor Juma hata Mhe. Hija Hassan Hija.

Mhe. Spika, hapa Waheshimiwa Wajumbe nataka nieleze kidogo, katika ile misaada ambayo mmeitaja na Mhe. Hija Hassan Hija na yeye ameitaja *one point something billion,* sio misaada yote ya *1.5 billion* Zanzibar inapata 4.5, ndani ya ile misaada mna misaada inayokwenda kwenye sekta moja kwa moja. Kwa hivyo, toa ile inayokwenda kwenye sekta ambazo sio za Muungano.

Mhe. Spika, lakini nataka nimshukuru sana Waziri wa Fedha wa Muungano Mhe. Saada Mkuya, mmoja aliniuliza kwa nini sikusema kama ni Mzanzibari? Huyu ni Mtanzania mwenye asili ya Kizanzibari kama mimi, tumekaa tumezungumza hata ile misaada ya kisekta tumesema kama ni elimu Zanzibar nayo elimu ina matatizo, kama ni umeme Zanzibar nako umeme una matatizo, kama ni afya tumesema hata ile sasa tuangalie jinsi na Zanzibar wanavyopata 4.5. Tunachokihitajia kutoka kwenye sekta ku-*review* sekta zao na kuwa na *review paper* ambayo inaweza kuonesha changamoto ziko wapi na zinahitaji kiasi gani ili ile *paper* tukaweza kuwasilisha kwa wenzetu pale ambapo sekta zitakapoitwa kwa kuweza kufanya huo uwasilisho.

Mhe. Spika, kwa hivyo, hili lisiunganishwe pesa zote zile za msaada kwamba Zanzibar tunapata 4.5. Hivyo, ni 56 billion, hapana, toa zile za sekta kwa mfano mle ndani kuna Sekta ya *TANESCO*, kama *TANESCO* inasaidiwa, basi toa za *TANESCO*, kile kinachobakia ambacho hakina *commitment* za sekta, ndicho tunachogawana na gawio letu lilikuwa ni shilingi 40 bilioni.

Mhe. Spika, Mhe. Abdalla Juma Abdalla vile vile, alitaka maelezo juu ya miradi mbali mbali. Namshukuru sana Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Ikulu na Utawala Bora ameitolea maelezo baadhi ya miradi, isipokuwa Mhe. Waziri ameuacha Uwanja wa Ndege wa Pemba, naomba kidogo niutolee maelezo.

Mhe. Spika, Uwanja wa Ndege wa Pemba *Feasibility Study* imeshakamilika, wataalamu walipokuja nataka niseme hivi, mwanzo tulitaka tuongeze *run away*, njia ya kurushia ndege, tulitaka tuiongeze ili ndege *Boeing 7737* tuweze kutua kama zile *Boeing* walizokuwanazo *Air Tanzania*, baadae wataalamu walipokuja wakaiangalia ile *run away* iliyoko sasa hivi, wakasema kwamba hii ya sasa hivi haitaweza kuhimili ndege ile, ikija tu ile ndege ikitua *run away* ile inaweza ikadidimia. Kwa hivyo, wataalamu wakatushauri kwamba lazima iongezwe *surface* ili iwe ngumu zaidi. Kwa hivyo, katika ile bajeti yetu ya awali sasa hivi bajeti yetu itaongezeka, lakini Uwanja wa Ndege wa Pemba

utajengwa, *run away* itaongezwa, itajazwa *surface* ile, itatiwa *fence*, litajengwa jengo, kitawekwa kila kitu ambacho tunakiweka katika viwanja vya ndege.

Mhe. Spika, matarajio yetu *document* hii wakati wowote ule itaweza kwenda *Exim* ya Uturuki, tayari tumeshawaandikia Serikali ya Jamhuri ya Muungano kutoa *Concessional letter* kwa ajili ya mkopo huu na tayari tumeshafanya mazungumzo na Benki ya *Exim* ya Uturuki na wao wameonesha nia mradi ukishakufika pale tunatarajia fedha zitapatikana, tunachokimbizana ni kwamba miradi hii iweze kuanza kabla ya kumalizika kwa mwaka huu. Kwa hivyo, nakuombeni Waheshimiwa Wajumbe muendelee kustahamili.

Mhe. Spika, Mhe. Jaku Hashim Ayoub alihoji shilingi 35 tulizoongeza mwaka jana kwenye bajeti, kwenye mafuta zimekwenda wapi wakati barabara ni mbovu? Nataka niseme tu kwamba hizi shilingi 35 ukisoma bajeti yangu ya mwaka jana hatujaziongeza katika *road fund,* lakini tayari watu wa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kama sio leo kesho wanatiliana saini na Mfuko wa Barabara ili waanze kuzitengeneza hizi barabara ambazo zinahitaji marekebisho, Fedha Mfuko wa Barabara wanazo.

Mhe. Spika, Mhe. Jaku Hashim Ayoub vile vile, alisema mafao madogo kwa wataalamu wa afya. Nataka nimthibitishie kwamba mafao ni madogo, lakini juhudi za kuongeza mafao kwa wataalamu wote sio wa afya tu, zinaanza kuonekana. Nimekuja na takwimu hapa Mhe. Naibu Waziri wa Afya ananiangalia, mwaka 2007 na hizi nataka wenzangu waziweke kwenye vichwa. Mwaka 2007 daktari ambaye ana *degree* mshahara wake ulikuwa ni shilingi 140,000 na *nurse* ambaye mwenye *degree* mshahara wake ulikuwa ni 129,000. Dr. Ali Mohammed Shein alipoingia mwaka 2011 daktari mwenye *degree* mshahara wake shilingi 601,000 na *nurse* mwenye *degree* shilingi 482,000, leo tunazungumza hapa, nazungumzia leo, daktari mwenye *degree* shilingi 934,000 na *nurse* mwenye *degree* shilingi 507,000.

Mhe. Spika, mambo mawili nataka muwe nayo, hii ni mishahara ya kuingilia, lakini vile vile, hii ni mishahara sio na posho. Nataka nikwambieni mwakani tutaondoka hapa twende zaidi, tuombe Mungu nchi yetu iwe na utulivu, iwe na amani ili uchumi uweze kukua, haya ndio maslahi ambayo tunayazungumza na hatuwezi tukaacha maslahi ya watu wetu.

Mhe. Spika, madaktari hawa kama hujawashughulikia ipasavyo kwa maslahi yao, watatukimbia, sisi kazi yetu itakuwa tunasomesha na wao wanakimbia tena kwa jirani tu hapo, lakini leo tofauti ya daktari anayeingia na *degree* kwetu na wao sio kubwa sana. Sasa mtu anaweza kufikiria afanye kazi nyumbani akafanye kazi ugenini. Tutaendelea kuboresha maslahi ya madaktari na maslahi ya watumishi wa umma wote kwa ujumla wao.

Mhe. Spika, nimeulizwa na Mhe. Makame Mshimba Mbarouk kianzio gani cha uchumi na kianzio gani cha mapato kilichopelekea uchumi kukua na kianzio cha mapato kilichopelekea mapato kukua. Nataka nimwambie kianzio kilichopelekea uchumi kukua ni kilimo na huduma, ndio zinazoonesha kwamba *contribution* yao katika *GDP* ni kubwa zaidi, lakini vianzio vyetu vya mapato ambavyo vinaonesha kukua vizuri ni kianzio cha *VAT*, kianzio kile ukitizama kinakua vizuri sana, *ofcourse* na vianzio vyengine navyo vile vile tunaviangalia ili viweze kukua vizuri.

Mhe. Spika, Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi ameuliza mengi, lakini nataka ninukuu mawili matatu, la kwanza amesema mishahara kima cha chini bado ni midogo, mimi nakubaliana na yeye, bado ni midogo, lakini juhudi zitaendelezwa kukuza kuongeza mishahara ya kima cha chini na mishahara katika *levels* zote, tuombe Mungu uchumi wetu ukue na utakuwa *Inshaallah,* la msingi ni kujituma na kuiweka nchi yetu katika amani na utulivu.

Mhe. Spika, lakini vile vile, amesema kwamba watalii ni wengi mapato hayaonekani. Nataka niseme tu kwamba mapato yapo yanaonekana, mapato ya mtalii yanaonekana katika maeneo gani? Kwanza mapato ya mtalii yanaonekana katika kodi ya *Airport*, kila mtalii anapokuja na kuondoka anatakiwa alipe *Airport service charge*, kuna mapato pale yanaonekana, lakini la pili, mapato ya mtalii yanaonekana katika *VAT*, anapokwenda kwenye hoteli kuna *VAT* mtalii anatakiwa alipe, pale yanaonekana.

Mhe. Spika, lakini la tatu, mapato ya mtalii yanaonekana kwenye *visa*, nne mapato ya mtalii yanaonekana katika *hotel levy*, lakini la tano, mapato ya mtalii yanaonekana katika mafuta, tusikae tukamtizama mtalii katika eneo la *visa* tu, mtalii anatembea, wanakodishwa magari mafuta yale yanavyotumika na ukitizama tumetoka viwango fulani vya mafuta na sasa hivi tunatumia mafuta zaidi ya milioni sita. Kwa hivyo, mapato ya mtalii yanaonekana, lakini yamo katika sekta tofauti tofauti.

Mhe. Spika, Mhe. Mohammed Haji Khalid yeye ameeleza fedha za maendeleo asilimia 80, ni misaada na mikopo, hii ina maana tumetawaliwa kiuchumi. Nataka Waheshimiwa Wawakilishi na hizi *data* ninazowapa waziandike zitawasaidia. Katika bajeti yetu mikopo ni shilingi 199.14 bilioni kwenye miradi, *contribution* ya SMZ kwenye miradi ni shilingi 65.9 bilioni, misaada shilingi 66.3 bilioni. Kwa hivyo, mikopo na *contribution* ya serikali ni pesa zetu, si misaada hii, tutalipa ni za kwetu na kukopa haina maana kwamba umetawaliwa kiuchumi, hata Mataifa makubwa duniani yanakopa.

Mhe. Spika, mimi nikitoka nikienda kumkopa Mhe. Jaku Hashim Ayoub haina maana kama nimetawaliwa na Mhe. Jaku Hashim kiuchumi, lakini ukope kwa maendeleo ukikopa kwa maendeleo unaondokana na yale matatizo leo na miaka 20 au 50 inayokuja. Kwa hivyo, tuendelee kukopa ili kukuza uchumi wetu.

Mhe. Spika, lakini Mhe. Omar Ali Shehe alisema nini tufanye ili tuondokane na utegemezi. Nataka niseme maeneo matatu nini tufanye ili tuondokane na utegemezi. La kwanza, mimi nitasisitiza kauli ile ya Mhe. Shamsi Vuai Nahodha amani na utulivu, tutumie amani na utulivu katika kuimarisha uchumi wetu, ikiwa nchi hii haina amani, siku zote mtakuwa tegemezi, mtaletewa chakula cha misaada kwa ndege, tena ndege inaning'inia juu huko anamwaga tu puu puu.

Mhe. Spika, lakini la pili, ni umoja, leo Wazanzibari tumeondoka kwenye umoja, yaani tuna ubinafsi tu sasa hivi, tutaendelea kutegemea, kwa sababu kama hamna umoja wenzetu watakuja *divide and rule*, wataendelea ku-*divide na ku-rule* hamna umoja, lakini la tatu, kujituma, leo Wazanzibari wengi hatujitumi jamani. Kwa hivyo, hayo matatu Mhe. Omar Ali Shehe tukiyasimamia utegemezi utaondoka tu, ndio wenzetu wa China sasa hivi walivyo, Wachina ndivyo walivyofanya wanajituma, Wachina wako wamoja, China iko amani na uwezo wa kufanya hivyo Wazanzibari tunao.

Mhe. Spika, Mhe. Mahmoud Mohammed, maana sasa hivi wako Mahmoud wawili hapa, amesema sababu zipi zilizopelekea deni la Taifa kuongezeka? Tunataka tupige hatua haraka, tunajaribu kukopa haraka tujenge miundombinu ili tuondokane na matatizo ya miundombinu ile, ukisubiri ukope kesho gharama za ile miundombinu unayotaka kujenga zitaongezeka. Kwa hivyo, acha tukope leo ili gharama zisije zikakua, leo kilomita moja ya barabara ukitaka kuijenga tena katika maeneo ambayo udongo wake ni mzuri kama maeneo ya kusini ni dola milioni moja, ukienda katika maeneo ambayo yana udongo lepe lepe zaidi ya dola milioni moja, kilomita moja ya barabara, tukichelewa gharama zitakuwa kubwa, ndio sababu zilizopelekea tunataka kukopa mapema na si aibu kukopa, wacha tukope, madhali tunakopesheka wacha tukope.

Mhe. Spika, Mhe. Salma Mohammed Ali suala lake limekuwa *echo* na Mhe. Salim Abdalla Hamad na Mhe. Asha Bakari Makame. Mhe. Abdalla Mohammed Ali vile vile na hapa nataka nitoe ufafanuzi kidogo ili tuweze kufahamiana. Mhe. Salma Mohammed amesema, wananchi wengi tunalipa kodi, lakini wanaofaidika na kodi hii ni watumishi wa umma tu kwa sababu ya mishahara yao ya *hundred and fifty five billion* tulizowawekea na mwaka huu kuna *hundred and eight four billion*.

Mhe. Spika, nataka niseme kwamba wanaolipa kodi hata hawa wafanyakazi wa serikali wanalipa kodi, tena ndio wanaolipa kodi kwa ukamilifu hao, lakini tunafaidika sote, tunajenga skuli tunatumia sote, tunajenga barabara tunatumia sote, tunajenga vituo vya afya tunatumia sote, maji tunakunywa sote, lakini leo usipomuajiri daktari ukamlipa mshahara nikiumwa mimi, nitakwenda wapi? Leo nisipowaajiri walimu nikizaa mtoto nitampeleka akasomeshwe na nani? Kwa hivyo, mimi unayenilipa mshahara ninawatumikia wale ambao hujawaajiri, kwa sababu wanakuja vituo vya afya, wanakuja Hospitali, wanakuja skuli nawasomesha watoto wao. Kwa hivyo, ni muhimu kwamba kodi hizi zinatusaidia sote. Mkulima sasa hivi anapata pembejeo, ndio hizi hizi kodi zetu tunamsaidia na yeye. Kwa hivyo, tunasaidiana na sote tunafaidika na kodi zetu.

Mhe. Spika, Mhe. Abdi Mosi Kombo amesema matatizo makubwa yako katika miundombinu, serikali iyafanyie kazi. Nakubaliana na yeye na ndio maana serikali katika bajeti hii imeweka fedha nyingi kwenye miundombinu kwa sababu ya hilo, tunataka tuondokane na matatizo tuliyonayo kwenye miundombinu yetu.

Mhe. Spika, Mhe. Abdalla Mohamed Ali ameuliza kwamba, je, tumepata gawio kutoka *BoT*? Tumepata 1.8 bilioni. Gawio ni kutokana na faida, faida ikishapatikana 4.5 inakuja Zanzibar, tumepata 1.8 bilioni na zimeshaingia katika hazina zetu.

Mhe. Spika, Mhe. Asha Abdu Haji amesema tutenge fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara, mimi nakubaliana na yeye tutatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara, lakini amezungumzia barabara moja iliyoko Jambiani hii barabara hata Mhe. Jaku Hashim Ayoub anaisemea sana. Nataka nikumbushe tu kwamba barabara haiwezi kujengwa hasa barabara za fukwe, haiwezi kujengwa kama iko ndani ya mita 300 kutoka fukwe. Haya sio ya miundombinu, sio ya Waziri wa Fedha, haya ni ya watu wa mazingira.

Mhe. Spika, kwa hivyo, hiyo barabara yako kama iko ndani ya mita 300 kutoka fukwe, kwa ujumla nazungumza barabara yoyote ile haitaweza kujengwa kulingana na kimazingira barabara ya lami. Kwa hivyo, iangalie vizuri kama iko nje ya mita 300, tutawaagiza watu wetu wa mindombinu ili tuje tuiangalie na watu wa mazingira. Ujenzi wa barabara kwetu sisi ndio muhimu.

Mhe. Spika, Mhe. Suleiman Hemed Khamis, amezungumzia deni la *MECO*, deni hili tunalijua, lakini deni hili lilianzia na mfadhili wa zile barabara za awali, *ADB* tunalijua, lakini tumekubali kulilipa na tunaanda utaratibu wa kulipa deni la *MECO* na tumeshaanza kulilipa sio kwamba hatujaanza tumeshaanza kulilipa.

Mhe. Spika, Mhe. Hija Hassan Hija vile vile, alizungumzia suala zima la *Tanzania Insurance Regulatory Authority* na *Insurance* ya Zanzibar. Akazungumzia vile vigari vidogo, sijui vinaitwa "*Carry"* akasema Zanzibar tunalipa laki mbili na Tanzania Bara wanalipa laki moja. Nataka kusema hili lifahamike ile gari ni moja, ikiwa na matumizi tofauti na bima tofauti, gari ambayo utakayoifanya *Private,* kama umeamua iwe *Private,* maana yake mwenyewe unaondoka hapa unakwenda hapa na watoto ukirudi, *Private* bima yake ni laki moja.

Mhe. Spika, lakini ukiifanya *commercial* kama vi-*carry* vingi vilioko Zanzibar zinapakia mizigo, bima yake ni laki mbili na hivyo wanazo Tanzania Bara na wanazo Zanzibar, hizo *Rate* zote mbili. Sasa kama kuna bima kule Dar -es Salaam ina-*register carry,* lakini kinafanya *commercial* kwa shilingi laki moja, ni kosa. Sasa hii ambayo aliyonayo Mhe. Hija Hassan Hija nitaomba niione hiyo gari kama inafanya *commercial* , tutaifatilia ili tuweze kulirekebisha.

Mhe. Spika, Mhe. Farida Amour Mohammed, kwa nini watumishi wanachelewa kulipwa mafao yao. Nataka niseme utaratibu ni kwamba mtumishi miezi sita kabla hajastaafu na hili Waheshimiwa Wawakilishi nakuombeni sana muwaelimishe watu wenu ndani ya majimbo yenu. Mtumishi miezi 6 kabla hajastaafu anatakiwa aandike barua kueleza kwamba ikifika tarehe fulani, yeye anastaafu. Zianze kutayarishwa zile *Documents* zake na baada ya kukamilika matayarisho yote ya *Documents* zile na kufanyiwa uhakiki kutoka kwenye wizara yake kuja kwa *Auditor in Controller General,* halafu kuna Hazina, ni miezi mitatu anatakiwa alipwe mafao yake na tunatarajia kwamba wale tuliokuwa tunatarajia tuwalipe katika kipindi cha miezi mitatu, kidogo mwezi huu tumechelewa tunaingia kwenye mwezi wa nne.

Mhe. Spika, lakini tunatarajia kwamba kuanza kuwalipa ambao waliokamilisha utaratibu. Kwa hivyo, lengo letu sio kuchelewa hata mimi huwa sifurahi nikicheleweshewa malipo yangu. Lengo letu ni kuwalipa watu wetu *on time* na tutajitahidi tuwalipe *on time,* tunakushukuru kwa kutukumbusha hilo.

Mhe. Spika, Mhe. Rufai Said Rufai, umetaka *X-ray* katika viwanja vya Airport.Tunaanda utaratibu sasa wa kununua *X-ray* mpya, lakini tuna matatizo baadhi yetu hatuna utaratibu wa *Maintenance,* kitu kikishakuharibika inawezekana pesa kidogo tu kutengeneza unakiachia kife ili upate kipya. Jamani tuhimizane katika suala zima la ukarabati. Umesema kiwanja cha ndege hakina magari ya Zima moto, hili nalo tunalifanyia kazi wakati wowote tutamalizana na wale ambao tuliwataka watengeneze hayo magari, tumeshapeleka *Specification* na magari mangapi tunayataka na wameshatuletea *Down Payment,* ni kiasi gani. Kodi za ardhi za mahoteli nimeshaziongelea.

Mhe. Spika, Mhe. Shadya Mohamed Suleiman, amesema bado wapo wafanyakazi hawajapa haki zao ni kweli, lakini watapata. Hakuna mtu ambaye atanyimwa haki yake. Umezungumza vile vile kutoa taaluma kwa wafanyabiashara kabla ya kutumia mashine za kutoza kodi na Mhe. Thuwaybah Kisasi na yeye vile vile amenisisitiza hili. Tutafanya hivyo kwa kushirikiana na wataalamu wetu, lakini uzuri ni kwamba hili jukumu tunalo Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na Wizara ya Biashara tutatoa taaluma hiyo.

Mhe. Spika, Mhe. Salum Abdullah Hamad, alisema kwamba bado hatuko makini katika kukusanya kodi za utalii. Nasema tuko makini kweli kweli kiasi ambacho hatulali katika kuzikusanya, sio za watalii tu, ni kodi zozote zile.

Mhe. Spika, Mhe. Hamad Masoud Hamad, rafiki yangu huyu amasema *paragraph 9,10,11* zisitolewe ni nzuri na zinatioa moyo. Nasema nimeziondoa kwa kuheshimu makubaliano yetu ya kikoa cha Baraza, namuheshimu sana rafiki yangu mpenzi Mhe. Hamad Masoud Hamad, lakini kwa hizi nimeziondoa na nimesema zisiingie kwenye *Hansard* na wala zisijadiliwe nimeheshimu kikao chetu, lakini kama wengine tena hatuheshimu kikoa tena, shauri zenu Mhe. Spika, anakuoneni mimi nimeheshimu kikao. Pia, amesema fomula tuliokubaliana baina ya *ZANTEL* na Mashirika haya ya simu, namwambia fomula bado haijatoka, lakini tumeshakubaliana, tutakubaliana na fomula moja ambayo haitakuwa na hasara kwa upande wetu katika kupata kodi zetu.

Mhe. Spika, vile vile, amesema kuna kero, kuna ada nyingi zinatolewa na Wizara ya Elimu, tumekubaliana baada ya kumaliza kwa bajeti hii, tutakaa na wenzetu wa Wizara ya Elimu tuziangalie ni ada zipi hizo? Kama kuna ada ambazo zinatolewa kulingana na Kamati ya Maendeleo ya Shule, hizo ni zenu nyinyi Wawakilishi na Wabunge, shule zimo ndani ya majimbo yenu kama mna Kamati ya maendeleo ya Shule na ada zenu, hizo ni zenu nyinyi huko, kama kuna ada ambazo ziko ndani ya Serikali Kuu na zinatozwa ndani ya Wizara ya Elimu, tutaziangalia na tutaanda utaratibu tukishirikiana na Waziri wa Elimu kama tulivyoshirikiana kwa ile ada ya mtihani tukaiondoa, tutaziangalia hizo.

Mhe. Spika, Mhe. Mohammed Said Mohammed, amesema wananchi wapewe taarifa juu ya bajeti asilia. Tutatoa taarifa na kila mmoja aweze kufahamu, lengo letu hasa tunataka tuanze pale ambapo tulipopata fedha, sio tuanze pale ambapo tulipojipangia tunahitaji kiasi gani. Nakushukuru vile vile Mhe. Naibu Waziri kwa kutoa ufafanuzi katika sekta yako ya Uvuvi na Mifugo.

Mhe. Spika, Mhe. Mussa Ali Mussa, nakushukuru umeeleza jinsi ya miundo mbinu ilivyoimarika na hizi ndizo kodi ambazo nimezizungumza hapa.

Mhe. Spika, Mhe. Bikamae Yussuf Hamad, amesema kwamba tuangalie muhimili wa tatu wa Mahakama. Lengo letu mihimili yote mitatu kwa sababu inafanyakazi kwa ushirikiano kwa pamoja tutaiangalia yote iweze kufanya kazi na kushirikiana.

Mhe. Spika, Mhe.Assa Othman Hamad, bado wananchi wanahangaishwa na uchumi. Nakubaliana na wewe tutahangaika na ndio lengo la wananchi lazima tuhangaike na uchumi, tujitume na tufanye kazi ili uchumi huu uweze kukuwa. Ukijifungia ndani hakikisha kwamba hutapata chochote, lazima tutoke tukafanye kazi. Umeeleza kwamba afya binaadamu ni muhimu katika kujenga uchumi na nimeiweka kama kibwagizo, umezungumzia suala la pencheni la wazee ni ndogo, lengo letu ni kuziongeza hizi pencheni za wazee na Mwenyezi Mungu akitujaalia tutaziongeza, sio katika mwaka huu wa bajeti, lakini tunaliangalia kwa kipindi kijacho.

Mhe. Spika, Mhe.Shamsi Vuai Hahodha, ameeleza naomba na mimi niunge matumizi ya *SDL*, amesema yanakwenda kinyume na sheria. Nataka niseme tu kwamba mwanzoni tulipotunga Sheria ya *SDL* ilikuwa ni kwa matumizi ya Elimu ya Amali kuongeza ujuzi kama alivyosema Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, lakini baadae Mheshimiwa, sheria ile ilifanyiwa marekebisho ikasogea zaidi kui-*cooperate* wanafunzi wa vyuo vikuu na ukitizama kuanzia mwaka 2006 serikali imechangia karibu bilioni 23 kwenye Elimu ya Juu, lakini kwa bahati mbaya *Collection*, yaani *Return* ni kama milioni 300 tu. Kwa hivyo, tukaona ni vyema tukaongeza hizi fedha tukazigawa Elimu ya Juu, tukawapa *share* ya asilimia 60 na amali ikapewa asilimia 40.

Mhe. Spika, kwa hivyo, ni sahihi unaposema pale mwanzo ilikuwa ni kwa ajili ya kuongeza ujuzi, lakini baadae ilipofanyiwa marekebisho hii sheria sehemu za zile fedha ziende kwa Elimu ya Juu na sehemu ziende katika kuongeza ujuzi. Kwa hivyo, sasa hatujakosea hatuzitumii kinyume cha sheria.

Mhe. Spika, lakini vile vile, umesema kwamba huu ni mfumo nataka nisahihishe kidogo, ni kwamba hii ni *level* sio mfuko. Kwa hivyo, kila mwaka makusanyo yake sasa hivi nadhani kila mwezi zinapatikana kama sitokosea, ukichukua ile asilimia 5 ya mshahara wa mfanyakazi, kila mwezi inapatikana kama milioni mia saba au minane, hivi zinagawai 60% zinakwenda Elimu ya Juu na 40%, zinakwenda katika Elimu ya Amali. Kwa hiyo, hii ni *level* ambayo inatumia kila mwaka zikipatikana zinagaiwa, hakuna mfuko kwamba tunaziweka. Nilikuwa naomba tu kidogo Mhe. Shamsi Vuai Nahodha nikupe hiyo taarifa.

Mhe. Spika, Mhe. Ali Abdalla Ali, ambaye aliuchangia kwa maandishi na yeye alizungumzia suala la uendelezaji wa viwanda. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame amelizungumzia vizuri sana, lakini na mimi nataka niseme kwamba

tutaendelea kushajihisha wawekezaji wa ndani na nje wawekeze kwenye viwanda. Tatizo tulilonalo kwa wawekezaji wetu wa ndani wengi hawaekezi kwenda wanaekeza kwenye biashara ya kuuza na kununua. Tutawashajihisha waelekeze huko kwa sababu sasa hivi kuna faida kubwa sana.Tutanue wigo wa mapato hasa tutakapojenga Bandari mpya. Mimi nakubaliana na wewe, tuimarishe huduma za wazee, watoto, watu wenye ulemavu, tutaziimarisha na kuimarisha huduma zote za jamii. Tutafanya hivyo Mheshimiwa.

Mhe. Spika, Mhe. Mahmoud Thabit Kombo, nadhani huyu atakuwa wa mwisho. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo, amechangia kwa maandishi na mambo mengi sana ameniletea, mengi tumeyachukuwa tutayafanyia kazi, lakini ya msingi ambayo nataka ni ya *highlight* hapa kila mmoja aweze kuyasikia, la kwanza na mimi nakubaliana na yeye amesema hivi:-

(1) Kama tunaiona sekta ya huduma ina mchango asilimia 44 kwenye *GDP*, kwa nini sisi kama serikali hatuichangii zaidi na hili ndilo tunalolifanya kwenye karafuu? Tunasema karafuu ni uti wa mgongo. Tumefanya maamuzi ya makusudi kuendeleza mkarafuu Wizara ya Biashara, Wazira ya Kilimo wote wanaelewa maamuzi ya makusudi kuendeleza mkarafuu. Sasa nasema Mhe. Mahmoud Thabit Kombo, kwa nini sasa hatui-*jet more* katika sekta ya huduma. Tumelipokea na tutaangalia tuna-*contribute* kiasi gani kwenye sekta hizi za huduma kwa maana sekta ya utalii na sekta nyengine ambazo zinazo-*cover* sekta ya huduma *Bank System, Finacial System* zote tutaziangalia kwa pamoja ili tuone *what is the contribution for the Government?* Tutaangalia.

(2) Anasema kwamba tumeshaanza kuona misaada hii inapungua kutoka kwa Washirika wa maendeleo, tumejipangaje ? *Is a Government*. Hili ndio lile ambalo limeulizwa na Mhe. Omar Ali Shehe tutaondokaje katika kujitegemea, misaada inapungua, tunajipangaje serikali? Mpango wetu mkubwa njia zote ambazo tutakazoona kwamba miradi yote ambayo tutakayoona hii itaweza kuchangia kutupatia mapato zaidi tunataka tuikamilishe. Uwanja wa Ndege *Terminal* ikimalizika ya Unguja, itaweza kushughulikia wasafiri zaidi ya milioni mbili.Tunakimbilia kwenye Bandari ya Mpigaduri,Uwanja wa Pemba, *Irrigation*, hizi sekta ambazo tunaona kwamba zinaweza zikaja kutusaidia tunataka tuzifanyie kazi haraka sana ili ziweze kutusaidia wakiondoka hawa ili na sisi tuweze wenyewe, lakini vile vile tuna-s*truggle* na Mhe. Mahmoud Thabit Kombo unafahamu ili tupate nafasi tuanze kuchimba mafuta na gesi, tukifanikisha hapo, basi tumeondokana na huo utegemezi na sisi, lakini ni nzuri angalau umetushitua.

(3) Lakini la mwisho ambalo Mhe. Mahmoud Thabit Kombo, umetuuliza Taasisi za Kidini na *NGO's* kupata misamaha. Nataka niseme tu kwamba Taasisi za Kidini na *NGO's* nazo vile vile huwa tunazipa msamaha inategemea na ule msamaha ambao walioomba, kwa mfano kama Taasisi ya Kidini inataka kujenga msikiti au inataka kujenga kanisa huwa tunatoa msamaha kwa baadhi ya vitu ambavyo wanavyoletewa kutoka nje kwa ajili ya ujenzi wa taasisi zao.

Vile vile, kama *NGO's* wanataka kujenga Daghalia katika shule fulani ambayo shule hiyo haiendeshwi kibiashara tunasaidia vile vile kuwapa hizo *Exemption*, lakini *Exemption* zinatolewa baada ya wizara inayohusika ku-s*atisfy*. Wizara ya Elimu lazima i-*satisfy* kama kweli Daghalia hili litajengwa katika Shule ya Kiembesamaki, Wizara ya Afya lazima wa-*satisfy* kwamba kweli vitanda hivi vinakwenda Hospitali ya Kiwengwa tunatoa misamaha ya kodi.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, sasa nataka niseme jambo moja la mwisho kabisa ili nitoe hoja. Mwaka jana tulipitisha bajeti yetu shilingi bilioni 658.5 na hii ni hesabu nyengine, naomba ndugu zangu wainukuu bajeti asilia. Tulipitisha shilingi bilioni 658.5 bajeti yetu, lakini mpaka kukifika tarehe 30 Juni tutatumia shilingi 552.9 bilioni. Wengine walihoji, nataka nitoe ufafanuzi kidogo kwa nini hatutofikia kile kiwango?

Mhe. Spika, la kwanza, tumeisimamisha kuendelea kwa muda *Terminal Building* ya *Airport* kwa sababu ilikuwa ina matatizo matatu muhimu, lazima tuyasawazishe matatizo hayo na muda tuliosimamisha karibu mwaka mmoja, laiti ingekuwa hatujasimamisha ile *Terminal*, tungeweza kutumia dola milioni 35 sawa na bilioni 56, zingeweza kuingia kwenye 552.9 *plus* hizo.

Mhe. Spika, la pili, tumezisimamisha kwa muda barabara za Pemba, laiti ingekuwa hatujaweza kuzisimamisha na kutatua matatizo ya msingi yaliyopo tungeweza kutumia zaidi ya dola milioni karibu 20, katika kipindi hiki tulichozisimamisha karibu bilioni 32. Ukizijumlisha hizo ni bilioni 640.9, tofauti yetu 658 na 640 ingekuwa ni ndogo. Kwa ndugu zanguni tusione kwamba hatujafanya kazi ya kutafuta mapato, tumefanya kazi ya kutafuta

mapato, lakini kuna mambo ilibidi tuyasimamishe kwa sababu za msingi tunataka kitu kizuri tukipate kutokana na fedha zetu *value for money*. Tofauti ingekuwa *just* bilioni 17.6 tu, wala sio pesa nyingi kama hivi ambavyo tunavyoiona sasa hivi.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, namalizia kwa kuwashukuru tena sana Waheshimiwa Wawakilishi kwa kazi nzuri waliyoifanya kwa kunisaidia mimi na watendaji wangu katika kulitumikia Taifa letu hili. Nawaomba wasichoke kama kuna hoja yoyote tuizungumze kwa faida ya nchi yetu na faida ya wananchi wetu.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kutoa hoja. Ahsante sana.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Fedha kwa majumuisho hayo. Sasa Waheshimiwa Wajumbe naomba niwahoji wale wanaokubaliana na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kazi za Kawaida na Maendeleo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka 2014/2015 wanyanyue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Nakushukuruni sana na sasa tunaendelea.

MISWADA YA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Kutoza Kodi na Kubadilisha Baadhi ya Sheria za Fedha na Kodi Kuhusiana na Ukusanyaji na Udhibiti wa Mapato ya Serikali

(Kusomwa kwa mara ya kwanza)

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima naomba kusoma kwa mara ya kwanza Mswada wa Sheria ya Kutoza Kodi na Kubadilisha Baadhi ya Sheria za Fedha na Kodi Kuhusiana na Ukusanyaji na Udhibiti wa Mapato ya Serikali na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mswada umesomwa kwa mara ya kwanza na kama tunavyoelewa miswada ya aina hii husomwa kwa mara ya kwanza, mara ya pili na mara ya tatu yote inafanyika katika mkutano huo huo.

Mswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2014

(Kusomwa kwa mara ya pili)

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Spika, Sheria ya Kutoza Kodi na Kubadilisha Baadhi ya Sheria za Fedha na Kodi Zinazohusiana na Ukusanyaji na Udhibiti wa Mapato ya Serikali ya mwaka 2014 inakusudia kufanya mabadiliko katika sheria mbali mbali kwa lengo la kudhibiti na kukusanya mapato. Aidha, mswada huu unaopendekezwa umefanya marekebisho kwa sheria zinazosimamiwa na Bodi ya Mapato Zanzibar na sheria nyengine zinazohusiana na mapato ikiwemo Sheria ya Rufaa za Kodi Nam. 1 ya mwaka 2006, Sheria ya Usafiri Baharini Nam. 7 ya mwaka 2003 na Sheria ya Kazi Nam. 11 ya mwaka 2005. Sheria za Bodi ya Mapato Zanzibar zilizofanyiwa marekebisho ni kama zifuatazo:-

1. Sheria ya Usimamizi wa Kodi Nam. 7 ya mwaka 2009.
2. Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani Nam. 4 ya mwaka 1998.
3. Sheria ya Kodi ya Mafuta Nam. 7 ya mwaka 2001.
4. Sheria ya Bodi ya Mapato Nam. 7 ya mwaka 1996.

Mhe. Spika, kutokana na kuongezeka majukumu ya serikali na kwa lengo la kuongezeka usimamizi wa mapato na matumizi ya serikali ambayo yamekuwa yakiongezeka kila baada ya muda, Wizara ya Fedha imeona kuna umuhimu wa kufanya mabadiliko ya sheria mbali mbali zinazohusiana na ukusanyaji wa mapato. Hatua hiyo itatoa fursa ya

kuweka misingi na kufanya mabadiliko kutokana na mabadiliko ya hali ya uchumi na mfumo wa biashara ulivyo Zanzibar.

Mhe. Spika, waraka huu una madhumuni ya kuwasilisha Rasimu ya Mapendekezo ya Mswada wa Sheria ya Fedha na kubadilisha baadhi ya Sheria za Fedha na Kodi zinazohusiana na ukusanyaji na udhibiti wa mapato ya serikali ya mwaka 2014.

Muhtasari wa Mswada

Mhe. Spika, mswada huu wa sheria umegawika katika sehemu 8 ambapo sehemu ya kwanza ya mswada inahusiana na vifungu vya utangulizi ambavyo vinaeleza jina na sheria na utumiaji wa sheria. Sehemu ya pili ya mswada inahusiana na marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Kodi Nam. 7 ya mwaka 2009 ambayo inafanyiwa marekebisho ya vifungu vifuatavyo:-

1. Kifungu cha 3 kwa kuongeza maana ya maneno wakala wa kuzuia kodi ili kutoa mamlaka kwa Kamishna kuteua wakala wa kuzuia kodi na kuiwasilisha moja kwa moja *ZRB.*
2. Kubadilisha muda wa kuwasilisha *return* kutoka siku 15 kuwa siku 7 katika kifungu cha 18.
3. Kifungu cha 22 kinafanyiwa marekebisho kwa kufanya marejeo sahihi.
4. Kubadilisha muda wa malipo kutoka siku 25 na kuwa siku 15 ili kupunguza walipa kodi kukaa na pesa za serikali muda mrefu na kupata muda zaidi wa ufuatiliaji katika kifungu cha 31.
5. Kufuta kifungu cha 36 na kuweka kifungu kipya cha 36 kinachozungumzia marejesho ya kodi.Lengo ni kuwa na utaratibu maalum wa kurejesha fedha kama sheria za kodi zinavyoeleza.
6. Kwa kuweka marejeo sahihi katika kifungu cha 41.
7. Kwa kuweka wazi uwezo wa Kamishna wa kufunga biashara katika kifungu cha 43.
8. Kuweka wazi nyaraka zinazohitajika katika usafirishaji wa mizigo katika kifungu cha 5.
9. Kuweka kifungu kipya cha 54 (a) ili kutoa wajibu wa mtu mwengine katika kulipa kodi, Lengo ni kuwafanya watu wenye majukumu katika usimamizi wa biashara wawajibike katika ulipaji wa kodi.
10. Kifungu cha 56 kwa kufuta kifungu kidogo cha 1 na kuongeza kifungu kidogo kipya cha 6 kinachokataza kukata rufaa iwapo mlipa kodi au mtu yeyote amekubali kumaliza makosa.
11. Kifungu cha 62 kwa kuweka wazi maelezo ya uwakilishi katika kulipa kodi.
12. Kuongeza kifungu cha 62 (a) ili kuwatambua washauri wa kodi.
13. Katika kifungu cha 68 kwa kuongeza kifungu kidogo cha 2 kitakachompa uwezo Kamishna wa kuzuia chombo katika kulinda mapato ya Serikali.

Mhe. Spika, sehemu ya tatu ya mswada inafanyia marekebisho Sheria ya Kodi ya Mafuta Nam. 7 ya mwaka 2001 kwa kufanyia marekebisho kifungu cha 13 kifungu kidogo 7 ili kumpa mamlaka Kamishna kuzuia vyombo mbali mbali vinavyotumika kupakia au kusafirisha mafuta ya magendo.

Mhe. Spika, sehemu ya nne ya mswada inaweka marejesho ya Sheria ya Ongezeko la Thamani Nam. 4 ya mwaka 1998 kwa kufuta tafsiri ya neno Wakala wa Kuzuia Kodi na tafsiri hiyo imeshajumuishwa katika Sheria ya Usimamizi wa Kodi Nam. 7 ya mwaka 2009. Pili, kurejesha kifungu cha 26 (a) kwa kuondoa uwezo wa Waziri kutunga Kanuni za Washauri wa Kodi mamlaka ambayo yamezingatiwa katika Sheria ya Usimamizi wa Kodi Nam. 7 ya mwaka 2009.

Mhe. Spika, sehemu ya tano inafanyia marekebisho Sheria ya Bodi ya Mapato Zanzibar Nam. 7 ya mwaka 1996 katika sehemu hii.

1. Kifungu cha 5 kimerekebishwa namba ili kuweka vyema marejeo.
2. Kifungu 15 cha kurekebisha kifungu kidogo cha 3 ili kutoa uwezo kwa Kamishna kukasimu baadhi ya kazi zake kwa maofisa wa juu wanaomsaidia kiutendaji.
3. Kifungu cha 15 (a) kuweka jina sahihi la Bodi ya Mapato Zanzibar na kufuta kifungu kidogo cha 3 kilichopo na kuweka kifungu kipya cha 3 ili kumpa uwezo Naibu Kamishna kutekeleza majukumu yake yaliyoelezwa katika Sheria ya Kodi.
4. Kifungu cha 26 kwa kuweka marejeo sahihi.

Mhe. Spika, sehemu ya sita ya mswada inaweka marekebisho ya Sheria ya Rufaa za Kodi Nam. 1 ya mwaka 2006 katika vifungu vifuatavyo:-

1. Kufanyia marekebisho kifungu cha 4 kifungu kidogo 2 kwa kuanzisha nafasi ya Makamu Mwenyekiti ili kutoa uwezo wa kuendeshwa mashauri ya kodi pale Mwenyekiti atakapokuwa hayupo au itakapojitokeza kuwepo kwa mashauri mengi ya kodi.
2. Kifungu cha 5 kuweka uwezo zaidi wa Bodi ya Rufaa za Kodi pekee.
3. Kifungu cha 15 kwa kuweka marejeo sahihi.

Mhe. Spika, sehemu ya saba ya mswada inafanyia marekebisho Sheria ya Usafiri Barabarani Nam. 7 ya mwaka 2003 katika kifungu cha 86 (1) kwa kuongeza muda wa kutoa leseni za udereva kuwa ni miaka miwili hadi mitano. Lengo ni kupunguza gharama za uendeshaji na kutoa muda zaidi wa kuwa na leseni ya udereva.
Mhe. Spika, sehemu ya nane ya mswada inafanyia marekebisho Sheria ya Ajira Nam. 11 ya mwaka 2005 kwa kufanya marekebisho katika kifungu cha 40 kwa kutaka mgeni asipewe ruhusa ya kufanya kazi hadi atakapowasilisha hati za kutokudaiwa kodi ya mapato, ili kuhakikisha kwamba walipa kodi wa kigeni wanalipa kodi na mapato yao yanadhibitiwa. Pili, kifungu cha 68 (1) kwa kuweka masharti ya mishahara ya wafanyakazi kulipwa kupitia benki zilizopo nchini ili kuepusha baadhi ya wafanyakazi wa kigeni kulipwa mishahara yao katika akaunti zilizo nje ya nchi.

Mhe. Spika, kutokana na umuhimu wa mswada huu kama ni chachu ya kuongeza uwezo wa kusimamia mapato ya serikali, tunashauri mapendekezo haya yajadiliwe na kikao chako ili tuweze kuyapitisha siku hii ya leo.

Mhe. Spika, Waheshimiwa Wajumbe, nawaomba kuyatafakari vizuri mapendekezo ya mswada huu ili waweze kuyapitisha hapo jioni ya leo.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, hoja imetolewa ingawa amesema anawasilisha, lakini hoja imetolewa na kuungwa mkono.

Mhe. Hamza Hassan Juma (Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti): Mhe. Spika, na mimi kwa mara nyengine tena napenda nikushukuru kunipa nafasi hii, nikawa mtu wa mwanzo kuweza kuchangia mapendekezo ya Kamati ya Wenyeviti ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar kuhusu Mswada wa Sheria ya Kutoza Kodi na Kubadilisha Baadhi ya Sheria za Fedha na Kodi Kuhusiana na Ukusanyaji na Udhibiti wa Mapato ya Serikali na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, kabla sijaanza kuchangia mswada huu nilikuwa nawaomba sana Wajumbe wenzangu mswada huu ni muhimu sana, lakini mswada huu kuuchangia vile vile ni mgumu sana, kwa sababu mswada huu unarekebisha sheria mbali mbali za kodi. Sasa tayari tumeshapitisha Bajeti ya Serikali ambayo kama hatujaweza kuchangia vizuri na tukaboresha na tukamruhusu Mhe. Waziri kwenda kukusanya hizo kodi, basi ile bajeti ambayo tumeipitisha kwa kweli haitokidhi haja. Kwa sababu fedha hizo ambazo ameziomba Mhe. Waziri, ndio zimo katika mswada huu.

Mhe. Spika, Waheshimiwa Wajumbe, sasa mimi nitawaomba sana mswada huu pamoja na kwamba umechanganya sheria nyingi, lakini tuangalie yale maudhui yake na ili tuweze sasa kumsaidia Mhe. Waziri kumpa ushauri wa ziada na kuweza kwenda kufanya kazi yake vizuri.

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo, sasa naanza moja kwa moja kuja katika marekebisho ambayo Kamati yangu ya Wenyeviti iliyafanya tulipokuwa na timu ya Mhe. Waziri wa Fedha.

Mhe. Spika, kwanza Kamati yangu imeweza kufanya marekebisho katika jina la mswada ambao huo mliokuwa nao Wajumbe. Sasa hivi tunapendekeza jina la mswada lifanyiwe marekebisho na lisomeke kwamba Mswada wa Sheria ya Kutoza na Kurekebisha baadhi ya Kodi na Ushuru na Kubadilisha Baadhi ya Sheria za Fedha na Kodi kuhusiana na Ukusanyaji wa Udhibiti wa Mapato ya Serikali pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Hayo ndio marekebisho ya mwanzo ambayo tumeyafanya katika jina la mswada, lakini vile vile kifungu cha 4 cha mswada tumekifanyia marekebisho na tunaomba kisomeke kama hivi ifuatavyo:-

1. Katika aya ya (a) mstari wa pili kutoka juu neno "kijifungu" lisomeke "kifungu" na kila inaposomeka neno "kifungu" katika mswada huu, basi neno hilo lisomeke "kifungu".
2. Katika kifungu kidogo cha (b) mstari wa pili kutoka juu yaongezwe maneno katika kifungu kidogo cha 3.
3. Kifungu cha 7 (4) cha mswada tumekifanyia marekebisho na katika mstari wa 3 kutoka juu kwa kufutwa neno "amabacho" na kuweka neno "ambacho". Hapa ilikuwa ni *just typing error*. Lakini kifungu cha 9 kamati yangu imeweza kufanya marekebisho au inaomba kufanya marekebisho kama hivi ifuatavyo. Kwa kuzifanyia aya ya 1 na aya 2 zisomeke kuwa ni aya (a) na (b), badala ya namba isomeke tarakimu.

Katika aya ya 1 kwenye maelezo ya aya hiyo, herufi (a) isomeke (d). Lakini ya tatu kwa kuongeza aya mpya ya kifungu kidogo cha (c) ambacho kinasomeka kama ifuatavyo, kuongeza maneno ya "mlipa kodi", badala ya maneno sababu zinazokubalika na atakataa katika aya ya (c).

Mhe. Spika, kifungu cha 10 cha mswada tunaomba kufanya marekebisho kama hivi ifuatavyo. Katika aya (a) mstari wa pili kutoka juu yaongezwe maneno, "malipo ya fedha taslimu" baina ya neno malipo na au. Vile vile katika mstari wa nne kutoka juu yaongezwe maneno, "malipo ya fedha taslimu" badala ya neno "malipo".

Lakini 2 katika aya ya (b) mstari wa pili kutoka juu yaongezwe maneno, "au malipo ya fedha taslimu" baina ya neno "Forodha na au".

Marekebisho ya sita kifungu cha 11 cha mswada tunaomba kufanya marekebisho kama hivi ifuatavyo. Kwa kufutwa maneno, "anayehusika" yaliopo kwenye mstari wa nne kutoka juu na kusomeka, 'anayehusika". Namba mbili kwa kufutwa maneno, "ifahamike" iliopo katika mstari wa tano kutoka juu baina ya neno, "isipokuwa na kwamba". Kwa kuongeza neno mengine baina ya neno, "yake" na anayotakiwa yaliopo katika kifungu cha 54 (a) kinachopendekezwa katika mswada.

Lakini saba kigungu cha 12 (b) cha mswada tunaomba kifanyiwe marekebisho kama hivi ifuatavyo. Kwa kuongeza nyuma ya aya (d) ikae sawa na aya (a) kwa lengo la kusomeka vyema. Neno, "awingiza" lisomeke "kwa kuingiza".

Marekebisho ya nane, kifungu cha 18 cha mswada ambacho kinazungumzia kifungu cha 62 (2) cha sheria mama tumekifanyia marekebisho na tunaomba kisomeke kama hivi ifuatavyo. Kwa kufutwa neno, "kifunguu" na lisomeke, "kifungo". Mbili kwa kuongezwa maneno "kwa maandishi" mwisho mwa aya (a), (b), (c) na (d) kwa kuongezwa neno, "au aya (d)".

Mhe. Spika, kifungu cha 24 (a) cha mswada tunaomba kifanyiwe marekebisho kwenye mstari wa kwanza kutoka juu kwa kufutwa neno "kwa" liliopo baina ya neno, "cha" na mabano moja.

Marekebisho ya 10 tuliyoyafanya kifungu cha 27 cha mswada tunaomba kifanyiwe marekebisho kama hivi ifuatavyo kwa kuzifanyia aya 1, 2 na 3, zisomeke kuwa aya za (a), (b) na (c).

Marekebisho ya pili katika kifungu hiki cha 27, tunaomba aya (a) isomeke (a) (i). Na marekebisho ya tatu katika kifungu hiki aya ya (1) na (b) isomeke (a) na (ii). Na nne, aya tatu (a) isomeke kifungu kidogo cha (c) (i) na marekebisho ya tano naomba yasomeke aya ya tatu (d) isomeke aya ya (c) (2).

Mhe. Spika, haya ndio marekebisho ambayo tumeyafanya kwenye kamati. Sasa nilikuwa ninaomba moja kwa moja nije katika ufafanuzi wa haya marekebisho ambayo Mhe. Waziri aliyoyaleta kwenye mswada huu wa sheria.

Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena ninataka nimshukuru sana Mhe. Waziri wa Fedha pamoja na watendaji wake wote walioshiriki kuandaa mswada huu kwa ufafanuzi mzuri walioutoa mbele ya kamati yetu, na mpaka sisi tukapata uelewa na kuleta mapendekezo haya tuliyoyawasilisha hapa.

Mhe. Spika, pia ninapenda niendelee kuwashukuru tena wenyeviti wenzangu wa kamati kwa kuendelea kunivumilia kwa kunipa mashirikiano makubwa wakati wote tunapokuwa kwenye kazi za kamati yetu ya wenyeviti.

Mhe. Spika, kama alivyoeleza kwenye hotuba yake Mhe. Waziri kwamba anaomba tumruhusu afanye marekebisho katika sheria mbali mbali kwa lengo la kudhibiti na kukusanya mapato. Mswada huu zaidi unakusudia kufanya

marekebisho ya sheria zinazosiamiwa na Bodi ya Mapato ya Zanzibar, na sheria zinazohusiana na mapato ikiwemo Sheria ya Rufaa ya Nam.1 ya 2006, Sheria ya Usafiri wa Barabarani Nam. 7 ya 2003 na Sheria ya Kazi Nam. 11 ya 2005 kama alivyoeleza Mhe. Waziri wa Fedha wakati akiwasilisha mswada wake.

Mhe. Spika, kama alivyoeleza Mhe. Waziri kuwa mswada huu una sehemu nane na mimi nitaeleza tu madhumuni na pia kutoa ushauri kwa serikali katika maeneo hayo, ili kuweza kuyaboresha marekebisho katika vifungu mbali mbali. Katika marekebisho ya kifungu cha 3 ilikuwa ni kuweka tu sawa tafsiri ya kifungu ili kiweze kwenda na wakati na mahitaji ya sheria inayotaka.

Mhe. Spika, marekebisho ya kifungu cha 18, kimekusudia kupunguza muda wa mlipa mkodi ili asikae na fedha za serikali kwa muda ili kufanya serikali kuweza kukusanya fedha ilizojipangia kwa wakati, ili kuweza kutekeleza majukumu kama ilivyoidhinishwa na Baraza lako tukufu la Wawakilishi, na kuleta ufanisi uliokusudiwa.

Mhe. Spika, vile vile marekebisho ya kifungu cha 22 yamekusudia kumpa nguvu Kamishna ili kuidhinisha mabadiliko yote yaliyofanywa ili kuziba mianya ya udanganyifu unaoweza kutokea bila ya Kamishna kujua. Kwa hivyo hapa kamati yangu imeridhika na sasa kweli serikali yetu imeanza kusikia kile kilio chetu cha muda mrefu cha Wajumbe kudhibiti mianya na upotevu wa mapato ya serikali.

Mhe. Spika, marekebisho ya kifungu cha 31 ya kifungu hiki vile vile kimekusudia kupunguza muda wa mlipa mkodi wa kukaa na fedha za umma kwa muda mrefu ili kuleta ufanisi wa kazi serikalini. Kamati yangu katika hili inaungana na Mhe. Waziri na kuongeza ufanisi wa ulipaji kodi serikalini.

Mhe. Spika, marekebisho ya kifungu cha 36 yamekusudia kumpa nguvu za kisheria Kamishna wa Bodi ya Mapato ili aweze kurejesha malipo ya mlipa kodi aliyelipa kimakosa kwa kodi ambayo hakupaswa kuilipia hapo kabla. Hapo kabla hakukuwa na sheria iliyompa mamlaka Kamishna kumrejeshea malipo mlipa kodi aliyelipa kodi kimakosa serikalini.

Mhe. Spika, pamoja kwamba jambo hili lilikuwa likifanywa kihalali lakini ni kinyume cha sheria. Kwa kuwa sheria haikuwepo jambo hili ambalo lingeweza kumtia matatani Kamishna bila ya sababu yoyote. Kwa hivyo ili kumlinda Kamishna basi ni vyema kukiweka kifungu hiki cha kisheria ili kiweze kuwepo kisheria zaidi.

Mhe. Spika, marekebisho ya kifungu cha 41 ni marekebisho ya kuongeza maneno tu lakini kifungu hakijabadilika kama, kamati yangu imeridhia. Pia marekebisho ya kifungu cha 43 yanakusudia kumpa mamlaka Kamishna kuweza kufunga na kuweka nakiri aidha katika ghala au jengo lolote ili kumbana mlipa kodi kutoa maelezo ya ushahidi kwa mali yoyote iliyotiliwa mashaka aidha kwa udanganyifu wa aina yoyote au kutaka kuficha taarifa sahihi za malipo ya kodi iliyostahili kulipwa kupitia bidhaa hiyo.

Mhe. Spika, marekebisho ya kifungu cha 51, yanakusudia kudhibiti usafirishaji wa bidhaa bila ya kuwa na stakabadhi zinazohusika hasa kwa kuzingatia binadamu ni wajanja na wanaweza kushirikiana na watoza kodi. Aidha, bandari au viwanja vya ndege kwa kukwepa kulipa kodi ya serikali. Lakini bado Kamishna atakuwa na uwezo wa kuisimamisha gari au chombo chochote kilichobeba mzigo ili kudai ankara ya malipo, aidha kodi ya forodha ambayo mwanzo haikutajwa kwenye sheria.

Kamati yangu imeridhia suala hili, kwani hasa kwa hivi sasa kutokana na bandari yetu kutokuwa na nafasi ya kutosha, basi kuna bidhaa nyingi ambazo hutolewa kwenye makontena kutoka bandari na kuweza kusababisha ukwepaji wa kodi kulipwa kodi ya serikali.

Mhe. Spika, marekebisho ya kifungu cha 54, kamati yangu imeridhia marekebisho hayo kwani kumekuwa na ujanja baadhi ya wanaopewa dhamana kwenye makampuni na kusababisha hasara na pengine kupelekea makampuni haya kufilisika, na baadae watu hao kuanzisha kampuni nyengine huku mwanzo wakiwa wamebakisha madeni makubwa ya serikali yakiwa hayajalipwa. Kwa hivyo Kamishna ataweza kwa sasa kumshika muhusika huyu kulipa deni lile yeye mwenyewe binafsi au kampuni yenyewe kwa masuala kama haya yanapotokea.

Masuala kama haya tumeshayashuhudia kwenye uwekezaji mkubwa wa mahoteli hapa Zanzibar. Baadhi ya wawekezaji huuza mahoteli yao na kuwauzia wengine na baadae kuanzisha makampuni na wengine kubadilisha utawala. Lakini ukirudi kuyachunguza ni hayo hayo, wamejificha mgongoni kwa makampuni hayo.

Mhe. Spika, na hapa tunaiomba serikali kuhakikisha sio inasimamia ulipaji wa kodi ya serikali tu bali hata wananchi ambao waliuza bidhaa katika mahoteli hayo, kuhakikisha kwamba wanasimamia madeni ya wananchi hao ambao kwa hivi sasa kuna ushahidi wa kesi nyingi zipo katika vituo vya Polisi au Kamisheni ya Kazi. Nao Kamisheni ya Utalii, ambapo vijana wetu wametumia pesa zao nyingi na nyengine wamekopa kwa ajili ya ku-*supply* bidhaa mbali mbali kwenye mahoteli na wawekezaji baadae wakauza mahoteli hayo kwa watu na kubadilisha majina, uongozi ya mahoteli hayo. Lakini hadi leo wameshindwa kuwalipa pesa zao na kuwaacha vijana wetu na madeni makubwa na kuwafilisi mitaji yao na kuwadhoofisha maisha yao na familia zao. Kwa hivyo ninadhani ipo haja kuongeza kifungu chengine cha sheria kitakachoweza kumpa mamlaka Kamishna kupokea malalamiko ya wananchi kuhusu madeni yao na kuweza kuwa wakala wa kuwakusanyia na kuwalipa wananchi hao.

Mhe. Spika, isitoshe ipo haja ya serikali kuleta sheria ya kuwalazimisha wawekezaji wenye mahoteli kuweza kufunga mikataba na wasambazaji wa bidhaa mahotelini, yaani *suppliers* ili kuweza kuwalipa kwa wakati vijana wetu. Kwani wengine hufika miezi sita kusambaza hizo bila ya malipo yoyote, wakati bidhaa zao hizo huwa tayari zimeshatumika katika mahoteli hayo kwa muda mrefu uliopita.

Kwa kuwa sisi Waheshimiwa wao tumeshindwa kuwalinda kwenye ajira yao hii, basi wananchi wetu hao huendelea kusumbuliwa na wawekezaji hao bila ya kupata msaada wowote wa serikali. Mfano mzuri ni aliyekuwa mwekezaji wa hoteli ya *VENTA CLUB* kule Kiwengwa ambaye amechukua mali za watu na kuacha wananchi na madeni makubwa hadi leo, wengine wamefilisika na hakuna msaada wowote ambao wanaupata kutoka serikalini.

Mhe. Spika, kamati imeridhika na marekebisho yaliyopendekezwa kwa kumpa uwezo Kamishna kumtoza faini mlipa kodi yeyote ambaye amekiri kufanya kosa na kukwepa kodi ya serikali. Kwa uamuzi wa Kamishna kuwa ni wa mwisho na hautoweza kukatiwa rufaa kwenye Mahakama Kuu. Hii itarahisisha kuharakisha ulipaji wa kodi wa serikali bila ya kupelekana Mahakamani, kwani kodi hiyo kila ikichelewa kulipwa kwa wakati basi husababisha usumbufu mkubwa kwa upatikanaji wa fedha zinazolengwa katika kukusanywa wakati huo serikalini.

Mhe. Spika, marekebisho ya kifungu cha 62, kamati yangu imeyaridhia kuwa inamrahisishia mlipa kodi kumuidhinisha mtu yeyote ili kusimamia malipo ya kodi yake serikalini bila ya usumbufu wowote. Jambo ambalo litasaidia kuharakisha ulipaji wa kodi serikalini. Pia kuwapa nafasi wenye makampuni kufanya shughuli zao nyengine.

Mhe. Spika, kamati yangu imeridhia kuongezwa kwa kifungu chengine kinachompa mlipa kodi, kuwa na mshauri wa kodi au kuanzishwa mshauri wa kodi. Kifungu hiki kinavyoelezwa kuwa bado dhima inabaki kwa mlipa kodi kwa jambo au tendo lolote litakalofanywa na mshauri huyu, isipokuwa kamati yangu inamsisitiza Mhe. Waziri kuwa ili aweze kufanikisha hili ni lazima haraka iwezekanavyo aweze kutunga kanuni ambayo ndio itakayotoa muongozo kwa utekelezwaji wa sheria hii kama ilivyotajwa kwenye kifungu hiki. Kwani tumekuwa na utamaduni mawaziri wetu huwa wazito sana katika kutunga kanuni zinazowaongoza hawa mawakala wa kodi. Jambo ambalo kama halikutendeka kwa wakati muafaka basi linaweza kuja kuweka ugumu kwa Kamishna kuweza kutekeleza kazi yake hii ambayo tuliyompa.

Mhe. Spika, sehemu ya tatu ya mswada huu ambao unapendekeza marekebisho ya kifungu kimoja tu, Sheria ya Kodi ya Mafuta Nam. 7 ya 2001. Marekebisho ya kifungu kidogo cha (7) ya kifungu cha 13 cha sheria hiyo, kinachopendekezwa kuingizwa maneno, "vifaa, kontena, zana au chombo cha usafiri, mali yoyote, mnyama au vitu vyengine baina ya maneno chombo na kitakachopatikana".

Kamati yangu imeridhia marekebisho hayo ambayo pia yatampa nguvu Kamishna kuweza kudhibiti wizi wa mafuta unaofanyika. Kwani kwa hivi sasa ukiacha ile bidhaa ya magendo ya mafuta basi Kamishna hana tena mamlaka ya kukikamata kile chombo kilichokuwa kimebeba magendo yale. Jambo ambalo humfanya muhusika asione uchungu wowote lakini baada ya marekebisho ya sheria hii kupita, basi hata wenye vyombo vinavyotumika kusafirisha magendo hayo, hawatokubali kubeba bidhaa hizo, kwani wakijua kuwa wakikamatwa vyombo vyao vitaingia kwenye hatia. Hii itasaidia sana kupunguza sana wizi wa magendo ya mafuta hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, kamati yangu pia imeridhia marekebisho yaliyoletwa na Mhe. Waziri wa Fedha kuliomba Baraza lako tukufu kufanya marekebisho ambayo Kamishna hatoweza kushughulikia madai ya mlipa kodi yatakayozidi milioni moja hadi apitie kwa mshauri wa kodi, na hiyo itasaidia kumpunguzia Kamishna madai ambayo yanaweza

kushughulikiwa na msaidizi wake. Kwa hivyo kamati yangu hapa haikuwa na pingamizi yoyote, kwani inalenga kuongeza ufanisi wa kazi kwa Bodi ya Mapato.

Mhe. Spika, sehemu ya tano ya mswada ambao unaosema sehemu hii itasomwa pamoja na kodi ya Sheria ya Bodi ya Mapato Nam. 7 ya 1996 ambayo katika sheria hii itajulikana kama ni sheria mama. Marekebisho ya kifungu cha 5 kimerekebishwa kwa kuweka namba za vifungu tu. Kamati yangu pia imeridhia.

Mhe. Spika, kamati yangu pia imeridhia marekebisho ya kifungu cha 15(1) cha sheria mama kwa kuongeza maneno kama yalivyoletwa na Mhe. Waziri bila ya pingamizi yoyote. Mhe. Spika, marekebisho ya kifungu cha 15 (a) kwa kuongeza maneno, "na". Pia kifungu kidogo cha (3) (a) kinachompa majukumu yake Naibu Kamishna kama atakavyopangiwa na Kamishna. Kifungu (b) kitakachompa mamlaka kufanya kazi za Kamishna pale Kamishna anapokuwa hayupo. Kamati yangu haikuwa na pingamizi na hilo.

Pia kamati imeridhia marekebisho ya kifungu kidogo cha (4) na cha (6) cha kifungu cha 29 cha sheria mama, kwa kufutwa kifungu kidogo cha (2) na badala yake neno, kifungu kidogo cha (30) kamati yangu imeridhia.

Mhe. Spika, sehemu ya sita ya mswada ambayo inapendekezwa marekebisho ya Sheria ya Rufaa ya Kodi Nam. 1 ya 2006 kuingizwa kifungu kidogo cha (2) (a) na kuingiza aya mpya (b), "Makamu Mwenyekiti atakayeteuliwa na Mhe. Waziri" ambaye hapo mwanzo hakuwepo. Jambo ambalo hapo mwanzo lilikuwa likileta usumbufu mkubwa wakati mwenyekiti anapokuwa hayupo.Hili pia kamati yangu imeliridhia lakini pia katika kifungu kidogo cha (4) kinachoongeza kifungu kidogo cha (b), kinachoelezea sifa za mtu ambaye anaweza kuchukua majukumu kwa niaba yake. Na vifungu vilivyobaki ni marekebisho ya vifungu tu ambapo pia ni kuweka utaratibu wa kisheria ambapo kamati yangu haikuwa na pingamizi iliweza kuridhia.

Mhe. Spika, sehemu ya saba ya mswada, marekebisho ya Sheria ya Bandari ambayo itasomwa kwa pamoja na Sheria Nam. 7 ya 2003 ambacho kifungu cha 86 kinapendekezwa kufutwa na kuingizwa kifungu kidogo cha (1) kinachokusudia kumuongozea muda Msimamizi wa Leseni, Dereva na malipo ya mkupuo kwa zaidi ya mwaka mmoja ambapo kamati yangu iliridhia, hasa kwa kuangalia kuwapunguzia usumbufu madereva na kuongeza mapato ya serikali kwa wakati na pia kuwapa muda mzuri zaidi maafisa wetu wa kodi kuweza kushughulikia mambo mengine na kushughulikia ukusanyaji wa kodi ya serikali.

Mhe. Spika, sehemu ya nane ya mswada kama alivyoeleza Mhe. Waziri imekusudia kufanya marekebisho ya sheria ya kazi Namba 11 ya mwaka 2005, ambayo itajulikana kama sheria mama, ambapo katika kifungu cha 40(1) kwa kuongeza kifungu kidogo (f) kinachomlazimisha mgeni yeyote kabla ya kuomba kuongezewa muda wa kibali cha kazi, basi kwanza hulazimika kuonesha vielelezo vya kulipa kodi ambazo alistahiki kulipa kabla muda wake wa kazi kumalizika hapo kabla.

Jambo hili kamati yangu iliiliridhia hasa kwa kuzingatia hivi sasa hapa Zanzibar, kuna wageni wengi wanafanyakazi sehemu mbali mbali, lakini wengine kwa ujanja au kwa kutokujua kukwepa kulipa kodi mbali mbali za serikali ambazo alipaswa kuzilipa na kuikosesha serikali yetu mapato, ambayo ndio yanayotumika kutoa huduma mbali mbali kwa wananchi wetu hapa Zanzibari.

Isitoshe, hii itasaidia kuweza kuwahakiki wale wageni wote wanaoishi na kufanya kazi nchini kisheria, lakini pia itaweza kusaidia kuweza kuwatambua wale wageni wote ambao wako nchini na wanafanya kazi kinyume cha sheria, kwa zile kazi ambazo hawakutakiwa kuzifanya wao, ambazo wananchi wetu wanaziweza.

Mhe. Spika, mwisho kabisa kwa mara nyengine tena napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa kuendelea kunivumilia kunipa nafasi ya mwanzo kuweza kutoa maoni kwa niaba ya Wenyeviti wako wa Baraza la Wawakilishi hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa kuwa utaratibu wetu unamruhusu Mwenyekiti vile vile, kwa kuwa na yeye ni mwakilishi halali wa jimbo, basi anayo nafasi yake angalau ya kuchangia japo dakika 20. Lakini kwa kuwa mimi nimesoma ripoti ya kamati, Mhe. Spika, nitaomba unipe japo dakika 10, ili na mimi niweze kutoa maoni yangu.

Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Waziri pamoja na kuwa kamati yangu imeweza kuridhia mswada huu, lakini kwanza tunaishukuru serikali kwamba haya yote ni mambo ambayo tulikuwa tukiyashauri. Tulikuwa tunaelezea namna gani serikali kuna baadhi ya maeneo ilikuwa haikusanyi kodi. Tunashukuru sasa hivi yameongezwa.

Kama alivyosema Mhe. Waziri kwamba kwa mwaka huu na sio kwa mwaka huu tu, tokea alipokabidhiwa majukumu haya, kila siku kodi inaongezeka. Lakini ukiangalia vianzio vyenyewe ni vianzio sio kama ni vipya moja kwa moja, vilikuwepo, lakini tulikuwa hatuvikusanyi. Kwa hivyo, kwa kweli Mhe. Spika, tunampongeza sana Mhe. Waziri. Lakini pamoja na pongezi hizo, kwamba amejaribu kuelezea hapa na hata katika ile bajeti kuu ya serikali kwamba serikali inapokopa fedha zile bado inakuwa sio msaada. Ule unakuwa ni mkopo na kwa kuwa ni mkopo bado inakuwa ni fedha za serikali. Kwa hivyo zile fedha serikali baadae inatakiwa kuja kulipwa.

Mhe. Spika, sasa hoja yangu iko hapa, bado serikali yetu na katika ripoti nilieleza kwamba kuna miradi mingi ambayo tunakopa fedha kwa wahisani lakini miradi hii inachukuwa muda mrefu sana kuwa haimaliziki. Kwa kweli inatuongezea mzigo, lakini hata yale madhumuni ya kukopa zile pesa, kwa kweli Mhe. Spika, inakuwa haipatikani. Kwa sababu fedha zile tunategemea serikali ingeweza kuwekeza, ili zikaanza kurudisha *return* kwa haraka na wananchi waweze kutumia huduma hiyo.

Kwa hivyo, kama tulivyoeleza mradi wa *ZUSP* Mhe. Waziri Ofisi ya Rais Ikulu kaueleza vizuri. Lakini nitamuomba zaidi Mhe. Waziri anayeshughulikia Tawala za Mikoa akija atueleze vizuri zaidi. Huu mradi wa *ZUSP* hasa kwa mwaka huu tunategemea hatua gani zitaweza kuchukuliwa.

Vile vile Mhe. Spika, bado Mhe. Waziri kuna wawekezaji ambao hivi sasa wamezuwia maeneo katika ardhi, lakini bado hawayalipii kodi Mhe. Spika, bado kuna fedha za serikali haziendelei kukusanywa. Nakuomba sana kwa kushirikiana na Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, lakini wewe ndio wakala wake kupitia *ZRB* wa kukusanya kodi ya ardhi. Bado tunahisi kuna kodi, sio tunahisi tunajua kuna maeneo ambayo wawekezaji wameyakalia, maeneo hayo bila ya kulipia kodi.

Mfano, kama nilioutoa ambao haukuweza kunitolea ufafanuzi. Mfano kama pale Chumbuni, maeneo yale kwa kweli ni makubwa, kama tunampata mwekezaji aliyekuwa makini kwa kweli ajira nyingi pale zingeweza kupatikana, eneo kwa kweli limekaa kama *white elephant*.

Mhe. Spika, miradi kuchukua muda mrefu, kwa kweli inasikitisha sana. Ninasikitika zaidi kwamba mpaka leo bajeti ya mwaka uliopita barabara ya Amani Mtoni mpaka leo haijamalizika. Mhe. Spika, kwa kweli mnatubebesha mzigo, wananchi wetu wanaendelea kupata tabu. Basi hata hii miradi ya kwetu wenyewe? Hiyo iliyoletwa na wafadhili ambayo hatuna uwezo nayo, basi hata hii midogo midogo Mhe. Spika! Kwa kweli tunaomba kwamba kila siku tusiwe tunazungumza hayo kwa hayo, lakini tunataka hatua nyengine ziende mbele.

Jengine Mhe. Spika, ni kuhusu suala la mradi wa Chelezo. Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Ikulu alipokuwa akitoa ufafanuzi katika mipango ya maendeleo, katika maeneo niliyoyagusa katika miradi ambayo wazalendo wamewekeza ni huu mradi wa Chelezo Mwangapwani. Nadhani Mhe. Waziri alipitikiwa tu, lakini naamini akija kutoa ufafanuzi, kwa sababu pale tunategemea kutakuwa kuna kodi ya serikali itapatikana. Lakini pia kuna ajira kama nilivyoeleza zaidi ya 200 zinategemewa zitapatikana pale.

Mhe. Spika, kwa kweli mimi ninasikitika sana, hapa Mhe. Waziri alipotoa ufafanuzi alipokuwa akijibu hoja za wajumbe katika uwekezaji kulinganishwa Zanzibar na Mauritius. Mhe. Spika, kuna mambo mengine alieleza Mhe. Waziri Wazanzibari kama ile mitaji yao wangekuwa wanawekeza Zanzibar, kama nilivyoeleza karafuu mwaka huu Pemba peke yake ni bilioni 63 zimeweza kukusanywa. Lakini watu wamekwenda kuekeza Tanzania Bara na hii Mhe. Spika, ziko sababu.

Mimi nataka nizungumze, kama huu mradi wa Chelezo, leo Mzanzibari huyu kaamua kuwekeza fedha zake hapa Zanzibar, tunaendelea kumnyanyasa, tunaendelea kumsumbua, hatumpi nafasi ya kuwekeza, watu wasiende kuwekeza Bara! Tanzania Bara leo ukienda tu una mradi wako unakubaliwa.

Mfano mdogo, Turky yule pale alitaka kuweka Kiwanda cha Saruji Zanzibar. Tukampiga huku na huku, tukampiga vikuta akaamuwa kwenda kuwekeza Bara, baada ya kufika kapewa ardhi keshawekeza Kiwanda cha Saruji. Mhe. Spika, hawa watakimbia. Hebu tuigeni kama tunataka tuwe kama Mauritius bado bila ya kuangalia mambo mengine,

hebu tujaribu kuwapa nafasi, tuwape *green pasture* hawa wawekezaji wetu wazalendo waweze kuwekeza tusiwasumbuwe.

Mhe. Spika, kwa kweli mradi ule ungweza kuleta ajira, kodi ya serikali, kuna meli nyingi zingekuja. Mhe. Spika, vijana wetu zamani walikuwa wanakwenda Ugiriki kwenda kupanda meli. Kule wanakwenda kugonga na kutengeneza mameli. Leo Chelezo kinakuja hapa hapa tunakizuwia mpaka leo, taratibu zote wamefuata leo tunamzuwia. Tunaambiwa kuna sababu, hebu tuambiwe basi hizo sababu.

Mhe. Spika, kwa kweli mambo mengine haya yanarejesha nyuma wawekezaji wetu na kweli kwa usumbufu kama huu wawekezaji, wananchi wetu wa Zanzibar wataendelea kwenda kuwekeza upande wa pili wa Muungano, halafu tuseme kwamba hawataki kuwekeza hapa na kumbe tunawafukuza sisi wenyewe.

Mhe. Spika, mradi sio huu tu, kama nilivyosema na nitakuja kuzungumza kwenye Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano. Kuna mradi huu wa *Air Strip* ambapo kuna mwekezaji kama nilivyoeleza katika bajeti iliyopita, ingawa mawaziri wanatupiga maneno ambayo hayana uhakika. Wengine wanasema kwamba mpaka kipatikane kibali cha *TCIA*. Tuliulizia kule Bara, wakasema matatizo mnayo nyinyi Zanzibar. Sisi hapa tumo mawaziri tunasingizia Muungano, kumbe matatizo tunayo wenyewe.

Mwekezaji yule anataka kuwekeza Mradi wa *Air Strip*. Nimejaribu kuangalia Bara. Bara kuna *Air Strips* nyingi. Mimi mwenyewe nimeshatua katika *Air Strip* ya hapa Tanga, lile jina kidogo limenitoka. Ipo *Air Strip* moja pale, yaani ni *very simple* na mheshimiwa kutokana na mazingira ya nchi yetu mwekezaji yule, yeye alitaka kuwekeza Nungwi. Eneo tayari ameshanunua, ameshalipa *compensation* zote, tunampiga chenga huku na huku na kwa sababu Mhe. Spika, miradi ile tunataka kuwekeza sisi wenyewe wakubwa, hiyo ndio sababu. Tumeshafanya utafiti tunataka kuwekeza sisi tunawazuwia wawekezaji.

Mhe. Spika, kama kweli tunataka nchi yetu iwe kama Mauritius hebu tuondowe huu urasimu. Mhe. Spika, Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano nafikiri hii *message* naileta itakapofika bajeti yako pamoja na Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa kweli mambo kama haya tunataka yamalizike.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache niliyoyaeleza nakushukuru tena kwa kunipa nafasi hii na kuweza kuwasemea wananchi. Lakini vile vile kwa kuweza kuionesha serikali ni maeneo gani ambayo tutakapoweza kujitahidi basi tunaweza kuongeza mapato na tukafungua ajira kubwa kwa uapande wa Zanzibar. Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, ahsante sana. *(Makofi).*

Mhe. Spika: Ahsante sana. Naomba nimkaribishe Mhe. Hija Hassan Hija.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, naomba nikushukuru sana na naomba nichangie mswada huu wa Mhe. Waziri kwa ufupi, na kwa lengo la kumsaidia jinsi ya kupata nyenzo ya ukusanyaji wa mapato kama ambavyo yeye mwenyewe ameomba kwa kupitia mswada huu.

Mhe. Spika, ni jambo la wazi kwamba duniani kote serikali mbali mbali hutegemea kodi. Kodi ndizo ambazo husababisha mapato ya nchi na mapato hayo ndio ambayo huendesha nchi kwa kazi za ndani na kazi za maendeleo.

Mhe. Spika, tumekuwa tukiwashauri sana serikali mara nyingi kwamba kuna haja ya kukaa na kuangalia uwezekano wa wigo wa kodi kwa maana vyanzo vya mapato na sisi kama ambavyo kaka yangu Mhe. Hamza Hassan amesema, yako maeneo ambayo tumekuwa tukiona kwamba yanaweza kuchangia mapato ya nchi. Jambo ambalo hawatuelezi serikali huwa wanakwama wapi maeneo hayo kuyasimamia na kuongeza huo wigo wa kodi.

Mhe. Spika, kodi hizi kwa kiasi kikubwa zingechangiwa na kasi ya uwekezaji. Zanzibar ina upungufu wa kasi ya uwekezaji hasa sekta ya viwanda, jambo ambalo serikali haijaona umuhimu wa kusimamia sekta hii kwa kisingizio kwamba Zanzibar ni kisiwa, hatuna eneo, hali ya mazingira kama Mhe. Hamza Hassan alitoa mfano wa Mhe. Turky pale alipokuwa akitaka kuwekeza Kiwanda cha Saruji.

Mhe. Spika, tumuangalie mwekezaji Bakharesa kwenye sekta hii ya usafiri wa bahari jinsi gani anatengeneza ajira na kuongeza mapato katika nchi yetu na hivi sasa amewekeza Kiwanda cha Maziwa kule Fumba, ni jinsi gani ambavyo ataongeza ajira na kuongeza mapato ya nchi. Kwa hivyo, ni kusema kwamba uwekezaji wa viwanda hasa

wawekezaji wa ndani ndio watu pekee ambao wangepaswa kupewa kipaumbele kwa ajili ya kuongeza ajira na mapato ya nchi.

Naungana kabisa na Mhe. Hamza Hassan kwamba hatuoni sababu ya msingi Mwekezaji wa Chelezo Mangapwani, kwa nini sasa ni mwaka wa saba hajapewa kibali kama ambavyo aliomba. Visingizio ambavyo vilimkimbiza ndugu yetu Turky, nadhani ni vile vile ambavyo vitamkimbiza huyu mwekezaji wa Chelezo. Hii athari yake ni kupunguza mapato ya nchi na kuwanyima Wazanzibari ajira.

Mhe. Spika, nimuombe sana Mhe. Waziri wa Fedha waliombe Baraza la Mapinduzi kuzingatia umuhimu wa kuwalinda wawekezaji wa ndani ili mitaji yao isipotee na kuimarika nje ya Zanzibar, ili iongeze kasi ya ajira na mapato ya nchi.

Mhe. Spika, sasa niseme kwamba mswada huu una malengo mazuri, lakini wakati mswada huu tunataka kuupitisha kwa kuidhinisha serikali kutumia, Mhe. Waziri naomba unijibu swali moja kwanza. Bajeti ambayo tumeipitisha ni bajeti ya mwaka 2014/15, ikiashiria kumalizika kwa bajeti ya mwaka 2013/14 ambapo serikali kwanza ilitenga fedha za Mfuko wa Jimbo, kwa maana ya milioni 15 kila jimbo.

Je, serikali wakati inaingia kwenye bajeti mpya, wakati serikali haijatoa hata shilingi moja kwenye mfuko wa jimbo, majimbo yote 50 ya Zanzibar. Vipi Wazanzibari wa majimbo yote 50 pesa ile itatolewa. Wasi wasi wangu Mhe. Spika, wakati kodi hii mpya imeidhinishwa, fedha ile itakuwa imefifia na itatoka mwaka 2014/15 na wakati ni haki ya mwaka 2013/14.

Mhe. Waziri wa Fedha nakuomba sana kabla hatujapitisha bajeti ya Wizara ya Makamu wa Pili wa Rais, tupate matumizi ya fedha yetu ya jimbo ili isije ikaingia mwaka wa usoni na hatimae kufifia. Mhe. Spika, wenzetu Wabunge wakati bajeti iko juu ya meza fedha zao tayari zimeingizwa juzi na wameanza kutumia. Mhe. Waziri wa Fedha naomba utuahidi basi, pengine kesho au Ijumaa fedha zetu zitaingia ili tuidhinishe hizi fedha mpya kwa ajili ya maendeleo ya majimbo yetu.

Mhe. Spika, nimpongeze Mhe. Waziri wa Fedha kwa kuamua kuweka kodi ya wafanyakazi wa kigeni. Kwa kweli ni hatua nzuri. Tuseme ukweli kwamba mahoteli mengi ya Zanzibar yameajiri wafanyakazi wa kigeni ambao ni wataalamu na kwa sababu ni wataalamu maana yake watakwenda na mishahara mikubwa. Mishahara ambayo itaongeza kodi ya ndani na mishahara ambayo kwa kweli itaongeza mapato ya nchi yetu. Sasa hatua hii ya kulinda kodi ya wafanyakazi wa kigeni ni hatua moja muhimu sana.

Naomba pia nimuambie Mhe. Waziri kwamba afanye utafiti kujuwa ni wafanyakazi wangapi wa kigeni wanatumia mishahara yao kwa kupitia *PBZ* Zanzibar.

Mhe. Spika, wafanyakazi wengi wa kigeni hawatumii benki yetu kama ni rasilimali Zanzibar. Wafanyakazi wengi wanatumia benki za kigeni ingawa zina matawi hapa Zanzibar. Sasa hii kimapato, kiuchumi ina athari kubwa. Nimuombe Mhe. Waziri pamoja na kuwatoza kodi wafanyakazi wa kigeni, lakini washajihishwe wafanyakazi hawa kutumia benki yetu ya ndani, ili kwa faida ya kuongeza mapato ya benki yetu na mapato ya nchi yetu. Sio busara kabisa kwamba Benki ya Zanzibar inatumiwa na Wazanzibari wenyewe tu, bila ya kutumia wafanyakazi wengine wa nje ya Zanzibar.

Mhe. Spika, niombe kumwambia Mhe. Waziri suala zima la marejesho. Sheria hii tayari imeweka uwezo wa kupeleka marejesho kwa wakati. Mimi ningeomba na majeshi haya yangepangiwa muda maalum. Marejesho ndio yanaweka usahihi wa mapato na matumizi ya taasisi. Kwa hivyo, mbali ya kusema marejesho yarejeshwe kwa wakati, lakini ningeomba ule wakati wenyewe ukatajwa hasa, ikiwa ni wiki moja au wiki mbili baada ya mahesabu kukamilika, vyenginevyo bado mwanya upo wa kuwakilisha mahesabu haya na hatimae yataathiri mapato ya taasisi za ukusanyaji wa kodi.

Jengine Mhe. Spika, ni suala zima la kuzuwia chombo, pia nilishauri kwamba Kamishna pale atakapoamua kuzuwia chombo, ningeomba kuwe na muda maalum wa kuzuwia chombo, kwa sababu Kamishna anaweza kuzuwia chombo, pengine ikafika miezi mitatu.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, hebu turekebishe hii simu inayotuletea tatizo. Au sijui ni mitambo yetu. Haya endelea.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nadhani ni mitambo, kwa sababu *bench* yangu haina simu iliyowazi.

Mhe. Spika, namshauri Mhe. Waziri kwamba uzuwiaji wa chombo ni jambo zuri sana, lakini nadhani ungewekwa muda ni muda gani Kamishna anaweza akazuwia chombo ambacho amegundua kina matatizo ya ulipaji kodi. Hii faida yake ni nini, faida yake ni kwamba fursa ya mwenye chombo kufanya haraka ya malipo na vile vile kuingiza mapato serikalini. Sio vyema kwamba chombo hiki pengine wakizuwie miezi mitatu, miezi mitano au mwaka mmoja. Hatua hii Mhe. Spika, ni dhahiri mapato ya nchi yanapotea na lazima sheria hii basi Mhe. Waziri atuwekee muda wa kuzuwia chombo hicho.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo nataka Mhe. Waziri atuambie, kuna suala la afisa wa kuzuwia kodi, mimi sijafahamu kwamba yule afisa ndio kazi yake kuzuwia kodi au kazi yake ni kuzitafuta kodi na kuzidhibiti kodi, kwa sababu hii lugha iliyozungumzwa hapa sijaifahamu. Kama kuzuwia kodi, unaweza pia kumwambia kodi zisiingie. Nadhani imekusudiwa kwamba kodi zipatikane kwa ajili ya kudhibiti maslahi ya serikali.

Mhe. Spika, jengine ambalo nataka Mhe. Waziri aniambie ni kwamba jana nilitoa mchango hapa kuwa yako makontena ya wafanyabiashara wa Zanzibar, walidhamiria yashuke Zanzibar kwa ajili ya kuchangia kodi ya Zanzibar na bahati mbaya yakashushwa pale Dar es Salaam. Makontena yale yangeshushwa hapa Zanzibar maana yake fedha zingeingia katika *account* ya Zanzibar.

Je, hii si hatua ya kuzuwia kodi, kama ni hatua ya kuzuwia kodi, vipi serikali imeweka sheria hii kudhibiti watu kama wale wasizuwie kodi ambayo ingeingia hapa Zanzibar kwa wakati na kodi Mhe. Spika, sio kuingia tu, lakini pia kuingia kwa wakati. Kodi ambayo ilitegemewa iingie Jumatatu, ikiingia Ijumaa kimahesabu kuna athari kubwa ya mapato. Kwa hivyo, Mhe. Spika, Mhe. Waziri naomba pia atuwekee sawa kwenye eneo hili la uzuwiaji wa kodi ambao kwa kweli unafanywa na wenzetu wa *TRA* Bara, kwa ajili ya kudumaza mapato na uchumi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, baada ya hayo naomba Mhe. Waziri azingatie sana umuhimu wa wawekezaji wa ndani, hawa ndio pekee ambao wataongeza mapato na ajira ya Wazanzibari wetu na taifa letu Mhe. Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Mahomoud Mohammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipatia nafasi ya kuweza kuchangia mawili matatu juu ya mswada wetu ambao upo mbele yetu. Mimi ni mmoja kati ya wajumbe wa kamati ya uongozi na maoni yetu na michango yetu tulikwisha kutoa katika kamati ya uongozi kule juu, na ni yale ambayo Mheshimiwa Mwenyekiti amewasilisha hapa. Lakini zaidi nilikuwa naomba kuweka *hansard* sawa tu katika marekebisho ya kumi katika kifungu cha 27 pale ambapo kulikuwa na aya kutoka namba mbili ya kirumi mpaka namba tano na huku mbele vile vile isomeke (a) moja ya kirumi (b) mbili ya kirumi pamoja na chini (c) moja ya kirumi na (d) mbili ya kirumi.

Baada ya marekebisho hayo sasa Mhe. Spika, nakubaliana na naunga mkono vile vile ripoti iliyosomwa na mwenyekiti wetu hapa juu ya maoni ya wenyeviti wa kamati, kwa hotuba ambayo Mwenyekiti wetu alikuwa ameisoma.

Jengine ambalo nilikuwa naomba kuchangia pia Mhe. Spika, ni katika sehemu ya saba katika marekebisho ya sheria, kifungu cha 31 Mhe. Spika, nilikuwa vile vile naiomba Serikali kwamba sina tatizo na suala la ulipaji wa hizi leseni ikiwa kwa muda wa miaka miwili mitatu mpaka mitano ambayo ilikuwa imependekezwa, isipokuwa tatizo langu sasa nahisi kwamba wakati umefika kuangalia afya za wale watu ambao watakuwa wanapewa leseni, kwa ajili ya kuendesha magari katika barabara zetu.

Hali za binaadamu wetu na hali halisi ya uendeshaji wa magari katika barabara zetu, iko haja sasa mbali ya kuangalia uwezekano wa kuzidisha muda wa leseni, lakini vile vile kuangalia hali za afya za wale watu ambao wanamiliki vyombo hivi na kuviendesha katika barabara zetu.

Jengine ambalo nilikuwa nataka kuchangia, tulipopata tafsiri au tuliopopata hii miswada ya Kiswahili na Kiingereza yale matatizo ya tafsiri mswada wa kiingereza kwenda kwenywe kiswahili, yale matatizo bado yanaendelea. Naomba kuchukua fursa hii kusisitiza tena na kuwaomba wenzetu ambao wanafanya tafsiri ya hii miswada

waendelee kuwa makini zaidi na wajitahidi wanapotafsiri. Tafsiri zao ziwe zinaendana baina ya maelezo ya Kiingereza na maelezo yanayotolewa tafsiri katika lugha ya Kiswahili.

Baada ya hapo Mhe. Spika, mimi kwa heshima na taadhima naunga mkono mswada huu pamoja na marekebisho yake ambayo yalikuwa yemeletwa kwetu na kwa niaba yangu binafsi na kwa niaba ya wananchi wa jimbo la Kikwajuni, nakubaliana na mswada huu. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika, nakusudia nimkaribishe Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa angalau nikachangia machache kwenye mswada huu ambao ni mswada muhimu sana kwetu. Kwanza nikubaliane na Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti naungana nae mkono kwa marekebisho ambayo ameyaleta.

Mhe. Spika, mswada huu ni muhimu na ni mswada wa kurekebisha sheria ya kutoza kodi na kubadilisha baadhi ya sheria za fedha na kodi na kuhusiana na ukusanyaji na udhibiti wa mapato ya Serikali na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Sheria hii ni muhimu na tukirekebisha sheria mbali mbali ambazo zimo katika sheria hii ya fedha na kudhibiti mapato ya Serikali, sheria za kutoza kodi na kubadilisha baadhi ya sheria za fedha zinazohusiana na ukusanyaji wa mapato, ni muhimu sana na hata tuseme kwamba umekuja kwa wakati muafaka.

Mhe. Spika, mapato ni muhimu katika nchi kwani ndio yanayosababisha utekelezaji wa Serikali kwa mambo yake mbali mbali. Kuna vianzio vya mapato kupitia taasisi mbali mbali ambazo taasisi hizi zina majukumu na uendelezaji wa taasisi hizo.

Mhe. Spika, ningeomba mapato hayo yaachiwe taasisi zenyewe ili taasisi hizi ziweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, nitoe mfano wa taasisi iliyokuwa muhimu ni kama vile mamlaka ya uwanja wa ndege ambao una vianzio vyake vingi vya mapato, moja ya vianzio hivyo ni *Airport service charge*. Lakini fedha hizi zinakwenda kwenye mfuko mkuu wa serikali na kuiachia mamlaka kuwa na ukosefu wa kupata fedha za kuboresha viwanja hivyo.

Mhe. Spika, mamlaka ina jukumu la kuboresha viwanja vyake ili kufanya uwanja kuwa wa kimataifa. Ukitizama pale kwenye ule uwanja wa ndege kuna mambo mengi; kwanza kuna magari ya kuzimia moto, *Extra machine* nazo ni mbovu kwa kipindi kirefu, ili kufanikisha basi inabidi fedha hizi wanazozikusanya basi ziachiwe taasisi zenyewe na wao basi kuwe na lile gawiyo baada ya kufanya vizuri. Basi kutapatikana lile gawiyo ambalo litakwenda Serikalini, lakini kuzichukua fedha hizi Serikali kwenye mfuko mkuu, kwa kweli ni changamoto na niseme kwamba taasisi hizi zitakuwa sio endelevu.

Mhe. Spika, kwa kuwa kama nilivyosema kwamba sheria hii imekuja wakati muafaka na ni juu yetu waheshimiwa wawakilishi humu ndani kuweza kusoma vizuri na kuzipitisha, kwa sababu sheria ni muhimu kuwa nazo na zile sheria ambazo kila siku zimekuwa zimepitwa na wakati basi ni wajibu wetu kuzifuta na kupitisha sheria nyengine, ili ziweze kufanya kazi vizuri zaidi.

Kama nilivyosema mapato kwa Serikali ni muhimu sana kwa sababu ina majukumu mengi na ni lazima majukumu hayo kama ni serikali ni lazima iyatekeleze bila ya mapato, serikali haiwezi kujiendesha. Kwa hivyo ni lazima kuzisimamia na kuzitekeleza kwa uwazi na uwajibikaji ipasavyo ili haki itendeke. Hapa kama sheria hizo zitasimamiwa kwa uwazi basi naamini kwamba hapo sheria itakuwa imesimamiwa na haki itakuwa imetendeka.

Mhe. Spika, Sheria ya kutoza kodi na kubadilisha baadhi ya sheria za fedha na kodi kuhusiana na ukusanyaji na udhibiti wa mapato ya Serikali na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Niseme tena kwamba imekuja wakati muafaka wakati huu wa kupitisha bajeti ya Serikali. Kwa hivyo ni lazima ili sheria hizi zifanye kazi basi ni lazima kuwe na sheria ambazo tutazitumia kodi hizi pamoja na mapato haya, ili sasa tuweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

Baada ya hayo machache Mhe. Spika, naomba kuunga mkono mswada huu kwa niaba ya wananchi wangu wa Amani, niseme ahsante sana kwa kunipa fursa hii. (*Makofi*)

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Spika, kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambae ametuwezesha siku hii ya leo kufika tena hapa katika mjadala kwa mintarafu ya kutengeneza mambo yetu ya taifa

letu. Lakini pia nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa tena fursa hii, mimi sitokuwa na mengi isipokuwa nataka nifahamishwe vizuri na Mheshimiwa Waziri. Maana siku zimepita kuna ile sheria mama sijui inasemaje ule mswada wa sheria mama, ule sijui sheria inasemaje maana siku tena zimekuwa nyingi. Lakini nitaomba tu anifafanulie je, huyu kamishna atakuwa hashitakiwi akifanya makosa?

Maana mtu kumuachia madaraka makubwa kama haya halafu kukawa hakuna lolote, kwa kweli ningemuomba Mhe. Waziri hili aje hapa atufahamishe Baraza lako hili tukufu ili tuelewe zaidi. Maana kuelewa zaidi ni vizuri kuliko kupitisha jambo ambalo ikawa hulielewi, hilo moja.

La pili niseme naunga mkono hoja mia chini ya mia, ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Spika, na mimi nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuweza kutoa mchango wangu katika masuala mazima ya kodi au udhibiti wa kodi. Mimi nina moja tu, nilitaka ufafanuzi kwa Mheshimiwa Waziri jambo ambalo kidogo linanipa wasi wasi katika uandishi wake na sheria zake, zimekuwa kidogo zina mashaka.

Nataka waziri aangalie kifungu cha tisa ukurasa wa 19 ambao unazumgumzia ikiwa kwa maoni yake kufunga biashara kutaharakisha malipo ya kodi hapa ni kama maoni tu, au anafikiria kwamba kufunga biashara kutaharakisha malipo ya kodi. Chini kifungu cha pili kinasema kwa kuingiza maelezo yanayofuata au yafuatayo, atafunga au kuweka lakiri katika jengo la mlipa kodi na baadae bidhaa zilizomo ndani zitachukuliwa kuwa zimekamatwa na kukabidhiwa kwa kamishna.

Hayo maelezo yanahitaji tafsiri na ufafanuzi. Kwa sababu ninachokiona mimi hatua za adhabu katika eneo hili zimekuja mbili kwa mpigo; adhabu ya kwanza ni ya kuweka lakiri kwenye mlango wake na adhabu ya pili ni ya kuchukuliwa mali yake. Sasa naona kwamba katika eneo hili kuna adhabu mbili kwa mpigo, kwa nini haioneshi kwamba ichukuliwe ile kufunga mlango ni adhabu peke yake. Sasa haya malipo utayapata vipi wakati mlango wake umeshaufunga? Sasa kwa hivyo ningeomba kidogo Mhe. Waziri atusaidie ufafanuzi katika hili.

Jengine ambalo naliona kwamba zitakuwa zimekamatwa bidhaa hapa, hazijakamatwa hizi kukamata mnakamata huko mbugani ndio mnakokamatana, lakini mali ipo katika eneo ndani ya *store* sio ya kukamata ile, labda tuseme hapa kwamba zitachukuliwa na kukabidhwa ingekuwa afadhali zaidi, kwa sababu pale hapana kukamata. Iko tayari mali inajulikana isipokuwa huyu hajalipa kodi tu, kwa hivyo ningependa hapo Mhe. Waziri atusaidie ufafanuzi, ahsante Mhe. Spika. *(Makofi)*

TAARIFA

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba niweke kidogo *hansard* sawa kwa sababu nilipokuwa nikisoma ripoti yangu niligundua kwamba kwenye *item* namba 8 naomba isomeke kifungu cha 13 cha mswada na sio kifungu cha 14. Unajua kwenye kuchapa pale mkono uliteleza. Baada ya marekebisho hayo Mhe. Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Spika, kwanza nataka niwashukuru Waheshimiwa wajumbe kwa kuchangia mswada huu. Mswada wetu huu kwa sababu haukuwa mgumu sana, kila mmoja ameufahamu vizuri ndio maana kwamba waliochangia walikuwa wachache na hii inanipa faraja kwamba kila tunapokwenda mbele uelewa wetu unakuwa mkubwa zaidi, na Mwenyezi Mungu atatuongezea uelewa mkubwa zaidi.

Sasa waliochangia ni Waheshimiwa sita. Mhe. Hamza Hassan Juma Mwenyekiti wa Wenyeviti, Mhe. Hija Hassan Hijja, Mhe. Mahamoud Mohammed Mussa, Mhe. Fatma Mbarouk Said, Mhe. Asha Bakari Makame, na Mhe. Suleman Hemed Khamis.

Mhe. Spika, naomba nisaidia kwa kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya maeneo ambayo nimeulizwa. Kwanza Mheshimiwa Hamza ametaka kanuni ziharakishwe ili kusaidia utekelezaji wa zile sheria. Mimi nakubaliana naye sana na hivyo ndivyo ambavyo wenzetu hawa wa TRA na ZRB mara nyingi zikibadilika hizi sheria huwa suala la kanuni hazichelewi. Kwasababu unapochelewesha kanuni maana yake unachelewesha na kodi. Inapofika mfanya biashara anataka tafsiri haioni, sasa kodi inaanza kuchelewa kwa hivyo hili tunalichukua na kulifanyia kazi vizuri zaidi.

La pili Mheshimiwa Hamza amekuja na malalamiko kidogo kwamba miradi yetu tunayoitelekeza kupitia fedha hizi inachukua muda mrefu. Hata na mimi nakubaliana na wewe kwamba isichukue muda mrefu, kwa sababu inapochukua muda mrefu na gharama kwa Serikali nazo zinaweza kuongezeka. Mimi nitashauriana na wenzangu ndani ya Serikali, mawaziri wenzangu tumesikia. Tutashauriana na Makatibu Wakuu wenzetu na watendaji ili tuisimamie miradi hii iweze kukamilika kwa mujibu wa muda uliopangwa.

Vile vile amezungumzia kodi ya wale ambao wamechukua maeneo yetu zilipwe kama nilivyoeleza, kwamba zamani mtu alikuwa anachukua eneo halafu anakaa mpaka anapojenga mradi ndiyo anaanza kulipa kodi ya ardhi. Sasa hivi ukipewa eneo siku ile ile hatukupi muda, tunakwambia kwamba uanze kulipa kodi ya ardhi na tunawapa. Nadhani kama sio miezi kumi na mbili ni ishirini na nne, hujafanya *development* yoyote ile ardhi inafutwa inapewa wengine ambao wanataka kui-*develop.*

Umezungumzia barabara ya Amani/Mtoni; nadhani jana tu nilikuwa na watu wa miundo mbinu tumezungumza barabara ya Amani/Mtoni na nadhani itabidi tuanze kuendeleza kwa haraka zaidi.

Mradi wa Chelezo ni mmoja ambao nitaomba baadae tuje kukaa pamoja tuone hasa tatizo lake ni nini kama liende *master plain* basi tuangalie jinsi tunavyoweza kusaidiana katika huu mradi. Kwa sababu ni mradi mmoja ambao unawahusisha wazalendo na hili ambalo ndilo nilikuwa ninalizungumza sana hapa.

Mhe. Hija moja ambalo alilozungumza ni hilo la chelezo nimeshaeleza. Tuwalinde wawekezaji wa ndani, mimi ninakubaliana na wewe kabisa kwamba tutakapowalinda wawekezaji wa ndani itasidia zaidi kupata zile fedha zao badala ya kuekeza maeneo mengine wataendelea kuziwekeza ndani. Muekezaji wa ndani unapomlinda anaweka ndani kila kitu. Muekezaji wa ndani anakuwa mara nyingi hana *account* nje ya nchi, *account* za humo humo ndani. Kwa hivyo fedha yake yote inatumika humu humu ndani.

Tutajitahidi sana lakini nawaomba sana wawekezaji wa ndani wawekeze katika miradi mikubwa yenye tija. Washirikiane wawekeze katika miradi yenye tija sio miradi hii midogo midogo ambayo haina tija halafu na yeye anataka alindwe, tena kulindwa wenyewe anataka umlinde kwa mabunduki. Sasa hizo gharama za kumlinda zitakuwa ni kubwa zaidi kuliko hata gharama zake alizoekeza.

Ndugu yangu Hija usiwe na wasiwasi mfuko wa jimbo tunajiandaa, fedha hizo tutazitoa kabla ya tarehe 30 Juni, fedha itatoka. Lakini nataka niseme msije mkawalaumu watendaji wangu nimeweka *instruction*, yule ambaye amesharejesha *return* ndie tutakayempa pesa. Msiwalaumu watendaji wangu mkasema kwamba ni watendaji ndio waliokudhulumuni. Ni mimi Waziri nimeweka *instruction* hizo. Aliyerejesha *return* atapewa pesa, aliyekuwa harejeshi hatumpi. Kwa sababu lazima sisi tuwajibike, sisi viongozi kwanza halafu wawajibike watendaji wengine. Kwa hivyo hilo nataka niliweke wazi Mhe. Spika, mbele ya kikao chako waelewe kwamba na mimi nimezuia mpaka watakaporejesha *return*. *(Makofi).*

Suala la wafanyakazi wa kigeni tumesema hapa kwamba hawa wafanyakazi wa kigeni waliopo Zanzibar, sisi tunawataka mishahara yao ipitie kwenye benki yoyote iliyoko Zanzibar, kama itapitia kwenye PBZ, ipitie kwenye CRDB, ipitie kwenye Barclays, lakini ipitie hapa kwa Zanzibar ili tuweze kum-*monitor* huyu analipa kodi, halipi kodi.

Ushauri wako uliosema kwamba tufanye utafiti kwa upande wa PBZ kuelewa ni wafanyakazi gani wa kigeni wanaopeleka pesa zao PBZ, hili tutawaambia watu wetu wa PBZ watutayarishie kama wapo wanapeleka PBZ. Lakini sisi tunachokitaka waweke hapa Zanzibar, wapitishie Zanzibar. Sio ninasikia mtu analipwa benki LIoyds iko London hatutaki utaratibu huo, tunataka hapa hapa *Zanzibar.*

Mhe. Hija vile vile umetaka kwamba kuwe kuna muda wa kuzuia chombo. Kwa mujibu wa sheria ile ya usimamizi wa kodi muda Kamishna kapewa siku 5, anakizuia chombo anatakiwa awe amemuandikia mwenye chombo *within* 5 *days* kwamba chombo chako nimekikamata kwa sababu kinafanya *magendo 1, 2, 3 na nimekamata na magendo yamo ndani.* Baada ya hapo anatakiwa achukuwe zile *procedures* za kukipeleka mahkamani hicho chombo. Sasa hizo *procedures* za kisheria zitafuata baadae. Lakini *procedures* za kisheria inawezekana chombo kikawa ndio ushahidi kikakaa miaka 2 pale, lakini Kamishna ana siku 5 lazima am-*notify* mwenye chombo. Kwa hivyo hili ninafikiri Kamishna amenisikia na yeye atalisimamia, kwa hivyo ni siku 5.

Umezungumzia Afisa wa kuzuia kodi; huyu ni yule ambaye wewe mwenyewe umemtolea tafsiri sio kuzuia kwamba kodi anaizuia isiingie aa, anaizuia kwamba huyu lazima tupate kodi yetu ili iende serikalini hiyo kodi.

Umezungumzia makontena yaliyozuiliwa Dar es Salaam, nimewaagiza wenzangu wa TRA wanitafutie maelezo ya kina juu ya haya makontena nitakapopata taarifa hii tutaweza ku-*share* mimi na wewe. Lakini kimsingi ni kwamba kuzuiwa makontena Dar es Salaam inawezekana ni mambo 2.

Inawezekana kwamba lile kontena lenyewe mfanyabiashara wa Zanzibar lakini ameliandika lishuke Dar es Salaam, ili aweze kuli-*transfer* baadae kulipeleka Zanzibar likishuka Dar es Salaam. Ukiliandikia lishuke Dar es Salaam utalipa kodi pale, lile sio *transit* kwa mujibu wa sheria ya *custom*, lile haliitwi *transit.* Kwa hivyo hili tutaliangalia lina matatizo gani tukipata taarifa tuta-*share* na wewe Mhe. Hija.

Mhe. Mahmoud ume-*raise* kitu kizuri sana Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa, tunatoa leseni sasa za muda mrefu, lakini *to what extent*? Hawa madereva tunawachunguza afya zao. Unatoa leseni ya miaka 5 huyu dereva afya yake ataendelea kuendesha kumbe haoni. Kuna kesi moja juzi Mhe. Ali Salum hayupo, kuna kesi ambayo dereva amechukua gari ameendesha amefika pahala kumbe macho yake haoni, sijui imetokea ajali, kuna kesi kama hizo.

Mimi ninadhani wenzangu tulioko ndani ya serikali, hili nadhani tuweze kulifanyia kazi. Bahati nzuri Waziri wa Afya hayupo lakini Kaimu Waziri wa Afya yupo, tuanze kulifanyia kazi. Kuwe kuna utaratibu wa hawa madereva nao ku-*check* afya zao ili kunusuru ajali.

La pili, kama dereva kwa mfano ana TB na gari anayoendesha ya abiria, hili nalo vile vile tuliangalieni, kwa hivyo wazo ulilolileta ni zuri mimi nadhani tutakaa tuone jinsi gani tutakavyoweza kulifanyia kazi. Tukishirikiana na wenzetu wa ZRB, ili tujuwe hili kwamba tunalifanyia kazi kwa kiasi gani kama mtu anapokwenda ku-*renew* leseni yake, tunataka kitu gani na kitu gani na kitu gani, angalau viweze kusaidia kutoa ithibati kwamba huyu afya yake iko *okay*, kwa kunusuru afya na maisha ya watu wetu.

Umeeleza kitu kizuri tafsiri ya Kingereza na Kiswahili lazima zioane na hilo ndio lengo. *Of course* sisi Barazani tunatumia sheria zote mbili Zanzibar ya Kiswahili na ya Kingereza. Lakini kwa wenzetu ambao hawafahamu Kiswahili watalazimika wao kuitumia tafsiri ya kingereza. Kwa hivyo ulilolieleza ni zuri na wenzangu wanasheria pale ni wazuri tu kwa lugha ya kingereza. Nadhani watakuwa wanaziangalia ili ziweze kuoana lugha ya Kingereza na lugha ya Kiswahili katika zile sheria zetu.

Mhe. Fatma Mbarouk Said umeeleza kwamba taasisi zikusanye halafu mapato yao yawe wanatumia. Mimi hili ningelilikubali kama taasisi zote zingekuwa zinakusanya, lakini nitakupa mfano taasisi kama Wizara ya Elimu; Wizara hii hawana kodi zaidi ya SDL lakini ni watumiaji wakubwa wa bajeti yetu.

Wizara ya Afya hawana kodi nyengine yoyote ile, lakini ni watumiaji wakubwa wa bajeti yetu. Sasa tutakapoliona kwamba hawa wanaokusanya watumie wenyewe hawa waliokuwa hawakusanyi watakuwa hawana la kufanya, hali ita-*deteriorate.* Lakini ukiwaambia wakusanye maana yake nini, maana yake wafanye kila kitu wao. Nitakupa mfano uwanja wa ndege wa Zanzibar. Serikali imebeba mikopo mitatu mikubwa, imebeba mkopo wa milioni 41 dola, ile *runaway* kutoka Benki ya Dunia, tumebeba mkopo serikali inalipa.

Tumebeba mkopo wa *Terminal Building*, hili ndio linaendelea kutengenezwa sasa hivi 120 milioni dola. Tumebeba mkopo wa *taxiway* na *apron* 51 milioni dola hizi zote ukiwaambia sasa nyinyi pesa hizi kwa mapato yenu mnokusanya *airport* hawataweza kulipa ng'o.

Kwa hivyo utakuta ukibeba mapato na ubebe na mikopo yako itakuwa ni ngumu sana. Lakini la msingi Mhe. Fatma ambalo mimi nataka nikubaliane na wewe ni kwamba tuangalie serikali kwa ujumla wake iangalie maeneo ambayo yana dharura, yana mahitaji haraka na ni maeneo ambayo yanatutilia mapato tuweze kufanya kazi nao, tuweze kuwatekelezea yale mahitaji yao.

Kwa mfano umezungumzia magari ya zimamoto *airport na x-ray machine airport*, hivi sasa nataka nikuhakikishie kwamba tuko kwenye harakati za kukamilisha haya yote mawili kwa pamoja. Tunataka tununue magari ya zimamoto, *specification* tayari tumeshampatia mtu ambaye atakaye-*supply* hayo magari. Tunataka tununue *x-ray*

hizi tumeshapata kampuni ambazo tunataka zituletee hizo *x-ray machines* zote. Haya ndio muhimu ya kuharakisha kama serikali, ili taasisi ile iweze kuyapata.

Mhe. Asha Bakari umezungumzia kama Kamishna je yeye hashtakiwi, hakuna mtendaji, hakuna mtu yoyote *above the law* hakuna hata mmoja *above the law*. Kamishna akifanya makosa na ikithibitika kwamba kafanya kosa atapaswa kupelekwa katika vyombo vya sheria. Kamishna akitudokolea fedha zetu ikithibitika kwamba Kamishna kazidogokoa, atapaswa kupelekwa kwenye vyombo vya sheria, hakuna mtu *above the law*, hilo nilikuwa nataka niliweke wazi.

Mhe. Suleiman Hemed mchangiaji wa mwisho nataka niseme hivi, kuna mambo mawili hapa lazima uyazingatie; kufunga biashara katika kuharakisha ulipaji wa kodi mimi mwenyewe nimeshashuhudia watu wanafungiwa biashara zao, wanaekewa kufuli anakwenda mbio kulipa ili ifunguliwe. Katika kuharakisha ile kodi katika *measurews* za mwanzo ambazo ZRB wanatakiwa wafanye ni kufunga kwanza kabla hawajachukua hatua nyengine za kisheria, *of course* na hiyo ni sheria iko kwenye sheria. Lakini inapaswa uzingatie ukiona umeshatia kufuli lakini bado huyu mtu mfanyabiashara hajakimbilia kulipa kodi na mle ndani kuna *products* za kuharibika haraka utamtia hasara huyu mtu, lazima uondoe zile *products* ziuzwe. Sijui tumefahamiana Mheshimiwa. Ili usimtie hasara zaidi lazima zile product uziondoe, lakini ukiona kwamba amechukua muda mrefu nacho kitu gani kitakachokufanya wewe ulipe ile kodi, ni kuiuza ile *product* yake.

Sasa haya yote yanakwenda katika hatua na kuangalia ile *product* yenyewe iliyomo mule ndani. Sio kama unachukua hatua zote mbili kwa mpigo unaangalia kwanza ukiweka kufuli je, amekimbilia kuja kulipa unafungua aendelee na mali yake. Kwa sababu sio kila mfanyabiashara kwamba pesa zake ni zile ziliomo ndani ya duka tu, wengine wana *account* zao ziko benki pale.

Sisi kwa mujibu wa sheria zetu unaweza ukaizuia mpaka ukamwambia Meneja Mkuu wa benki kwamba zuia hiyo *account*, kwa mujibu wa sheria zetu za kodi hiyo account mpaka nilipwe. Sasa hizi ni hatua ambazo tunataka tuzifanye ili kurahisisha kuipata ile kodi. Kodi tunaihitajia na tunaitaka tuipate kwa wakati unaostahiki kulipwa kodi.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo ninawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe na sasa naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Ahsante sana, Waheshimiwa Wajumbe baada ya ufafanuzi wa Mhe. Waziri naomba sasa niwahoji. Wale wanaokubaliana na hoja ya mswada huu wa kurekebisha kodi na sheria za kodi wanyanyue mikono. Wanaokataa. Waliokubali wameshinda. *(Makofi).*

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Spika, sasa naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako tukufu likae kama kamati ya kutunga sheria ili kuupitia mswada huu kifungu baada ya kifungu. Ahsante.

KAMATI YA KUTUNGA SHERIA

Mswada wa Sheria ya Kutoza Kodi na Kubadilisha baadhi ya Sheria za Fedha na Kodi kuhusiana na Ukusanyaji na Udhibiti wa Mapato Ya Serikali na Mambo Mengine yanayohusiana na hayo pamoja na Marekebisho yake

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe mtakumbuka kwamba hata hili jina la mswada limekuwa na marekebisho. Inakubaliwa. Ndio.

Sehemu ya Kwanza

Utangulizi

Kifungu 1 Jina fupi na kuanza kutumika.

Sehemu ya Pili

Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Kodi Namba 7
Ya Mwaka 2009

Kifungu 2 Kusomwa
Kifungu 3 Marekebisho ya Kifungu cha Tatu
Kifungu 4 Marekebisho ya Kifungu cha 18 pamoja na marekebisho yake
Kifungu 5 Marekebisho ya Kifungu cha 22
Kifungu 6 Marekebisho ya Kifungu cha 31
Kifungu 7 Marekebisho ya Kifungu cha 36 pamoja na marekebisho yake
Kifungu 8 Marekebisho ya Kifungu cha 41
Kifungu 9 Marekebisho ya Kifungu cha 43 pamoja na marekebisho yake
Kifungu 10 Marekebisho ya Kifungu cha 51 pamoja na marekebisho yake
Kifungu 11 Kuongezwa Kifungu kipya cha 54(a) pamoja na marekebisho yake
Kifungu 12 Marekebisho ya Kifungu cha 56 pamoja na marekebisho yake
Kifungu 13 Marekebisho ya Kifungu cha 62 pamoja na marekebisho yake
Kifungu 14 Kuongezwa Kifungu kipya cha 62(a)
Kifungu 15 Marekebisho ya kifungu cha 68

Sehemu ya Tatu

Marekebisho ya Sheria za Kodi ya Mafuta Namba 7
Ya Mwaka 2001

Kifungu 16 Kusomwa
Kifungu 17 Marekebisho ya Kifungu cha 13

Sehemu ya Nne

Marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani Namba4
Ya Mwaka 1998

Kifungu 18 Kusomwa
Kifungu 19 Marekebisho ya Kifungu cha 2
Kifungu 20 Marekebisho ya Kifungu cha 26(a)

Sehemu ya Tano

Marekebisho ya Sheria ya Bodi ya Mapato Zanzibar Namba 7
Ya Mwaka 1996

Kifungu 21 Kusomwa
Kifungu 22 Marekebisho ya Kifungu cha 5
Kifungu 23 Marekebisho ya Kifungu cha 15
Kifungu 24 Marekebisho ya Kifungu cha 15(a) pamoja na marekebisho yake
Kifungu 25 Marekebisho ya Kifungu cha 29

Sehemu ya Sita

Marekebisho ya Sheria ya Rufaa ya Kodi Namba 1
Ya Mwaka 2006

Kifungu 26	Kusomwa
Kifungu 27	Marekebisho ya Kifungu cha 4 pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 28	Marekebisho ya Kifungu cha 5
Kifungu 29	Marekebisho ya Kifungu cha 15

Sehemu ya Saba

Marekebisho ya Sheria ya Usafiri Barabarani Namba7
Ya Mwaka 2013

Kifungu 30	Kusomwa
Kifungu 31	Marekebisho ya Kifungu cha 86

Marekebisho ya Sheria ya Kazi Namba 11
Ya mwaka 2005

Kifungu 32	Kusomwa
Kifungu 33	Marekebisho ya Kifungu cha 40
Kifungu 34	Marekebisho ya Kifungu cha 98

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Fedha: Ilivyokuwa Kamati ya Kutunga Sheria imeupitia mswada wangu kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake, sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wanaokubaliana na mswada pamoja na marekebisho yake wanyanyue mikono. Wanaokataa. Waliokubali wameshinda. *(Makofi).*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2014

(Kusomwa kwa mara ya tatu)

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kuwa Mswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2014 usomwe kwa mara ya tatu.

Mhe. Spika: Niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wanaokubaliana na mswada kusomwa mara ya tatu wanyanyue mikono. Wanaokataa, Waliokubali wameshinda. *(Makofi).*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Mswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa mara ya tatu na kupitishwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe ninakushukuruni kwa kazi nzuri, mumempa nguvu sasa Mhe. Waziri akakusanye hizo pesa, ili aweze kumudu kutekeleza bajeti ambayo umepitisha mapema kabla ya mswada huu. Baada ya kazi hiyo nzuri Waheshimiwa Wajumbe sasa tusitishe shughuli zetu hadi saa 11.00 jioni.

(Saa 6.44 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11.00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

HOJA ZA SERIKALI

MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015 – WIZARA YA NCHI OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajummbe kwa heshima kubwa sasa naomba jioni hii tumkaribishe Mhe. Makamu wa Pili wa Rais. Mheshimiwa Makamu karibu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Mapato na Matumizi ili lipokee, lijadili na hatimae liidhinishe Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2014/2015.

Mhe. Spika, tumekutana tena katika Kikao hiki cha Nne cha Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye Muundo wa Umoja wa Kitaifa kwa mwaka wa fedha 2014/2015 kwa ajili ya kuzungumzia mipango na masuala muhimu ya nchi yetu kwa nia ya kuleta maendeleo ya nchi na wananchi wake. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uwezo huu wa kukutana tena na ninamuomba aendelee kutupa afya njema na kutuwezesha kuendesha kikao chetu hiki kwa hekima, busara na uadilifu mkubwa. Ni imani yangu kuwa tutamaliza kikao hiki tukiwa tunaendelea kubakia wamoja na wenye mshikamano mkubwa katika kuendeleza nchi yetu.

Mhe. Spika, nachukua nafasi hii kumshukuru kwa dhati Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein kwa kuiongoza nchi yetu kwa umahiri na umakini mkubwa. Sote ni mashahidi kuwa chini ya uongozi wa Dkt. Ali Mohammed Shein, nchi yetu imeendelea kupata mafanikio makubwa katika nyanja zote za kiuchumi, kijamii na kisiasa. Aidha, nchi yetu imeendelea kuwa katika hali ya amani na utulivu mkubwa, hali ambayo imetoa nafasi kwa wananchi kuendelea na shughuli zao za maisha za kila siku bila bughudha wala usumbufu wowote. Namuomba Mwenyezi Mungu aendelee kumpa afya njema na umri mrefu yeye na familia yake, amzidishie hekima na busara ili aendelee kutuongoza katika hatua za kuiletea nchi yetu maendeleo zaidi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, vile vile nachukua nafasi hii kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Makamu wa Kwanza wa Rais, Maalim Seif Sharif Hamad kwa kuendelea kumsaidia na kumshauri vyema Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapindunzi na kwa mashirikiano yake mazuri kwa ofisi yangu.

Mhe. Spika, pongezi za pekee nazitoa kwako wewe mwenyewe binafsi Mheshimiwa Spika kwa jinsi unavyoliendesha Baraza letu hili kwa umahiri na umakini mkubwa kwa kufuata sheria na kanuni za Baraza. Uongozi wako wa busara kwa hakika umeimarisha demokrasia ndani ya Baraza hili na kulipa Baraza letu mafanikio makubwa katika kutekeleza majukumu yake. Tunakuombea kwa Mwenyezi Mungu akuzidishie uwezo na hekima katika kutekeleza majukumu yako makubwa katika taifa letu. Pia napenda kuwapongeza kwa dhati Naibu Spika, Mhe. Ali Abdalla Ali, Mwakilishi wa Jimbo la Mfenesini na Wenyeviti wa Baraza Mhe. Mgeni Hassan Juma, Mwakilishi wa Viti Maalumu na Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa, Mwakilishi wa Jimbo la Kikwajuni kwa namna wanavyokusaidia katika kuliendesha Baraza letu hili.

Mhe. Spika, naomba nitumie fursa hii pia kuwashukuru Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi kwa kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa malengo na maagizo mbalimbali wanayoyatoa kwa Wizara wanazozisimamia. Aidha, natoa shukrani maalum kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa Mhe. Hamza Hassan Juma, Mwakilishi wa Jimbo la

Kwamtipura, Makamu Mwenyekiti Mhe. Saleh Nassor Juma Mwakilishi wa Jimbo la Wawi na Wajumbe wote wa Kamati hiyo, kwa kuyapitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na kutupa ushauri unaotuongoza na kutusaidia katika utekelezaji wa malengo na majukumu ya ofisi yetu.

Mhe. Spika, pia nawapongeza Wajumbe wote wa Baraza hili tukufu kwa kuipitisha Bajeti ya Serikali iliyowasilishwa na Mhe. Waziri wa Fedha. Bajeti hiyo ndiyo itakayotuwezesha kuendesha kazi za Serikali katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/2015.

Mhe. Spika, maelezo ninayoyasoma hapa ni muhtasari wa hotuba yangu iliyomo katika kitabu changu cha Hotuba ya Bajeti ya mwaka wa fedha 2014/2015 kilichowasilishwa katika Baraza hili. Hii ni kwa sababu ya muda. Aidha, naomba maelezo yaliyomo katika kitabu hicho cha bejeti yangu yaingie katika *hansard* kama yalivyo.

HALI YA KISIASA

Mhe. Spika, tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kuijaalia nchi yetu amani na utulivu. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2013/2014 hakukua na matukio makubwa ya uvunjifu wa amani yaliyotokea katika nchi yetu. Hali hii inatokana na wananchi wengi kuzidi kuelewa umuhimu wa amani na kushirikiana na serikali yao kudumisha amani na utulivu kwa maendeleo ya taifa letu na ustawi wa jamii.

Mhe. Spika, kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2013/2014, nchi yetu imefanya chaguzi ndogo mbili (2) ambazo zilihusisha Uchaguzi wa Mwakilishi wa Jimbo la Kiembesamaki Wilaya ya Magharibi Unguja na Uchaguzi wa Diwani Wadi ya Kiboje Wilaya ya Kati Unguja**.** Tunavishukuru vyama vyote vya siasa vilivyoshiriki katika chaguzi hizo ambazo ziliendeshwa kwa haki, uwazi, amani na utulivu mkubwa.

Aidha, tunawapongeza sana viongozi walioshinda katika chaguzi hizo na tunawatakia mafanikio katika kuwatumikia wananchi waliowachagua na nchi yetu kwa ujumla. Vile vile nachukua nafasi hii kuwashukuru na kuwapongeza sana wananchi wa Jimbo la Kiembesamaki na wananchi wa Wadi ya Kiboje kwa kuweza kutumia demokrasia yao vizuri kuwachagua viongozi wao kwa imani ya kuwaletea maendeleo katika maeneo yao. *(Makofi)*

MAADHIMISHO YA SHEREHE ZA MIAKA 50 YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

Mhe. Spika, katika mwaka huu wa fedha, nchi yetu imeadhimisha Miaka 50 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar. Maadhimisho ya Sherehe hizo yalizinduliwa rasmi tarehe 15 Agosti, 2013 na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohamed Shein na kufikia kilele chake tarehe 12 Januari, 2014, Uwanja wa Amani, Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa muda wote wa maadhimisho haya hadi siku ya kilele tumeshuhudia shughuli na matukio mbali mbali ambayo wananchi na viongozi walishiriki kikamilifu katika maeneo yote ya Unguja na Pemba. Miongoni mwa matukio hayo ni Maonesho ya Miaka 50 ya Mapinduzi yaliyofanyika katika viwanja vya Chuo Kikuu cha Taifa (*SUZA*), Kampasi ya Beit el Ras kuanzia tarehe 2 – 5 Januari, 2014; Maonesho ya Fensi; Maonesho ya Biashara yaliyofanyika katika viwanja vya Maisara; Utoaji wa Nishani kwa viongozi na wananchi mbali mbali waliotoa mchango wao katika Mapinduzi ya Januari 12, 1964 pamoja na waliochangia katika maendeleo ya Zanzibar kwa jumla.

Pia palifanyika Matamasha ya Michezo na Burudani, Ujenzi wa Mnara wa Kumbukumbu ya Miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar hapo Michenzani, Uwekaji wa jiwe la msingi na uzinduzi wa miradi ya maendeleo mbali mbali na mwisho maonesho mbali mbali yaliyofanywa siku ya kilele katika Uwanja wa Amani.

Mhe. Spika, sote ni mashahidi kwa namna sherehe zetu zilivyokuwa zimefana sana na kuleta haiba kubwa kwa nchi yetu. Hii imeonesha jinsi gani wananchi wetu wanavyothamini Mapinduzi yetu ya Januari 1964 pamoja na maendeleo wanayoyaona kutokana na Mapinduzi hayo.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kutoa pongezi na shukurani zangu za dhati kwa wananchi na viongozi wote walioshiriki kwa njia moja au nyengine katika kufanikisha Maadhimisho ya Sherehe hizo. Ni matumaini

yangu kuwa sote kwa umoja wetu tutaendelea kudumisha Mapinduzi haya ili kuendeleza amani na maendeleo katika nchi yetu.

Mhe. Spika, pamoja na kutoa pongezi hizo, naomba kutoa masikitiko yangu kuona kwamba hadi leo hii wapo watu wachache miongoni mwetu ambao wanauliza uhalali wa Mapinduzi Matukufu ya Mwaka 1964. Ni dhahiri kwamba hata hawa wanaohoji uhalali wa Mapinduzi kwa kiasi kikubwa wamefaidika na Mapinduzi haya. Mwenye macho haambiwi tazama, kwani baada ya Mapinduzi ya 1964 ndio nchi hii imeshuhudia mafanikio makubwa ya maendeleo katika nyanja zote. Hivyo, hatuna budi kuyalinda na kuyaendeleza Mapinduzi yetu kwa manufaa yetu na vizazi vijavyo.

Mhe. Spika, dhana ya Mapinduzi ilikuwa ni kuleta maisha bora kwa kila Mzanzibari na kuondoa ubaguzi wa aina zote na kuleta umoja na maendeleo na ndio kilichofanyika. Haya mengi ambayo leo tunayaona hayakuwepo kabla ya Mapinduzi ambayo ni pamoja na kuwepo kwa nyumba bora za kuishi, nyumba bora kwa wazee, kuimarika kwa huduma za elimu, afya na kupatikana kwa maendeleo makubwa katika Sekta ya Miundombinu, Kilimo, Maji na Umeme, Uchumi na Biashara, na kuwepo kwa uhuru wa kushiriki shughuli za kisiasa.

Mhe. Spika, naomba tuelewe kwa nini tunatoa kipaumbele katika kuweka kumbukumbu za Mapinduzi hasa katika maadhimisho yake. Kwa kweli ni jambo la ajabu kuona miongoni mwetu bado wapo watu wanaohoji umuhimu wa Sherehe za Mapinduzi au kuweka vielelezo vya Mapinduzi. Tunasema tutaendelea kuenzi na kuheshimu kazi nzuri iliyofanywa na Wazee wetu ya kutukomboa na kutupatia Uhuru wa nchi yetu.

Mhe. Spika, kwa ajili ya kuweka kumbukumbu ya kutimiza miaka 50 ya Mapinduzi, serikali kwa makusudi imefanya uamuzi wa kujenga Mnara katika eneo la Michenzani. Hii inatokana na historia ya eneo hilo katika harakati za kuikomboa nchi yetu. Aidha, serikali ina dhamira ya dhati ya kuendeleza azma ya Marehemu Mzee Abeid Amani Karume ya kuendeleza eneo hilo na kulifanya kuwa eneo la biashara na kuwa kivutio kwa wageni, watalii na wananchi kwa ujumla.

Mhe. Spika, mnara unaoendelea kujengwa utakuwa pia ni kituo kwa wananchi na wageni kusoma historia ya Mapinduzi na waanzilishi wake, kwani kutakuwa na maktaba maalum. Katika eneo hilo kutakuwa na mkahawa na bustani ya mapumziko ambayo itasaidia sana kupunguza msongamano katika maeneo ya Forodhani hasa wakati wa sikukuu. Naomba wananchi waelewe kuwa mnara huo unajengwa kwa Fedha za Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*ZSSF*) na utaendeshwa kibiashara na kwa faida.

MASUALA YA MUUNGANO

Mhe. Spika, Muungano wa Tanganyika na Zanzibar hivi sasa umetimiza miaka 50 (Nusu Karne) tangu ulipoasisiwa tarehe 26 Aprili, 1964. Sherehe za kutimiza Miaka 50 ya Muungano wetu zilizinduliwa rasmi hapa Zanzibar na Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Tarehe 01 Machi, 2014 katika Ukumbi wa Salama, Hoteli ya Bwawani na kilele chake kilifanyika Dar es salaam tarehe 26 Aprili, 2014. Kipindi cha miaka 50 ni kirefu na nchi yetu ina kila sababu za kujivunia kutokana na kuudumisha Muungano wetu kwa kipindi chote hicho.
Yapo mafanikio mengi yanayotokana na Muungano, lakini makubwa kati ya mafanikio hayo ni kuwa na amani na utulivu katika nchi yetu. Aidha, Muungano huu umeweza kutoa fursa ya kuendeleza na kuimarisha mahusiano ya kidugu yaliyopo kati ya wananchi wa Tanzania Bara na Zanzibar.

Mhe. Spika, licha ya kuwa na mafanikio hayo, Muungano wetu huu umekuwa na changamoto katika baadhi ya maeneo ambazo zimekuwa zikipigiwa kelele na wananchi wa pande zote mbili za Muungano. Juhudi kubwa tayari zimechukuliwa na viongozi wetu katika kuzitafutia ufumbuzi changamoto hizo ili kuimarisha Muungano wetu huu wa kihistoria. Mambo ambayo mpaka sasa yameshapatiwa ufumbuzi kupitia Kamati Maalumu inayoongozwa na Mhe, Makamu wa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ni kama yafuatayo:-

- Utekelezaji wa Sheria ya Haki za Binaadamu;
- Utekelezaji wa "*Merchant Shipping Act*" katika Jamhuri ya Muungano na uwezo wa Zanzibar kujiunga na Shirika la Kimataifa la Usafiri Baharini [*International Maritime Organisation (IMO)*;

- Misamaha ya mikopo ya fedha kutoka *IMF*;
- Uwezo wa Zanzibar kukopa ndani na nje ya nchi;
- Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo wa SMT; na
- Kodi ya Mapato (Mgao wa Mapato yatokanayo na *PAYE*).

Mhe. Spika, pamoja na mambo ambayo yameshapatiwa ufumbuzi, kuna mambo ambayo yapo katika hatua nzuri ya kupatiwa ufumbuzi, mambo hayo ni kama yafuatayo:-

- Mgawanyo wa mapato yatokanayo na faida ya Benki Kuu;
- Utafutaji na uchimbaji mafuta na gesi asilia;
- Ushirikiano wa Zanzibar na Taasisi za Nje;
- Ajira kwa watumishi wa Zanzibar katika Taasisi za Muungano;
- Usajili wa vyombo vya moto;
- Tume ya pamoja ya fedha; na
- Ushiriki wa Zanzibar katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mhe. Spika, katika hotuba yangu hii, nimegusia masuala mbali mbali ya kiuchumi na kijamii ikiwemo hali ya uchumi na mipango ya serikali katika kuimarisha uchumi, uwezeshaji wananchi kiuchumi, sekta ya huduma ya kiuchumi, sekta ya huduma ya kijamii, masuala ya migogoro ya ardhi, masuala mtambuka pamoja na sekta ya utumishi na maslahi ya wafanyakazi. Masuala haya yameelezwa kwa kina kuanzia ukurasa wa 12 mpaka ukurasa wa 24 katika kitabu cha hotuba ya makadirio.

HALI YA UCHUMI NA MIPANGO YA SERIKALI YA KUIMARISHA UCHUMI

Mhe. Spika, Uchumi wa Zanzibar umeendelea kuonesha mwenendo mzuri na umeendelea kukua kwa asilimia 7.4 mwaka 2013 kutoka asilimia 7.1 mwaka 2012. Uchumi huu umekua kwa kipindi cha miaka minne (4) kutoka asilimia 6.4 mwaka 2010 hadi kufikia asilimia 7.4 mwaka 2013. Pato la Taifa kwa bei za miaka husika limefikia jumla ya Sh. 1,442.8 bilioni kwa mwaka 2013 kutoka Sh. 1,342.6 bilioni kwa mwaka 2012.

Mhe. Spika, mwaka 2013 pato la kila mtu limeongezeka kufikia wastani wa Sh. 1,077,000 (USD 667) kutoka wastani wa Sh. 1,030,000 (USD 656) kwa mwaka 2012 sawa na ongezeko la asilimia 4.3. Ukuaji huu mkubwa wa Uchumi umechangiwa na mambo yafuatayo:-

i. Kuimarika kwa Sekta ya Kilimo, Misitu na Uvuvi ambayo imekua kutoka asilimia 2.0 mwaka 2012 hadi asilimia 3.6 mwaka 2013;
ii. Kuimarika kwa baadhi ya Sekta ya Viwanda kulikochangiwa na ongezeko la ukuaji wa Sekta ndogo ya uzalishaji viwandani kutoka asilimia 0.1 kwa mwaka 2012 hadi asilimia 3.2 mwaka 2013;
iii. Kuimarika kwa Sekta ya huduma kulikochangiwa na ongezeko la ukuaji wa Sekta ndogo za Hoteli na Mikahawa kutoka asilimia 0.2 mwaka 2012 hadi asilimia 6.5 mwaka 2013, Sekta ya Utawala wa Umma kutoka asilimia 0.3 mwaka 2012 hadi asilimia 3.4, mwaka 2013 na Sekta ya Elimu kutoka asilimia 1.2 mwaka 2012 hadi asilimia 3.5 mwaka 2013; na
iv. Kuongezeka kwa idadi ya Watalii wanaoingia nchini kutoka Watalii 169,223 mwaka 2012 hadi kufikia Watalii 181,301 mwaka 2013 sawa na ongezeko la asilimia 7.1.

Mhe. Spika, mafanikio ya kukua kwa Uchumi yanatokana pamoja na sababu zilizotajwa hapo juu, na hali ya utulivu, amani na mshikamano wa wananchi ambayo imejenga mazingira mazuri ya kuwekeza na kufanyakazi kunakoleta tija kwa nchi.

UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI

Mhe. Spika, katika jitihada za kuwainua wananchi kiuchumi, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeshazindua Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Mfuko huo wenye thamani ya shilingi 1.1 bilioni utatoa mikopo kwa wananchi wa makundi mbalimbali yakiwemo kundi la vituo vya kutotolea wajasiriamali, kundi la watu wenye ulemavu, kundi la wanawake na kundi la vijana waliomaliza masomo katika vyuo na Skuli za

Sekondari. Pamoja na uzinduzi wa Mfuko huu juhudi nyengine za Serikali katika kuwawezesha wananchi kiuchumi ni kuanzisha kituo cha kulelea na kutotoa wajasiriamali (*Incubator Centre*), kuendeleza Kongano (*Clusters*) sita (6) zilizopo na kuanzisha Kongano nyengine tofauti.

Mhe. Spika, natoa wito kwa wananchi waache ile taabia ya kuona kuwa ajira ni ile ya serikalini. Hivyo basi tunawaomba watumie fursa zilizopo ili kuweza kujiajiri wenyewe na kuendeleza maisha yao ya kila siku.

SEKTA YA HUDUMA ZA KIUCHUMI

Mhe. Spika, katika kuimarisha huduma za kiuchumi Serikali inaendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya uimarishaji wa miundombinu ya usafiri ikiwemo miundombinu ya barabara, Bandari na Viwanja vya Ndege. Kwa upande wa barabara, Serikali inaendeleza ujenzi wa barabara mbalimbali Unguja na Pemba pamoja na kutafuta rasilimali kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa barabara zinazoingia ndani ya mji wa Zanzibar.

Mhe. Spika, kuhusu kuimarisha usafiri wa anga Serikali inaendelea na kukiimarisha Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Abeid Amani Karume Unguja na Uwanja wa Ndege wa Pemba kwa upanuzi wa njia za kurukia na kuegeshea ndege na ujenzi wa majengo mapya ya abiria pamoja na uwekaji wa taa katika kiwanja cha Pemba.

Kwa upande wa Sekta ya Mawasiliano, Serikali imekamilisha kuandaa Sera ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano Zanzibar (TEHAMA) ambayo itatoa muongozo wa matumizi mazuri ya TEHAMA kwa Zanzibar.

Aidha, Serikali inaendelea kuziunganisha Wizara na Taasisi za Serikali katika Mkonga wa Mawasiliano na hadi sasa jumla ya Wizara na Taasisi 56 kati ya 83 zimeshaunganishwa na Mkonga huo.

Mhe. Spika, kukamilika kwa Mradi wa kulaza waya mpya wa umeme wenye uwezo wa kuchukua "*MegaWatts*" 100 na mradi wa uimarishaji wa miundombinu ya ndani ya umeme imeimarisha upatikanaji wa huduma za umeme nchini na kutoa muelekeo kwa kuendelea kukua kwa uchumi wa Zanzibar kwani uwekezaji hasa katika maeneo ya Viwanda, Utalii na Biashara utaongezeka kwa kuwepo umeme wa uhakika.

Pamoja na hatua hii iliyofikiwa ya kupatikana kwa umeme, Serikali kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo inafanya uchambuzi yakinifu (*Feasibility Study)* katika masuala ya nishati mbadala ikiwemo umeme. Pia, hivi sasa Serikali imo katika kuandaa wataalam wa gesi na mafuta ili kuweza kukabiliana na upungufu wa wataalam wa fani ya nishati ikiwemo utafutaji na uchimbaji wa mafuta hapa nchini.

SEKTA YA HUDUMA ZA JAMII

Mhe. Spika, maji ni rasilimali ya kimaumbile na ya msingi ambayo ni muhimu kwa kuendeleza maisha. Umuhimu wa matumizi yake unaonekana kwenye mahitaji ya majumbani, viwandani na matumizi mengine mbalimbali ya kijamii. Serikali inaendelea na mipango ya kuwapatia wananchi maji safi na salama. Mipango hiyo ni pamoja na uhuishaji, upanuzi na usambazaji wa maji mijini na vijijini inayohusisha uchimbaji wa visima zaidi ya 50, ujenzi wa matangi ya maji, ununuzi na uwekaji wa pampu mpya, ulazaji wa mabomba, ujenzi wa vibanda vya kuwekea pampu za maji na ufungaji wa mita kwa wateja.

Mhe. Spika, katika kuendeleza upatikanaji na utoaji wa huduma ya maji kwa wananchi, Serikali inaendelea na mipango yake ya kulinda na kuhifadhi vyanzo vya maji kwa kujenga uzio katika vyanzo mbalimbali vya maji na kusogeza karibu huduma za malipo ya maji kwa wananchi kwa kujenga vituo vya kulipia maji katika sehemu mbalimbali nchini.

Mhe. Spika, serikali inaendelea kuwaomba wananchi kuthamini mipango mbalimbali ya kuimarisha upatikanaji wa maji kwa kuongeza ulinzi kwenye miundombinu ya maji na uhifadhi wa vyanzo vya maji kwa kupanda miti.

Mhe. Spika, kwa upande wa sekta ya Elimu, Serikali inaendelea na juhudi zake za kuwapatia elimu bora wananchi wa Zanzibar. Juhudi hizo ni pamoja na kujenga majengo ya kisasa kwa skuli za Sekondari na Msingi katika Wilaya za Unguja na Pemba, kuajiri walimu zaidi ya 700 walio na Shahada na Stashahada katika masomo ya Sayansi kwa mwaka 2014/2015.

Aidha, Serikali inaendelea kutoa mafunzo kazini kwa Walimu yakiwemo ya matumizi ya Lugha ya Kiingereza kwa kufundishia na mafunzo ya matumizi ya Kompyuta. Vilevile Serikali itanunua Vifaa vya Maabara kwa Skuli 100 za Sekondari na Kompyuta kwa Skuli mbili zenye Mchepuo wa Sayansi ya Kompyuta.

Pia, juhudi hizo za kuimarisha ubora wa elimu ni pamoja na kuandika na kuchapisha Vitabu vya kiada na Miongozo ya Walimu wa Madarasa ya Tano hadi Darasa la Saba. Serikali vilevile imepanga kuimarisha matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika elimu kwa kuziunganisha Taasisi za elimu na Mkonga wa Taifa na kuendelea na juhudi za kutumia Teknolojia hii kama nyenzo ya kufundishia na kujifunza.

Mhe. Spika, kwa upande wa Sekta ya Afya, Serikali inaendelea na azma yake ya kuhakikisha wananchi wa Zanzibar wanapata huduma bora ya afya ili kufikia malengo ya Dira ya mwaka 2020. Katika kufikia azma hiyo, Serikali imeweka mikakati mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuimarisha mifumo ya utoaji wa huduma za afya kwa kuzingatia makundi maalum, kutumia mfumo mpya wa ununuzi wa dawa kupitia Mfumo wa Ununuzi wa Dawa kwa Awamu *(Framework Contract).*

Aidha, serikali imepanga kuongeza juhudi za kupata madaktari bingwa katika magonjwa mbalimbali na kuwa na vifaa tiba vya kutosha ili kuweza kutoa huduma zinazohitajika.

MIGOGORO YA ARDHI

Mhe. Spika, serikali bado inaendelea kulitafutia ufumbuzi wa kudumu suala la migogoro ya ardhi. Kwa kiasi kikubwa hali hii inatokana na tabia ya wananchi na baadhi ya viongozi kuuza au kukodisha ardhi bila kufuata sheria na taratibu ziliopo nchini. Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi tayari amelitolea maagizo mara kadhaa suala hili kwa kuwataka viongozi na wananchi kutojihusisha na mambo yoyote yanayopelekea kuwa na migogoro ya ardhi.

Mhe. Spika, hata hivyo, serikali inaendelea kuchukua juhudi mbalimbali ili kuhakikisha kuwa migogoro ya ardhi inapatiwa ufumbuzi wa kudumu kupitia vyombo vyake mbalimbali ikiwemo Mahakama ya Ardhi pamoja na Ofisi ya Mrajis wa Ardhi inayoshughulikia usajili wa ardhi na kuwatambua wenye haki ya matumizi ya ardhi husika. Naomba kusisitiza kwa kuwasihi viongozi katika ngazi zote na wananchi kwa ujumla kuacha kujiingiza katika mambo ambayo yanasababisha kutokea kwa migogoro ya ardhi.

MASUALA MTAMBUKA

UKIMWI

Mhe. Spika, serikali inaendelea na juhudi za kupambana na maradhi ya UKIMWI. Kwa kupitia Mipango na Programu mbalimbali juhudi zinaelekezwa katika kutoa elimu na kudhibiti maambukizi mapya. Aidha, Serikali inaendelea kuwaelimisha wananchi kuacha kuwanyanyapaa wale wote ambao kwa bahati mbaya tayari wameshapata maambukizi ya virusi vinavyosababisha UKIMWI.

Watu Wenye Ulemavu

Mhe. Spika, **s**erikali inasimamia utekelezaji wa Mkakati wa kuwapatia haki watu wenye ulemavu na kuwajumuisha katika masuala mbalimbali ya kiuchumi, kijamii na kisiasa. Kwa sasa kumezuka wimbi kubwa la ubakaji wa watu wenye ulemavu. Serikali itahakikisha kuwa wale wote wanaohusika na vitendo hivi vya udhalilishaji wanapatikana na kuchukuliwa hatua kali kwa mujibu wa sheria. Watu wenye ulemavu ni binaadamu kama binaadamu wengine hivyo wanastahiki haki na usawa katika jamii kwa nyanja zote. Tusisahau kuwa na sisi pia ni walemavu watarajiwa.

Mapambano Dhidi ya Dawa za Kulevya

Mhe. Spika, madawa ya kulevya ni moja ya matatizo makubwa ya kiuchumi na kijamii duniani kwa sasa kutokana na athari wanazozipata watumiaji wa dawa hizo ambao wengi wao ni vijana. Zanzibar nayo inakabiliwa na tatizo kubwa la uingizwaji na matumizi ya dawa za kulevya. Janga hili limewakumba vijana wengi ambao ni tegemeo la nchi katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Serikali itasimamia utekelezaji wa Sheria ya Dawa za Kulevya na kudhibiti njia zote za uingizwaji wa dawa hizo na kuwachukulia hatua kali za kisheria wale wote wanaohusika na uingizaji na utumiaji wa dawa hizo. Aidha, Serikali itaendelea kutoa elimu kwa wananchi wote juu ya madhara ya matumizi ya dawa za kulevya na kuwasaidia wale wote walioacha matumizi ya dawa hizo. Serikali inazidi kutoa wito kwa wananchi kuachana na tabia ya kuingiza na kutumia dawa za kulevya ili kuinusuru nchi na janga hili.

Mazingira

Mhe. Spika, suala la kutunza mazingira lina umuhimu mkubwa sana katika kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii na kupunguza umasikini wa wananchi. Suala la mabadiliko ya tabianchi pia limeendelea kuleta athari mbalimbali za kimazingira katika maeneo yetu. Katika kuendeleza juhudi ya kukabiliana na hali ya uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi, Serikali itasimamia sheria na kanuni za utunzaji wa maliasili zisizorejesheka, kutoa elimu juu ya utunzaji wa mazingira na kusimamia utekelezaji wa mkakati wa mabadiliko ya tabianchi ikiwa ni pamoja na masuala ya mabadiliko ya tabianchi kuingizwa katika mipango ya maendeleo ya sekta mbalimbali nchini.

Mhe. Spika, serikali itaendelea kusimamia utekelezaji wa Programu ya upandaji miti katika maeneo mbalimbali ikiwemo katika vyanzo vya maji, misitu ambayo imeathirika na ukataji miti na maeneo ya wazi yaliyoathirika na ukataji wa miti ovyo. Ni vyema wananchi wakazingatia suala zima la utunzaji wa mazingira kwani athari zake kwa nchi ya kisiwa kama Zanzibar ni kubwa.

SEKTA YA UTUMISHI NA MASLAHI YA WAFANYAKAZI

Mhe. Spika, Moja ya vipaumbele vya Serikali ya Awamu ya Saba (7) ni kuimarisha sekta ya utumishi wa umma na maslahi ya wafanyakazi ikiwa na lengo la kuwepo kwa ufanisi na uwajibikaji katika utendaji wa shughuli za utumishi, uadilifu na usimamizi mzuri wa rasilimali za umma. Ili kufikia lengo hili serikali imetekeleza mageuzi makuu ya msingi yakiwemo mageuzi ya utumishi wa umma na kuimarisha serikali katika masuala ya uwajibikaji na uongozi.

Mhe. Spika, mageuzi haya yamejumuisha mambo yafuatayo:-

i. Kufanya tathmini na ufuatiliaji wa utekelezaji wa Miundo ya Utumishi wa Wizara, Idara na Taasisi zote za Serikali;
ii. Kuimarisha utendaji wa taasisi za umma ikiwemo miundombinu, mifumo ya utoaji huduma, kusimamia na kuendeleza watumishi wa umma pamoja na mageuzi ya Serikali za Mitaa;
iii. Kufanya Tathmini ya Uchambuzi wa Kazi na Madaraja (*Job Evaluation and Grading*);
iv. Kufanya tathmini ya idadi ya watumishi wa umma na majukumu yaliyopo; na
v. Kuandaa Mpango Mkakati wa Sera ya Malipo na Sera ya Uhifadhi Kumbukumbu na Nyaraka.

Mhe. Spika, pamoja na mipango hiyo Serikali itaendelea kutoa umuhimu kwa mafunzo kwa Watumishi wa Umma kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu, muda mfupi na semina elekezi ili kuwajengea uwezo wafanyakazi katika kutekeleza majukumu yao. Aidha, serikali imefanya marekebisho makubwa ya mishahara, kwa kuongeza mishahara ya wafanyakazi kwa mujibu wa viwango vya elimu na uzoefu kazini.

MWELEKEO WA VIPAUMBELE VYA OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

Mhe. Spika, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais katika kutekeleza majukumu yake katika mwaka wa fedha 2014/2015 imejipangia kutekeleza vipaumbele vifuatavyo:-

i. Kuimarisha huduma za usafiri na makaazi ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais;
ii. Kuongeza hadhi katika Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa;
iii. Kujenga uwezo wa kiutendaji kwa wafanyakazi wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kuwapatia mafunzo na vitendea kazi;
iv. Kujenga uwezo wa jamii katika kujikinga, kukabiliana na kuhimili majanga na maafa;
v. Kushughulikia malalamiko na migogoro ya wananchi kwa kushirikiana na Sekta husika.;
vi. Kusimamia masuala ya utafiti kwa kuzingatia vipaumbele vya taifa vya utafiti (*National Research Agenda*);
vii. Kuweka Muundo mpya wa Kitaasisi na Kiutumishi wa Ofisi ya Uratibu wa Shughuli za Serikali Dar es Salaam utakaoongeza ufanisi na tija;
viii. Kuongeza mapato yatokanayo na kuongezeka kwa huduma za upigaji chapa;
ix. Kuandaa mazingira bora kwa ajili ya kufanikisha Uchaguzi Mkuu wa 2015, ikiwemo kutoa elimu ya Wapiga Kura, kufanya uchunguzi wa idadi, majina na mipaka ya majimbo na kufanya mapitio ya Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.; na
x. Kuendesha mikutano ya Baraza la Wawakilishi na kusimamia kazi za Kamati za Kudumu za Baraza.

UTEKELEZAJI WA MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014 NA MALENGO YALIYOPANGWA KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na taasisi zake ilikadiriwa kutumia jumla ya Sh. 30,066,506,000. Kati ya hizo Sh. 22,094,970,000 ni kwa kazi za kawaida na Sh. 7,971,536,000 ni kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia mwezi Machi 2014, Ofisi iliingiziwa Sh. 19,416,893,755 sawa na asilimia 65. Kati ya hizo Sh. 15,837,895,300 ni kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 72 na Sh. 3,578,998,455 kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia 45 kama inavyoonesha katika kiambatanisho 1A na 1B.

Mhe. Spika, baada ya kutoa taarifa za jumla za utekelezaji kifedha kwa mwaka 2013/2014, sasa naomba kutoa taarifa za utekelezaji kwa kila idara na taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

OFISI YA FARAGHA YA MAKAMU WA PILI WA RAIS

Mhe. Spika, Ofisi ya Faragha ina jukumu la kutoa huduma zote muhimu kwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais na familia yake pamoja na kutunza makaazi ya Makamu wa Pili wa Rais yaliyoko Mazizini Unguja, Dar es Salaam na Dodoma.

Mhe.Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Baraza lako Tukufu liliidhinisha jumla ya Sh. 780,034,000 kwa Idara ya Faragha. Hadi kufikia mwezi Machi, 2014 Idara iliingiziwa jumla ya Sh. 317,824,974 kwa ajili ya kazi za kawaida ambazo ni sawa na asilimia 41.

Mhe. Spika, katika mwaka 2013/2014 Ofisi ya Faragha imetekeleza kazi zifuatazo:-

i. Ununuzi wa vifaa muhimu vya kuendeshea ofisi;
ii. Kufanya matengenezo madogo madogo yamefanywa kwa makaazi ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais;
iii. Kuratibu mikutano ya Mhe.Makamu wa Pili wa Rais na Mabalozi na Wanadiplomasia wengine; na
iv. Kuratibu ziara za ndani na nje ya nchi kwa Makamo wa Pili wa Rais na kuratibu na kufatilia utekelezaji wa ahadi zilizotolewa na Kamamo wa Pili wa Rais.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015 Ofisi ya Faragha imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuimarisha Ofisi ya Faragha ya Makamu wa Pili wa Rais kwa ununuzi wa gari moja, samani na vifaa vya ofisi;
ii. Kuratibu ziara 20 za ndani ya nchi na mbili za nje ya nchi za Mhe. Makamu wa Pili wa Rais;

iii. Kuwajengea uwezo wafanyakazi wawili (2) wa Idara kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu pamoja na kulipa stahiki za likizo kwa wafanyakazi wanne (4);
iv. Kuimarisha makaazi ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa kuzifanyia matengenezo nyumba za Mazizini, Dar es Salaam na Dodoma; na
v. Kuimarisha uhusiano na ushirikiano na nchi na taasisi mbalimbali za ndani, kikanda na kimataifa.

Mhe.Spika, ili Ofisi ya Faragha iweze kutekeleza malengo yake kwa mwaka wa fedha 2014/2015 naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Sh 483,116,224 kwa matumizi ya Ofisi. Kati ya hizo Sh 330,616,224 kwa malipo ya mishahara, posho za wafanyakazi na michango ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii na Sh 152,500,000 kwa matumizi mengineyo.

IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI

Mhe. Spika, Idara ya Uendeshaji na Utumishi ina wajibu wa kusimamia stahiki za watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na kusimamia mafunzo kwa wafanyakazi. Aidha, Idara ina jukumu la kusimamia usalama na mazingira bora ya kazi pamoja na uendeshaji wa kazi za kila siku za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe.Spika**,** kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Baraza lako Tukufu liliidhinisha jumla ya Sh. 1,004,880,000 kwa Idara ya Uendeshaji na Utumishi. Hadi kufikia mwezi Machi, 2014 Idara iliingiziwa jumla ya Sh. 577,298,515 kwa kazi za kawaida ambazo ni sawa na asilimia 57.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Idara ya Uendeshaji na Utumishi imetekeleza kazi zifuatazo:-

i. Idara imeendelea kuratibu na kuwalipia ada na gharama nyengine za masomo kwa wafanyakazi 66 wanaoendelea na masomo ndani na nje ya nchi. Kulipia stahiki za wafanyakazi zikiwemo likizo kwa wafanyakazi malipo baada ya saa za kazi na kutayarisha mafao kwa watumishi waliostaafu;
ii. Kufanya Semina elekezi kuhusu Sheria ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2011; na
iii. Ununuzi wa vifaa kwa matumizi ya Ofisi.

Mhe.Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Idara ya Uendeshaji na Utumishi imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuweka mazingira mazuri ya kazi za idara kwa ununuzi wa vifaa vya Ofisi, samani pamoja na kulipia gharama za umeme na mawasiliano na utunzaji wa majengo;
ii. Kuwajengea uwezo wafanyakazi kumi (10) wa idara kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu pamoja na kulipa stahiki za likizo kwa wafanyakazi tisa (9);
iii. Kuufanyia mapitio Mpango wa Mafunzo kwa wafanyakazi pamoja na kuandaa utaratibu wa kutathmini utendaji na upandishaji vyeo wafanyakazi kwa kufuata muundo wa utumishi *Scheme of Service*; na
iv. Kusimamia matumizi bora ya fedha na vifaa vya Ofisi kwa kuandaa vikao vinne (4) kwa Kamati ya Uongozi, vikao vinne (4) Bodi ya Zabuni, Vikao vinne (4) vya Kamati ya Ukaguzi wa ndani na kulifanyia mapitio Daftari la Mali za Serikali.

Mhe. Spika, ili idara ya Uendeshaji na Utumishi iweze kutekeleza malengo yake kwa mwaka wa fedha 2014/2015 naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya Sh. 704,166,316. Kati ya hizo Sh. 514,166,316 ni kwa malipo ya mishahara, posho na mchango wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii na Sh. 190,000,000 ni kwa matumizi mengineyo.

IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

Mhe. Spika, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti inaendelea na jukumu la kusimamia masuala ya mipango, bajeti, sera na utafiti. Pia Idara hii ina jukumu la kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa miradi ya maendeleo pamoja na kutayarisha ripoti za utekelezaji wa shughuli za kawaida na miradi ya maendeleo kwa kipindi cha miezi mitatu, miezi sita, miezi tisa na mwaka mzima.

Mhe.Spika**,** kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Baraza lako Tukufu liliidhinisha jumla ya Sh. 295,240,000 kwa Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Hadi kufikia mwezi Machi, 2014 Idara iliingiziwa jumla ya Sh. 125,771,732 kwa kazi za kawaida ambazo ni sawa na asilimia 43.

Mhe.Spika, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti katika mwaka wa fedha wa 2013/2014 imetekeleza kazi zifuatazo:-

i. Idara imelipa stahiki za wafanyakazi wanne (4) waliokwenda likizo;
ii. Idara imefanya semina ya siku mbili kwa wafanyakazi juu ya Sheria ya Utumishi wa Umma;
iii. Idara imenunua vifaa vya kufanyia kazi ikiwemo Projekta moja (1), Printa moja (1) na vifaa vya kuandikia.
iv. Idara imefanya ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyo chini ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais;
v. Idara imeratibu utekelezaji wa Miradi ya Mfuko wa Dunia (Global Fund) ya Kupambana na UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria;
vi. Idara imeandaa Mpango Mkakati wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.;
vii. Idara imeandaa Bajeti na Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa mwaka wa fedha 2014/2015;
viii. Idara imeandaa ripoti za utekelezaji kwa shughuli za kawaida na Miradi ya maendeleo kwa robo mwaka, nusu mwaka na miezi tisa. Pia imefanya vikao vya kupitia na kutathmini ripoti hizo; na
ix. Idara imetoa vibali 110 vya kufanya utafiti katika sekta za mazingira, historia, kilimo, maliasili, misitu na elimu. Aidha, Idara imeratibu vikao vinne; viwili vya Kamati ya Taifa ya Utafiti na viwili kwa Kamati ya Wataalamu ya Kutafiti Rasilimali za Asilin
x. Idara kwa kushirikiana na *COSTECH* imetekeleza kazi zifuatazo:-

- Imeratibu kikao cha Kamati ya Taifa ya Wataalamu ya Rasilimali za Asili juu ya kupitia vipaumbele vya utafiti *National Research Agenda*;
- Imeratibu mkutano wa siku tatu wa mashirikiano baina ya Afrika ya Kusini na Tanzania juu ya masuala ya Utafiti; na
- Idara kwa kushirikiana na *COSTECH, SUZA* na Chuo Cha Sayansi ya Afya imeratibu na kushiriki Siku ya Utafiti na Ugunduzi ikiwa ni moja ya shughuli za maadhimisho ya sherehe za Miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Spika, Kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuweka mazingira mazuri ya kazi za idara kwa ununuzi wa vifaa vya ofisi na samani;
ii. Kuwajengea uwezo wafanyakazi 11 wa idara kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na wafanyakazi watatu (3) kwa mafunzo ya muda mrefu na kulipa stahiki za likizo kwa wafanyakazi watatu (3);
iii. Kuufanyia mapitio Mpango Mkakati wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na kutayarisha Miradi mitatu ya Maendeleo;
iv. Kuandaa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 na kufanya ziara nne (4) za ufuatiliaji wa kazi za Wizara na utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais;
v. Kuandaa vikao 12 vya Kamati ya Kisekta ya kuidhinisha Tafiti mbalimbali na Vikao vinne vya Kamati ya Taifa ya Kutafiti Rasilimali za Asili;
vi. Kwa kushirikiana na *COSTECH* kuwajengea uwezo watafiti wa wizara za SMZ kwa kuandaa warsha mbili pamoja na kuweka utaratibu mzuri wa utoaji wa vibali vya Utafiti; na
vii. Kuratibu utekelezaji wa Miradi ya Mfuko wa Dunia *Global Fund* ya Kupambana na UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria.

Mhe. Spika, Ili Idara ya Mipango, Sera na Utafiti iweze kutekeleza malengo yake katika mwaka wa fedha 2014/2015 naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya Sh 184,007,400 kwa matumizi ya Idara. Kati ya hizo Sh. 100,718,400 kwa ajili ya malipo ya mishahara, posho za wafanyakazi na mchango wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii na Sh. 83,289,000 kwa matumizi mengineyo.

IDARA YA URATIBU WA SHUGHULI ZA SERIKALI

Mhe. Spika, Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali ina jukumu la kuratibu Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Shughuli za Muungano ndani ya Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Baraza lako Tukufu liliidhinisha jumla ya Sh. 397,530,000 kwa Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali. Hadi kufikia mwezi Machi, 2014 Idara iliingiziwa jumla ya Sh. 223,282,110 kwa kazi za kawaida ambazo ni sawa na asilimia 56. Aidha, Idara iliidhinishiwa Sh. 840,000,000 kwa kazi za maendeleo ikiwa ni mchango wa SMZ. Kati ya hizo Sh. 80,000,0000 ni kwa Mradi wa *TASAF* na Sh. 760,000,000

kwa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo. Hadi kufikia Machi, 2014, Idara imeingiziwa Sh. 25, 000,000 kwa mradi wa *TASAF*, sawa na asilimia 31.

Mhe. Spika, katika mwaka 2013/2014 Idara imetekeleza kazi zifuatazo:-

i. Idara imefuatilia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2010 – 2015 katika Wizara za SMZ na Mikoa yote ya Unguja na Pemba na kuandaa taarifa ya utekelezaji kwa kipindi cha mwaka mmoja (Oktoba 2012 – Septemba 2013);
ii. Idara imetoa mafunzo ya kuwajengea uwezo wa kukusanya na kuandaa taarifa za utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi kwa Maafisa viungo wa Wizara, Maafisa Mipango wa Mikoa pamoja na Waratibu wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais;
iii. Idara imepokea na inaendelea kuyafuatilia malalamiko 15 (10 yanayohusiana na ardhi na 5 mambo mengine) yaliyowasilishwa na wananchi;
iv. Idara imeendelea kufuatilia utekelezaji wa ahadi nane (8) za Viongozi Wakuu wa Kitaifa zilizotolewa katika maeneo mbalimbali ya Unguja na Pemba wakati wa ziara zilizofanywa na viongozi hao;
v. Idara imefuatilia vikao vitatu (3) vya Baraza la Wawakilishi vilivyofanyika katika mwezi wa Oktoba Mkutano wa 14, Disemba Mkutano wa 15 na Januari Mkutano wa 16, Katika Mikutano hiyo jumla ya masuali 221 ya msingi yaliulizwa na kujibiwa. Pia, miswada Saba (7), Ripoti moja ya Kamati Teule na hoja binafsi moja ziwasilishwa;
vi. Idara imeratibu vikao saba (7) vya mashirikiano baina ya Wizara za SMZ na SMT ambapo vikao vitatu (3) vimefanyika baina ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali SMZ na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi SMT, vikao vitatu (3) baina ya Wizara ya Kilimo na Maliasili SMZ na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika SMT, kikao kimoja (1) baina ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu SMZ na SMT.;
vii. Idara imeendelea kulipia ada na gharama nyengine za masomo ya muda mrefu kwa wafanyakazi sita (6) na masomo ya muda mfupi kwa wafanyakazi watatu (3) ndani na nje ya nchi;
viii. Idara imesimamia utekelezaji wa mradi wa *TASAF* Awamu ya Tatu (Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini) na kaya masikini 2,675 kwa Unguja na Kaya 4,084 kwa Pemba zimepatiwa malipo kwa awamu mbili (Januari na Machi 2014). Jumla ya Sh. 432,259,000 zimelipwa kwa Unguja na Pemba. (Kiambatanisho Nam. 3A-3F);
ix. Idara iliandaa semina kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa lengo la kuwapatia uwelewa wajumbe hao kuhusu utekelezaji wa Mradi wa *TASAF* awamu ya Tatu;
x. Idara imeratibu ziara za mafunzo kwa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya zote wa Unguja na Pemba pamoja na Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa waliotembelea eneo la mfano la utekelezaji wa Mradi wa *TASAF* awamu ya Tatu huko Bagamoyo - Tanzania Bara;
xi. Idara imetoa mafunzo maalumu kwa wawezeshaji 120 kutoka Wilaya zote za Unguja na Pemba (Unguja 60 na Pemba 60) wa kuibua kaya masikini;
xii. Idara imeandaa Rasimu ya Kanuni ya Sheria ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo;
xiii. Idara imefuatilia utekelezaji wa miradi ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo kwa Majimbo yote 50 ya Unguja na Pemba. Katika ufuatiliaji huo Kamati za kusimamia miradi hiyo zimehimizwa kufanya marejesho ya utekelezaji wa miradi hiyo;
xiv. Idara imetoa mafunzo kuhusu utekelezaji wa Sheria ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo ya mwaka 2012 kwa Makatibu wa Kamati za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo kwa majimbo yote 18 ya Pemba pamoja na Maafisa Mipango wa Mikoa na Wilaya za Pemba;
xv. Idara inaendelea kukiimarisha Kitengo cha Habari, Mawasiliano na Elimu (*ICE*) kwa kununua vifaa na kutoa mafunzo kwa watendaji wa Kitengo hicho; na
xvi. Tovuti ya Serikali imeimarishwa kwa kuwekwa taarifa mbali mbali za Mawizara na matukio muhimu ikiwemo maadhimisho ya Sherehe mbali mbali za kitaifa na hotuba za Viongozi Wakuu.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015 Idara imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuweka mazingira mazuri ya kazi za Idara kwa ununuzi wa vifaa vya ofisi na samani;
ii. Kuwajengea uwezo wafanyakazi wanne (4) wa Idara kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu pamoja na kulipa stahiki za likizo kwa wafanyakazi saba (7);

iii. Kufuatilia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM na kuandaa Taarifa ya utekelezaji kwa kipindi cha Miaka miwili kuanzia Oktoba 2012 – Septemba 2014;
iv. Kufuatilia utekelezaji wa Ahadi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa kila robo mwaka;
v. Kupokea na kufuatilia malalamiko ya wananchi na kusimamia utatuzi wa migogoro katika jamii;
vi. Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Miradi ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo katika majimbo 50 ya Unguja na Pemba ambayo yamepatiwa fedha;
vii. Kufuatilia mijadala na utekelezaji wa Ahadi za Serikali zinazotolewa katika vikao vya Baraza la Wawakilishi.
viii. Kuratibu vikao saba (7) vya mashirikiano kati ya Wizara za SMZ na SMT;
ix. Kuratibu vikao vinne (4) vya Mawaziri na Makatibu wakuu wa SMZ na SMT na vikao vinne (4) vya Sekretarieti ya Kamati ya Pamoja ya Mambo ya Muungano;
x. Kusimamia utoaji wa fedha *Cash Transfer* kwa Kaya masikini za Unguja na Pemba zinazotolewa kupitia Mpango wa *TASAF* awamu ya Tatu; na
xi. Kuimarisha kitengo cha *ICE* kwa ununuzi wa vifaa vipya na kutoa mafunzo kwa watendaji sita wa Kitengo.

Mhe. Spika**,** Ili Idara iweze kutekeleza majukumu yake kwa mwaka 2014/2015 naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Sh. 344,638,000. Kati ya fedha hizo Sh. 247,053,000 kwa malipo ya mishahara, posho za wafanyakazi na mchango wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii na Sh. 97,585,000 kwa matumizi mengineyo. Kwa upande wa Miradi ya Maendeleo naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya Sh. 1,060,000,000. Kati ya hizo Sh. 1,010,000,000 kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo na Sh. 50,000,000 mchango wa Serikali kwa ajili ya Miradi ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii – *TASAF* awamu ya Tatu.

IDARA YA URATIBU WA SHUGHULI ZA SMZ- DAR ES SALAAM

Mhe. Spika, Idara ya Uratibu wa Shughuli za SMZ Dar es Salaam imehamishiwa rasmi katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais tangu mwezi wa Septemba 2013. Kabla ya hapo Idara hii ilikuwa chini ya Iliyokuwa Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Mhe. Spika, Idara hii inajukumu la kuratibu kazi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar huko Tanzania Bara. Aidha, Idara inaratibu masuala ya SMZ na Ofisi za Balozi mbalimbali zilizopo Tanzania, Wadau wa Maendeleo pamoja na Mashirika ya Kimataifa yenye ofisi zao Dar es Salaam.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Baraza lako Tukufu liliidhinisha jumla ya Sh. 326,970,000 kwa Idara ya Uratibu wa Shughuli za SMZ Dar es Salaam. Hadi kufikia mwezi Machi, 2014 Idara iliingiziwa jumla ya Sh. 119,053,550 kwa kazi za kawaida ambazo ni sawa na asilimia 36.

Mhe. Spika, Idara ya Uratibu wa Shughuli za SMZ - Dar es Salaam katika mwaka wa fedha 2013/2014 imetekeleza kazi zifuatazo:-

i. Idara ilishiriki kwenye Mkutano wa Nane wa Tume ya pamoja ya Ushirikiano wa kiuchumi, kiufundi na Sayansi baina ya Tanzania na India. Ambapo India iliahidi kuipatia msaada SMZ katika kuimarisha huduma za Afya;
ii. Idara ilishiriki katika kikao cha mashauriano baina ya Tanzania na Japan, ambapo Zanzibar iliwasilisha mapendekezo ya miradi saba kupitia Tume ya Mipango Tanzania Bara kwa ajili ya kuombewa misaada kutoka Serikali ya Japan *(TICAD V);*
iii. Idara imeshiriki katika kikao cha wadau kuhusiana na mpango mpya wa ushirikiano baina ya Tanzania na Saudi Arabia, lengo likiwa ni kujenga ushirikiano baina ya nchi hizo mbili;
iv. Idara ilishiriki katika vikao vya maandalizi ya Mkutano wa Wakuu wa nchi za Afrika na Ufaransa, lengo ilikuwa ni kujadili mabadiliko ya tabianchi, ulinzi na usalama pamoja na mashirikiano ya kiuchumi;
v. Idara ilishiriki katika kikao cha wadau kuhusu mpango mpya wa ushirikiano kati ya Tanzania na Uingereza, lengo kuu ni kujadili sera iliyotolewa na Serikali ya Uingereza na kupendekezwa kuundwa kwa ubia wenye ustawi kati yake na Tanzania "Tanzania – *United Kingdom Partnership in Prosperity"* kwenye maeneo ya: Nishati Jadilifu *Renewable enegy*, kilimo na mazingira ya biashara; na
vi. Idara ilishiriki katika matayarisho ya Mkutano Mkuu wa Mawaziri unaojadili masuala ya kiuchumi ambao ulifanyika nchini Kenya.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015 Idara ya Uratibu wa shughuli za SMZ Dar es Salaam imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuweka mazingira mazuri ya kazi za Idara kwa ununuzi wa vifaa vya ofisi na samani;
ii. Kuwajengea uwezo wafanyakazi watatu (3) wa Idara kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu pamoja na kulipa stahiki za likizo kwa wafanyakazi tisa (9);
iii. Kuandaa Muundo mpya wa Kitaasisi na Kiutumishi wa Idara utakaoleta ufanisi zaidi na tija; na
iv. Kuimarisha mashirikiano baina ya Idara na Taasisi za SMZ na Taasisi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano, Ofisi za Kibalozi na Taasisi za Kimataifa.

Mhe. Spika, ili Idara ya Uratibu wa Shughuli za SMZ Dar es Salaam iweze kutekeleza malengo yake katika mwaka wa fedha 2014/2015 naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya Sh. 353,178,160. Kati ya hizo Sh. 208,178,160 kwa ajili ya malipo ya mishahara, posho za wafanyakazi na mchango wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii na Sh. 145,000,000 kwa matumizi mengineyo.

IDARA YA KUKABILIANA NA MAAFA

Mhe. Spika, Idara ya Kukabiliana na Maafa ina jukumu la kuratibu masuala ya maafa hapa Zanzibar, kama ilivyoelezwa katika Sheria ya Kukabiliana na Maafa Nam. 2 ya mwaka 2003.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Baraza lako Tukufu liliidhinisha jumla ya Sh. 262,528,000 kwa Idara ya Kukabiliana na Maafa kwa kazi za kawaida. Hadi kufikia mwezi Machi, 2014 Idara iliingiziwa jumla ya Sh. 112,283,620 kwa kazi za kawaida ambazo ni sawa na asilimia 43. Kwa upande wa miradi ya maendeleo Idara iliidhinishiwa Sh. 340,000,000. Kati ya hizo Sh. 70,000,000 ni mchango wa Serikali na Sh. 270,000,000 ni mchango kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Na hadi kufikia mwezi wa Machi 2014, Idara imeingiziwa Sh.10,000,000 kutoka mchango wa Serikali sawa na asilimia 14 na Sh. 175,176,000 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo sawa na asilimia 65.

Mhe. Spika, Idara ya Kukabiliana na Maafa katika mwaka fedha wa 2013/2014 imetekeleza kazi kama ifuatavyo:-

i. Idara imepatiwa na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) gari moja, redio za mawasiliano 10, pikipiki tatu (3) na kompyuta *(laptop)* nne (4);
ii. Idara imetayarisha na kurusha vipindi 18 vya kukabiliana na maafa kwa lengo la kuelimisha jamii kupitia *ZBC Radio*;
iii. Idara imetoa mafunzo ya kukabiliana na maafa kwa Shehia 36 zilizofanyiwa tathmini ya kujua uwezo wa kukabiliana na maafa katika Wilaya za Magharibi, Mjini na Kaskazini 'A'. Mafunzo hayo ni muendelezo wa mafunzo kwa Wilaya zilizopata fursa ya kutengeneza Mpango wa Dharura wa Kukabiliana na Maafa ambapo wilaya za Micheweni na Wete Pemba tayari zimeshatengeneza Mipango na kupatiwa mafunzo**.** (Kiambatanisho Nam. 4A & 4 B);
iv. Idara imekamilisha Mipango ya Kujiandaa na Kukabiliana na Maafa kwa Wilaya za Mjini, Magharibi na Kaskazini 'A'. Mipango kama hii imeshakamilika kwa Wilaya za Wete na Micheweni Pemba;
v. Idara imetoa huduma ya operesheni za uokozi kwa abiria waliopata ajali ya kudondoka katika meli ya MV. Kilimanjaro II iliyotokea katika bahari ya Nungwi tarehe 5 Januari, 2014;
vi. Idara imeendesha makongamano mawili (2) ya kukabiliana na maafa kwa wadau wa maafa nchini;
vii. Idara imeandaa Mwongozo wa Mafunzo kwa Wafanyakazi wa Idara ya Kukabiliana na Maafa pamoja na Mkakati wa Kutafuta Nyenzo za Kukabiliana na Maafa wa Zanzibar;
viii. Idara imetoa elimu ya kukabiliana na maafa kwa watu wenye ulemavu 100 na wanafunzi wa skuli za msingi na Sekondari (1,200) katika Wilaya za Mjini na Kaskazini 'A' Unguja na Chakechake na Mkoani Pemba;
ix. Idara imefanya mikutano miwili (2) Unguja na Pemba ya kuelimisha wadau juu ya Mwongozo wa Kukabiliana na Maafa Zanzibar pamoja na Mwongozo wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Sera ya Kukabiliana na Maafa ya Zanzibar; na

x. Idara imelipia gharama za mafunzo ya muda mrefu (Shahada ya Pili) kwa wafanyakazi watatu (3) wa Idara. Wafanyakazi hawa wote wanasomea kada ya kukabiliana na maafa.

Mhe. Spika, katika mwaka 2014/2015, Idara imepanga kutekeleza malengo yafuatayo: -

i. Kuweka mazingira mazuri ya kazi za Idara kwa ununuzi wa vifaa vya ofisi na samani;
ii. Idara kwa kushirikiana na Washirikia wa Maendeleo (*USAFRICOM,* Benki ya Dunia na Kamisheni ya Bahari ya Hindi) itaendesha mafunzo mbalimbali ya kukabiliana na maafa kwa watendaji na wadau wa kukabiliana na maafa pamoja na kuendesha mazoezi mawili (2) ya kukabiliana na maafa;
iii. Kuwajengea uwezo wafanyakazi wanne (4) wa Idara kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu pamoja na kulipa stahiki za likizo kwa wafanyakazi sita (6);
iv. Kuyafanyia matengenezo maghala mawili (2) na kununua vifaa vya kukabiliana na maafa kwa Unguja na Pemba;
v. Kujenga uwezo kwa jamii katika kukabiliana na majanga na maafa kwa Shehia 10; na
vi. Kukamilisha sheria mpya ya kukabiliana na maafa.

Mhe. Spika, ili Idara ya Kukabiliana na Maafa iweze kutekeleza malengo yake katika mwaka wa fedha 2014/2015, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya Sh. 298,447,800 kwa matumizi ya Idara. Kati ya hizo Sh. 128,875,500 kwa ajili ya malipo ya mishahara, posho za wafanyakazi na mchango wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii na Sh. 169,572,300 kwa matumizi mengineyo. Aidha, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya Sh. 1,322,880,000 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, Sh. 40,000,000 ikiwa ni mchango wa Serikali na Sh. 1,282,880,000 ni mchango kutoka washirika wa Maendeleo.

IDARA YA SHEREHE NA MAADHIMISHO YA KITAIFA

Mhe. Spika, Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa ina jukumu la kuratibu Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa pamoja na shughuli za kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa. Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa yanayoratibiwa na Idara ni Sherehe za Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar, Sherehe za Muungano wa Tanganyika na Zanzibar pamoja na ushiriki wa Viongozi na wananchi wa Zanzibar katika Sherehe za Uhuru wa Tanganyika.

Aidha, kwa upande wa shughuli za kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa, Idara inaratibu mazishi ya Viongozi kama ilivyoainishwa kwenye Sheria ya Kuwaenzi Viongozi Nam. 10 ya Mwaka 2002, Hitma na Dua ya Marehemu Sheikh Abeid Amani Karume pamoja na kutunza kumbukumbu za viongozi hao.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Baraza lako Tukufu liliidhinisha jumla ya Sh. 2,189,103,000 kwa Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa. Hadi kufikia mwezi Machi, 2014 Idara iliingiziwa jumla ya Sh. 2,480,329,652 kwa kazi za kawaida ambazo ni sawa na asilimia 113.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2013/2014, Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa imetekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuratibu kwa mafanikio makubwa maadhimisho ya Sherehe za Miaka 50 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ambazo zilikuwa za kipekee na za aina yake zilizofikia kilele tarehe 12 Januari, 2014;
ii. Idara imeratibu kwa mafanikio makubwa Sherehe za Miaka 50 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar zilizofanyika katika uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam tarehe 26 Aprili, 2014. Aidha, Idara imeratibu ushiriki wa viongozi na wananchi wa Zanzibar katika Sherehe za miaka 52 ya Uhuru wa Tanganyika zilizofanyika tarehe 09 Disemba, 2013. Kazi hii imefanywa kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu;
iii. Idara imeratibu Hitma na Dua ya Marehemu Sheikh Abeid Amani Karume iliyofanyika Afisi Kuu ya CCM, Kisiwandui tarehe 7 Aprili, 2014;
iv. Idara imeendelea kukusanya taarifa na kumbukumbu za Marehemu Sheikh Abeid Amani Karume;

v. Idara imenunua vifaa vya sherehe ikiwemo zulia jekundu na bendera pamoja na kuendelea kulifanyia matengenezo Ghala la Idara lililopo Mwanakwerekwe Unguja.; na
vi. Idara imewapatia mafunzo ya muda mrefu wafanyakazi wawili (2) wa Idara pamoja na kulipia stahiki za wafanyakazi wawili (2) waliokwenda likizo.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuweka mazingira mazuri ya kazi za idara kwa ununuzi wa vifaa vya ofisi na samani.
ii. Kuwajengea uwezo wafanyakazi wawili (2) wa idara kwa kutoa mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu pamoja na kulipa stahiki za likizo kwa wafanyakazi wawili (2);
iii. Kuratibu na kusimamia sherehe za Miaka 51 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar;
iv. Kuratibu sherehe za Miaka 51 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar na ushiriki wa viongozi na wananchi wa Zanzibar katika Sherehe za miaka 53 ya Uhuru wa Tanganyika kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu;
v. Kuratibu Hitma na Dua ya Marehemu Sheikh Abeid Amani Karume (Siku ya Mashujaa);
vi. Kuifanyia mapitio Sheria Nam. 10 ya 2002 ya Kuwaenzi Viongozi pamoja na mambo yanayohusiana nayo; na
vii. Kuendelea kukusanya na kutunza kumbukumbu za Marehemu Sheikh Abeid Amani Karume.

Mhe. Spika, ili Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa iweze kutekeleza malengo yake iliyojipangia kwa mwaka wa fedha 2014/2015, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya Sh. 871,615,500 kwa matumizi ya Idara. Kati ya hizo Sh. 87,259,800 kwa malipo ya mishahara, posho za wafanyakazi na mchango wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii na Sh. 784,355,700 ni kwa matumizi mengineyo.

IDARA YA UPIGAJI CHAPA NA MPIGA CHAPA MKUU WA SERIKALI

Mhe. Spika, Idara ya Upigaji Chapa na Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali ina majukumu ya kuchapisha Miswada ya Sheria, Gazeti Rasmi la Serikali, risiti, hotuba za bajeti na nyaraka zote za Serikali pamoja na kuuza vifaa vya kuandikia kwa Taasisi zote za Serikali na watu binafsi. Vile vile, Idara ina jukumu kuu la kuchapisha na kuhifadhi nyaraka za siri za Serikali.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Baraza lako Tukufu liliidhinisha jumla ya Sh. 546,868,000 kwa Idara ya Upigaji Chapa na Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali. Hadi kufikia mwezi Machi, 2014 Idara iliingiziwa jumla ya Sh. 288,754,082 kwa kazi za kawaida ambazo ni sawa na asilimia 53. Aidha, Idara iliidhinishiwa jumla ya Sh. 2,500,000,000 kwa kazi za maendeleo ikiwa ni mchango wa SMZ na hadi kufikia mwezi Machi, 2014 Idara iliingiziwa jumla ya Sh. 2,050,000,000 sawa na asilimia 82.

Mhe. Spika, Idara ilipangiwa kuchangia jumla ya Sh.500,000,000 kwa mwaka wa fedha 2013/2014 katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2014, Idara imechangia Sh. 14,623,400 sawa na asilimia 4. Mchango huu mdogo umetokana na kiwanda kupunguza uzalishaji kutokana na kuharibika kwa mashine pamoja na kuanza kwa zoezi la kuhamisha mashine na kufunga mashine mpya. Aidha, Idara inazidai baadhi ya taasisi za Serikali jumla sh. 42,480,000 za mapato ambazo ni sehemu ya mapato yanayotarajiwa kukusanywa katika kipindi cha Julai 2013 - Machi 2014.

Mhe. Spika, Idara kwa mwaka wa fedha 2013/2014 imeweza kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Jumla ya wafanyakazi saba (7) wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu na mfupi katika ngazi za cheti, diploma na shahada ya pili;
ii. Idara inaendelea kutoa huduma ya machapisho mbali mbali zikiwemo kazi za uchapishaji wa sheria, Gazeti Rasmi la Serikali, Katiba, madaftari ya mishahara, kalenda, na kazi nyengine za taasisi za umma na binafsi;
iii. Idara imekamilisha matengenezo ya jengo jipya la kiwanda cha uchapishaji huko Maruhubi na tayari jengo hilo limeanza kutumika'
iv. Idara imechapisha miswada ya sheria 11 na matoleo 1,400 ya Gazeti Rasmi la Serikali; na

v. Idara imenunua pamoja na kufunga kwa awamu ya kwanza mashine mpya nne (4) za aina ya dijitali.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Idara ya Upigaji Chapa na Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali imejipangia malengo yafuatayo:-

i. Kuweka mazingira mazuri ya kazi za Idara kwa ununuzi wa vifaa vya ofisi na samani;
ii. Kuwajengea uwezo wafanyakazi watano (5) wa Idara kwa kutoa mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu pamoja na kulipa stahiki za likizo kwa wafanyakazi saba (7);
iii. Kutoa huduma za uchapishaji wa nyaraka na Sheria za Serikali;
iv. Kutangaza huduma za kiwanda kwa ajili ya kuongeza idadi ya wateja na mapato; na
v. Kukamilisha utaratibu wa kuanzisha Bohari Kuu ya Serikali ya Vifaa vya Ofisi.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Idara ya Upigaji Chapa na Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali imekadiriwa kutumia jumla ya Sh. 482,066,600. Kati ya hizo Sh. 347,066,600 kwa matumizi ya mishahara ya wafanyakazi, michango ya *ZSSF* na Sh. 135,000,000 kwa matumizi mengineyo.

Mhe. Spika, kwa upande wa mapato Idara imepangiwa kukusanya Sh. 600,000,000 kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

OFISI KUU PEMBA

Mhe. Spika, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Pemba ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa kazi za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa upande wa Pemba.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Baraza lako Tukufu liliidhinisha jumla ya Sh. 452,817,000 kwa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Pemba. Hadi kufikia mwezi Machi, 2014 Idara iliingiziwa jumla ya Sh. 254,014,050 kwa kazi za kawaida ambazo ni sawa na asilimia 56.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014 Ofisi Kuu Pemba ilikuwa na lengo la kusimamia shughuli za Idara zilizo chini ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Kisiwani Pemba na imetekeleza kazi zifuatazo:-

i. Ofisi iliratibu na kufuatilia utekelezaji wa ziara 23 za Viongozi Wakuu wa Kitaifa;
ii. Ofisi ilifanya Semina ya siku moja (1) kwa Maafisa Mipango wa Mawizara, Mikoa na Wilaya juu ya uandishi wa taarifa ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala (CCM);
iii. Ofisi iliratibu na ilisimamia utekelezaji wa miradi ya *TASAF* Pemba;
iv. Ofisi iliendelea kutoa mafunzo, kusimamia na kuratibu shughuli za kukabiliana na maafa; na
v. Ofisi iliwapatia mafunzo wafanyakazi wanane (8) katika kada mbali mbali.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015 Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Pemba itatekeleza malengo ya idara na taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais.

Mhe. Spika, ili Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Pemba iweze kutekeleza malengo yake iliyopanga naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Sh. 388,964,000 kwa matumizi ya Ofisi. Kati ya hizo Sh. 241,266,000 ni kwa malipo ya mishahara na posho za wafanyakazi na mchango wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, na Sh. 147,698,000 ni kwa matumizi mengineyo.

TUME YA UCHAGUZI YA ZANZIBAR

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Baraza lako tukufu liliidhinisha jumla ya. Sh. 987,000,000 kwa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar. Hadi kufikia mwezi Machi, 2014 Tume iliingiziwa jumla ya Sh. 827,303,454 kwa kazi za kawaida ambazo ni sawa na asilimia 84. Aidha, Tume iliidhinishiwa Sh. 3,594,000,000 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na hadi kufikia mwezi Machi, 2014 Tume ya Uchaguzi iliingiziwa jumla ya Sh. 768,165,455 sawa na asilimia 21.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Tume ya Uchaguzi imetekeleza malengo yafuatayo:-

i. Katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar iliendesha chaguzi ndogo mbili. Chaguzi hizo ni Uchaguzi Mdogo wa Jimbo la Kiembesamaki Wilaya ya Magharibi kujaza nafasi iliyoachwa wazi na Ndugu Mansoor Yussuf Himidi aliyekuwa Mwakilishi wa Jimbo hilo na Uchaguzi Mdogo wa Wadi ya Kiboje Wilaya ya Kati iliyoachwa wazi kufuatia kifo cha Diwani wa Wadi hiyo Ndugu Mayunga Maftah Mayunga. Chaguzi zote mbili ziliendeshwa kwa usalama na utulivu mkubwa;
ii. Tume imetoa elimu ya Wapiga Kura kupitia vyombo mbali mbali vya habari vya Redio na Televisheni, semina za Wanafunzi wa Skuli za Sekondari na kupitia vikundi vya Sanaa za Maonesho kwa Unguja na Pemba. Aidha, imeendelea kutoa elimu ya uandikishaji wa Wapiga Kura katika Shehia mbalimbali ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015; na
iii. Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar imeanza maandalizi ya awali ya kuchunguza idadi, majina na mipaka ya Majimbo ya Uchaguzi kwa kuwapatia Wajumbe wa Tume ya Uchaguzi na Watendaji wake mafunzo kuhusu uchunguzi wa majimbo. Mafunzo hayo yamefanyika kwa awamu mbili ambapo awamu ya kwanza iliwahusisha Maafisa Uchaguzi wa Wilaya za Unguja na Pemba, na awamu ya pili iliwahusisha Wajumbe wa Tume na Sekretarieti.
iv. Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar imeendesha kazi za uandikishaji wa Wapiga Kura wapya na uendelezaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga kura. Kazi hiyo ilianza katika mwezi wa Juni, 2013 Mkoa wa Kaskazini Unguja na ilimalizika katika mwezi wa Novemba 2013, Mkoa wa Kusini Pemba. Zoezi hilo lilifanyika kwa kuwaandikisha wananchi wote waliojitokeza ambao wana sifa za kupiga kura kwa Uchaguzi Mkuu wa Zanzibar. Jumla ya wananchi 41,261 waliandikishwa. (Kiambatanisho Nam. 5).

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuweka mazingira mazuri ya kazi za Tume kwa ununuzi wa vifaa vya ofisi na samani;
ii. Kuwajengea uwezo wafanyakazi watatu (3) kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na wafanyakazi (15) mafunzo ya muda mfupi pamoja na kulipa stahiki za likizo kwa wafanyakazi sita (6);
iii. Kuendeleza Daftari la Kudumu la Wapiga Kura;
iv. Kufanya uchunguzi wa idadi, majina na mipaka kwa majimbo yote 50 ya uchaguzi;
v. Kusimamia na kuendesha Kura ya Maoni ya kuthibitisha Katiba Mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliyopendekezwa; na
vi. Kufanya matayarisho ya jumla ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015.

Mhe. Spika, ili Tume ya Uchaguzi iweze kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2014/2015, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Sh. 1,314,100,000 kwa matumizi ya kawaida. Kati ya hizo Sh. 971,500,000 ni kwa malipo ya mishahara, posho na stahiki za wafanyakazi na Sh. 342,600,000 kwa matumizi mengineyo. Aidha, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya Sh. 1,750,000,000 kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za maendeleo kupitia mchango wa Washirika wa Maendeleo.

Mhe. Spika, Tume ya Uchaguzi kupitia Mfuko Mkuu wa Serikali imepangiwa kutumia jumla ya Sh. 3,000,000,000 kwa ajili ya maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015, kufanya uchunguzi wa idadi, majina na mipaka ya majimbo ya uchaguzi pamoja na kuendeleza Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

BARAZA LA WAWAKILISHI

Mhe. Spika, Baraza la Wawakilishi Zanzibar limeundwa chini ya Kifungu cha 63 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 na majukumu ya msingi yanatajwa kwenye kifungu cha 88 cha Katiba ambayo ni kama yafuatayo:-

i. Kutunga Sheria pale ambapo utekelezaji wa jambo unahitaji kuwepo kwa sheria hiyo;
ii. Kujadili shughuli za kila Wizara wakati wa kikao cha mwaka wa Bajeti katika Baraza la Wawakilishi;

iii. Kuuliza maswali mbalimbali kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika Baraza la Wawakililshi; na
iv. Kuidhinisha na kusimamia Mipango ya Maendeleo ya Serikali katika njia ile ile ambayo Bajeti ya mwaka inaidhinishwa.

Mhe. Spika, katika kutekeleza majukumu hayo kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014 Ofisi ya Baraza la Wawakilishi iliidhinishiwa jumla ya Sh. 14,852,000,000. Hadi kufikia mwezi wa Machi 2014 Baraza limeingiziwa Sh. 10,501,979,561 kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 71. Kwa upande wa fedha za Miradi ya Maendeleo Baraza la Wawakilishi liliidhinishiwa jumla ya Sh. 697,536,000 na hadi kufikia mwezi Machi 2014 Baraza limeiingiziwa Sh. 544,658,000 Sawa na asilimia 78.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Baraza la Wawakilishi limetekeleza kazi zifuatazo:-

i. Baraza limefanya Mikutano minne ya kawaida ambapo kwenye Mikutano hiyo jumla ya Miswada kumi (10) ya Sheria ilijadiliwa na kupitishwa na maswali 250 yameulizwa na kujibiwa. Mgawanyo wa Miswada na Maswali hayo ni kama ifuatavyo.

Mkutano wa Kumi na mbili wa Bajeti ya mwaka wa fedha wa 2013/2014 ulikuwa na Miswada miwili ya Sheria na jumla ya Maswali 75 ya msingi yaliulizwa na kujibiwa.

Mkutano wa Kumi na Tatu uliofanyika mwezi wa Oktoba, 2013 ulipitisha Miswada minne ya Sheria na jumla ya maswali 71 ya msingi yaliulizwa na kupatiwa majibu.

Mkutano wa Kumi na Nne uliofanyika mwezi wa Disemba 2013 ulipitisha Miswada Mitatu ya Sheria wakati jumla ya maswali 61 ya msingi yaliulizwa na kujibiwa. Aidha, kwenye Mkutano huo Baraza lilipokea na kuijadili Ripoti ya Kamati Teule ya Kuchunguza Migogoro ya Ardhi. Pia, kulikuwa na Hoja mbili za Wajumbe. Moja ni Hoja ya Mjumbe kuomba Ridhaa ya Baraza kwa ajili ya kuwasilisha Mswada wa Sheria ya Utawala wa Baraza, iliyowasilishwa na Mhe. Hamza Hassan Juma na Pili ni Hoja ya Mjumbe ya kuliomba Baraza kutoa Azimio Dhidi ya Vitendo vya Udhalilishaji wa Watoto, Zanzibar. Hoja ambayo iliwasilishwa kwenye Baraza na Mhe. Mgeni Hassan Juma

Mkutano wa Kumi na Tano uliofanyika mwezi wa Februari, 2014 nao ulipitisha Miswada miwili ya Sheria na jumla ya maswali 50 yaliulizwa na kujibiwa. Wakati huo huo, Baraza lilipokea Taarifa za Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati za Baraza yaliyotolewa mwaka 2012/2013 na Kamati za Kudumu za Baraza ziliwasilisha Ripoti za Kazi kwa mwaka 2013/2014. Katika Mkutano huo pamoja na mambo mengine yaliyojadiliwa na kufikiwa maamuzi, Baraza liliunda Kamati Teule ya Kuchunguza Upotevu wa Nyaraka za Serikali katika Jengo la Nyaraka na Makumbusho. Kamati hiyo iliundwa ikiwa na Wajumbe watano. Hili liliibuka wakati wa kuwasilisha Ripoti za Kamati na lilitokana na Ripoti ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. (Kiambatanisho Nam. 6)

ii. Kamati za Kudumu za Baraza zilifanya kazi zake za Kawaida za kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Serikali kupitia Wizara na Idara mbali mbali za Serikali. Aidha, Kamati Teule ya Baraza iliyopewa kazi ya kuchunguza Migogoro ya Ardhi nayo ilimaliza kazi yake na kuwasilisha Ripoti yake kwenye Baraza;
iii. Ofisi imewapatia mafunzo Wafanyakazi 16 katika fani za Sheria, Uchumi, Uhusiano wa Kimataifa, Utawala wa Biashara, Utawala wa Raslimali Watu, Ufundi, Teknolojia, Ununuzi na Ugavi, Ukutubi na Elimu, hii ni kwenye ngazi za Vyeti, Stashahada, Shahada, Shahada ya Uzamili na Shahada ya Uzamivu;
iv. Baraza limeshiriki katika Mkutano wa Jumuiya ya Makatibu Mezani *(SOCAT*) Dar-es-Salaam kwa lengo la kuendeleza uhusiano wa Kimataifa wa kikanda baina ya Baraza na vyombo vyengine vya Kutunga Sheria na Umoja wa Mabunge ya Jumuiya ya Madola;
v. Ofisi ya Baraza la Wawakilishi bado inaendeleza vipindi vyake vya kutoa elimu kwa Umma kupitia Shirika la Utangazaji la Zanzibar (ZBC) kwa upande wa Redio na Televisheni. Kwa kipindi cha mwaka 2013/2014 jumla ya vipindi 24 vya LIJUE BARAZA LA WAWAKILISHI vilirushwa hewani;

vi. Ofisi imefanya matengenezo makubwa ya majengo kwa Ofisi za Baraza Unguja na Pemba hasa yanayohusu miundombinu ya maji, tatizo ambalo sasa limepungua kwa kiasi kikubwa. Aidha, katika kupunguza matumizi ya umeme hasa kwa kuendesha vipoza hewa muda wote, mfumo wa muundo wa madirisha nao umeanza kubadilishwa ambapo badala ya kuwa na madirisha yasiyofunguka, sasa yamewekwa yale yanayofunguka; na
vii. Ofisi imefanya tathmini ya athari zinazotokana na nyufa ili kuweza kutafuta ufumbuzi wa kuziba nyufa hizo.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Baraza la Wawakilishi limepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kujenga Mazingira mazuri kwa kuwezesha kufanyika kwa Mikutano minne (4) ya Baraza la Wawakilishi pamoja na kazi za Kamati katika kufuatilia Shughuli za Serikali na Kusimamia uwajibikaji wake;
ii. Kutoa mafunzo ya kuongeza uwezo wa kitaalamu kwa Wajumbe na Wafanyakazi wa Baraza
iii. Kuweka majengo yote ya Ofisi katika hali nzuri;
iv. Kutoa taaluma kwa wananchi kuhusu utendaji wa Shughuli za Baraza kupitia vyombo vya Habari; na
v. Kuimarisha mahusiano kati ya Baraza na Mabunge mengine ya Umoja wa Mabunge ya Jumuiya ya Madola.

Mhe. Spika, ili Ofisi ya Baraza la Wawakilishi iweze kutekeleza malengo yake kwa mwaka wa fedha 2014/2015, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Sh. 14,564,000,000 kwa matumizi ya Ofisi. Kati ya hizo Sh. 7,664,000,000 ni kwa malipo ya mishahara, posho za wafanyakazi, Stahiki nyengine na mchango wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii na jumla ya Sh. 6,900,000,000 kwa matumizi mengineyo. Kwa upande wa fedha za maendeleo naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Sh. 710,615,000 ikiwa ni mchango wa Washirika wa Maendeleo.

UKUSANYAJI MAPATO

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ilipanga kukusanya mapato ya jumla ya Sh. 544,400,000 kwa mchanganuo ufuatao:-

i. Idara ya Upigaji Chapa na Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali Sh. 500,000,000
ii. Idara ya Uendeshaji na Utumishi (Kodi ya Ukumbi wa Mikutano wa BLW wa zamani Sh. 38,000,000
iii. Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa(Kodi ya milango ya duka na mashamiana) Sh. 6,000,000

Jumla Sh. 544,000,000

Mhe. Spika, hadi kufikia mwezi Machi 2014 ukusanyaji halisi wa mapato ulikua ni jumla ya Sh. 16,519,200 Sawa na asilimia 4 kama ifuatavyo:-

i. Idara ya Upigaji Chapa na Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali Sh. 14,899,200
ii. Idara ya Uendeshaji na Utumishi (Kodi ya Ukumbi wa Mikutano wa BLW wa zamani)
iii. Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa (Kodi ya Milango ya duka na mashamiana) Sh.1,620,000

Jumla Sh. 16,519,200

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais imepanga kukusanya mapato ya jumla ya Sh. 608,000,000 kwa mchanganuo ufuatao:-

i. Idara ya Upigaji Chapa na Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali Sh. 600,000,000
ii. Idara ya Uendeshaji na Utumishi (Kodi ya Ukumbi wa Mikutano wa BLW wa zamani) Sh. 5,000,000
iii. Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa (Kodi ya mashamiana) Sh. 3,000,000

	Jumla	Sh. 608,000,000

Mhe. Spika, muhtasari wa makadirio ya fedha kwa kazi za kawaida na za Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2014/2015 ni kama unavyoonekana katika (Kiambatanisho Nam. 7A na 7B).

HITIMISHO

Mhe. Spika, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru kwa dhati Mhe. Mohamed Aboud Mohamed, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kunisaidia kutekeleza majukumu ya Ofisi yangu kwa ufanisi mkubwa. Aidha, nawashukuru kwa dhati watendaji wote wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wakiongozwa na Katibu Mkuu, Dkt. Khalid Salum Mohamed kwa juhudi zao katika kutekeleza majukumu yao.

Mhe. Spika, natoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi na shukurani za pekee kwa Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mashirikiano, maelekezo, ushauri na michango wanayotupa ambayo ilisaidia katika utayarishaji wa hotuba hii.

Aidha, napenda kuwashukuru sana Washirika wa Maendeleo (*Development Partners*) na nchi marafiki ambazo zinaendelea kuchangia katika kufanikisha utekelezaji wa malengo ya Ofisi yetu na ya nchi kwa jumla katika mwaka wa fedha 2013/2014. Miongoni mwao ni: *AL-Youssef Foundation*, Benki ya Dunia, *Clinton Foundation*, China, *FAO*, Finland, Norway, Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, India, Japan, Marekani, Mfuko wa Dunia wa Kupambana na Kifua Kikuu, Malaria na UKIMWI (*Global Fund*), Oman, *UNAIDS, USAID, UNDP, UNICEF, UNFPA, WHO, WFP* na *WIPO*.

Vile vile, naishukuru sana Ofisi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Ofisi ya Waziri Mkuu kwa ushirikiano wao wa karibu sana na Ofisi yetu. Pia nazishukuru Taasisi zisizo za Kiserikali kama ZAYEDESA, Jumuiya ya Wafanyabiashara, Wenye Viwanda na Wakulima kwa kuendelea kuisaidia Serikali katika kutoa huduma za jamii na kuiletea maendeleo nchi yetu. Pia, nawashukuru wananchi wote ambao wamefuatilia na kusikiliza Hotuba yetu hii.

Mhe. Spika, Baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe Jumla ya Sh. 19,988,300,000 kwa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Taasisi zake (Tume ya Uchaguzi na Baraza la Wawakilishi) kwa matumizi ya kazi za kawaida na Sh. 6,343,495,000 kwa kazi za maendeleo (Kiambatanisho Nam. 7A na 7B). Mchanganuo halisi wa fedha hizo ni kama ifuatavyo:-

	Kazi za Kawaida	
i	Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais	Sh. 4,110,200,000
ii	Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar	Sh. 1,314,100,000
iii	Ofisi ya Baraza la Wawakilishi	Sh. 14,564,000,000
	Jumla Kuu	Sh. 19,988,300,000
	Kazi za Maendeleo	
i	Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais	
a	Kujenga Uwezo wa Kukabiliana na Maafa	Sh. 1,322,880,000
b	Mradi wa *TASAF III*	Sh. 1,550,000,000
c	Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo (*CDF*)	Sh. 1,010,000,000
	Jumla Ndogo (OMPR)	Sh. 3,882,880,000
ii	Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar	
	Mradi wa kuwezesha Demokrasia (*DEP*)	Sh. 1,750,000,000
iii	Ofisi ya Baraza la Wawakilishi	
	Mradi wa Kuwezesha BLW (*LSP*)	Sh. 710,615,000

Jumla Kuu (Miradi) Sh. 6,343,495,000

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa hotuba hiyo uliyoiwasilisha punde, Mawaziri wengine watafuata mfano wako, umetumia muda wa saa moja na dakika tano tu. Kwa hivyo ninakushukuru sana kuendana na muda ambao tumejipangia.

Hoja imeungwa mkono na sasa ipo tayari kuanza kujadiliwa. Ninamuona Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, karibu.

Mhe. Hamza Hassan Juma (Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa): Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena, kama kawaida yako ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya mwanzo kuanza kuchangia na kutoa maoni ya Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015 kwa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar.

Mhe. Spika, nitaomba radhi kidogo kwa sababu kwa kweli nilichelewa sana kukipata hiki kitabu, na kwa kuwa ratiba ya wizara hii ilikuwa iwe kesho. Kwa hivyo kutokana na shughuli zetu zinavyokwenda imebidi nimepata muda kidogo ulikuwa mgumu lakini nimejitahidi kwa kadri iwezekanavyo. Kwa hivyo, kuna baadhi ya maeneo ambayo katika hotuba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais yatakuwa yamejitokeza lakini katika ripoti ambayo nitakayoisoma yatakuwa hayakujitokeza, lakini nitaomba vile vile maeneo hayo kwa kuwa ni muhimu basi nitaomba utaniruhusu nitayazungumza kama ni mchango wangu wa kawaida.

Mhe. Spika, baada ya hayo sasa naomba moja kwa moja nianze kuingia katika hotuba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais. Mhe. Spika, kama nilivyokwisha kutoa shukurani zangu kwako, vile vile kwa niaba ya Wajumbe wa kamati yangu naomba nichukue nafasi hii kusimama mbele ya Baraza lako tukufu ili niweze kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa.

Mhe. Spika, vile vile ninapenda kutumia nafasi hii kumshukuru Mhe. Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar kwa kazi kubwa ambayo ameifanya; ya kusimamia utekelezaji wa shughuli za serikali, lakini vile vile kuweza kusimamia majukumu ya wizara yake.

Mhe. Spika, pia tunamshukuru Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais pamoja na timu yake, kuanzia Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi mpaka wafagiaji kwa kazi kubwa ambayo wanayoifanya lakini vile vile kwa mashirikiano wanayotupa wakati wote tunapokuwa katika kusimamia utendaji wa wizara yao.

Mhe. Spika, vile vile kamati yangu katika kuisimamia wizara hii. Aidha ninapenda kuchukua fursa hii pia kuwashukuru Wajumbe wa kamati yangu kwa michango yao ya kina waliyoitoa wakati kamati yetu ilipokuwa inajadili makadirio na matumizi ya fedha ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mhe. Spika, kwa hivyo kwa ruhusa yako nitaomba tu basi niwataje Wajumbe wa kamati yangu ambao tumeshirikiana kwa kipindi chote cha mwaka mzima kusaidiana au kusimamia Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kutekeleza majukumu yake. Naomba kwanza nianze na:-

1. Mhe. Hamza Hassan Juma -Mwenyekiti
2. Mhe. Saleh Nassor Juma -Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Ali Mzee Ali -Mjumbe
4. Mhe. Subeit Khamis Faki -Mjumbe
5. Mhe. Shadya Mohammed Suleiman -Mjumbe
6. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk -Mjumbe

7. Mhe. Ashura Sharif Ali -Mjumbe
8. Ndg. Rahma Kombo Mgeni -Katibu
9. Ndg. Makame Salim Ali -Katibu

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo, sasa naomba kutoa maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa bajeti hii ya 2014/2015 ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

IDARA YA MAAFA

Mhe. Spika, hii ni idara muhimu sana katika Ofisi ya Makamu wa Pili Rais ambayo licha ya ufinyu wa bajeti tulionao lakini kwa kweli wanafanya kazi kubwa sana na inapaswa kuangaliwa sana ili kuhakikisha kwamba idara hii inakuwa na uwezo wa kutosha katika kutekeleza majukumu yake ya kukabiliana na maafa.

Mhe Spika, ukizingatia kwa dunia hii ya leo ambayo imeathiriwa sana na mabadiliko ya tabia nchi, na kwa kuzingatia kuwa Zanzibar ni nchi ya visiwa, kwa hiyo iko haja ya Serikali yetu kuweza kujiandaa wakati wote kukabiliana na hali yoyote itakayojitokeza ya maafa aidha ya Baharini, angani au nchi kavu, kwa hiyo ndio maana bado Kamati yangu inaitaka Serikali kama tunavyoshauri siku zote kutekeleza ile sheria ya 2003 kwa kuanzisha Mfuko wa Maafa ambao ndio itakuwa uhakika wa idara hii kuweza kukabiliana na maafa wakati wowote yatakapotokea, na sio kutegemea *OC;* kwani hivi sasa muda mwingi idara inakuwa kavu hawana hata akiba ya kudhibiti jambo lolote linapotokezea kwani kazi ya Idara hii sio tu kukabiliana na maafa, bali pia kuzuia maafa yasitokee pahala popote hasa kwa kuweza kutoa elimu. Kwa hiyo Serikali tunaiomba kuharakisha suala hili la kuundwa mfuko huu wa maafa.

Mhe. Spika, kamati yetu pia ilitembelea ghala ya Idara ya maafa iliyopo Saateni Zanzibar, lakini kamati ilisikitishwa sana kwanza hali ya jengo tuliyoikuta hairidhishi na pia katika ghala hamna vifaa vya kutosha kwa ajili ya kukabiliana na maafa. Aidha kamati ilipatiwa maelezo kuwa vifaa vyote vilivyokuwemo katika ghala ni vifaa vinavyotumika baada ya maafa lakini katika ghala hamna vifaa vinavyotumika kabla ya maafa na wakati wa maafa. Taarifa hii iliisikitisha sana Kamati yangu na kuona kwamba hivi sasa ipo haja kwa Serikali kuelekeza nguvu zake zote katika Idara hii ili kuweza kukabiliana na maafa wakati wowote na mahala popote yanapotokea. Suala la vifaa katika Idara hii ni muhimu sana kama ilivyo wa jina lake la maafa.

Mhe Spika, kamati yangu pia inaitaka Serikali kuhakikisha Idara hii inapatiwa jengo lake la kudumu ili kuweza kufanya kazi zake kwa ufanisi na pia kuwa na ghala lake lenyewe, kwani kwa hivi sasa hata wakimpata muhisani yeyote kuwasaidia lakini pa kuweka vifaa vya kutosha hawana eneo hilo

Mhe. Spika, suala la mawasiliano ya uharaka wakati yanapotokea maafa ni jambo muhimu sana, hivyo basi kamati inasisitiza kuwa Idara hii ipatiwe vifaa vya mawasiliano vya kisasa ili kuweza kupata taarifa mapema yanapotokea maafa ili waweze kuchukua hatua za uharaka pindi yanapotokea maafa hayo.

Mhe. Spika, kwa ujumla uingizwaji wa fedha kama ulivyo katika idara na taasisi nyengine za Serikali umekuwa ni tatizo kubwa, kwa hivyo kamati yangu itaendelea kusisitiza kuwa Serikali iharakishe uundwaji wa Mfuko wa Maafa kama tulivyopitisha kwenye sheria ya mwaka 2003 kwani suala hilo limetajwa kwenye sheria hiyo bado kilichokosekana mpaka sasa hivi ni utekelezaji tu.

IDARA YA SHEREHE NA MAADHIMISHO YA KITAIFA

Mhe, Spika, kwanza kamati yetu inatoa pongezi za kipekee kwa Rais wetu Mhe. Dr. Ali Muhammed Shein kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais pamoja na Wizara na taasisi nyengine kwa kufanya sherehe kubwa na za kipekee za miaka 50 ya Mapinduzi matukufu ya Zanzibar, jambo ambalo limeonesha heshima kubwa kwa Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na kumuenzi muasisi wa Mapinduzi yetu, Mzee Abeid Amani Karume; Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema peponi Amin.

Mhe, Spika, pili kamati yetu inaipongeza sana serikali kwa maamuzi mazuri ya kujenga mnara wa kumbukumbu ya maadhimisho ya miaka 50 ya Mapinduzi matukufu ya Zanzibar, ambao utakuwa ni kielelezo na kivutio kikubwa kwa watu wanaoishi ndani ya Zanzibar na pia wale wageni wanaotoka nje ya Zanzibar. Tunaiomba serikali yetu kuutumia vizuri mnara huo kwa kuweka kumbukumbu zote za Mapinduzi yetu ili kuweka ukumbusho kwa vizazi

vyetu vijavyo, kwani na wao miaka 50 ijayo waweze kukumbuka wazee wao walitokea wapi na wao wako wapi, kwani asiyejua historia yake ni mtumwa. Kwani kila nchi duniani inajivunia namna walivyojikomboa kutoka katika makucha ya Wakoloni na kujitawala wenyewe, bila ya kuingiliwa na mtu mwengine yeyote.

Mhe, Spika, kamati yetu licha ya juhudi kubwa za serikali zinazofanywa katika kuyaenzi Mapinduzi matukufu ya Zanzibar pamoja na muasisi wetu Mzee Abeid Aman Karume, inashauri kwamba sasa wakati umefika wa kufanya juhudi za ziada, ili kuhakikisha kwamba kumbukumbu za Marehemu Mzee Abeid Amani Karume zinahifadhiwa, zinatunzwa na kuenziwa. Katika kufanya hivyo kamati yetu tunashauri na sisi hapa Zanzibar angalau tuanzishe Kigoda cha Mzee Karume, ili kuenzi kumbukumbu zake kwa ajili ya vizazi vya sasa na vijavyo.

Mhe, Spika, vile vile kamati yangu, inashauri kuwa fungu la fedha zinazotumika kwa ajili ya sherehe za Kitaifa liwekwe kwenye Mfuko Mkuu wa serikali, kwa sababu kuendelea kuuweka kwenye wizara hii ni kuongeza fungu tu katika wizara hii, jambo ambalo ni mzigo mkubwa kwao, hasa kwa kuzingatia fungu lenyewe siku zote linakuwa halitoshi, kwani mahitaji yake ni makubwa mno na idara wakati wote inakua lawamani. Pia wizara ya Fedha wakati wa kupanga *ceiling* ya mawizara huona wizara hii ina fungu kubwa sana, kumbe pesa hizo zote hupita njia tu na hazitumiki wizarani kwa kazi husika za wizara.

Mhe Spika, kamati yangu wakati wa kuipitia bajeti ya wizara, iligundua kuwa kuna milango ya maduka ambayo inamilikiwa na Idara ya Sherehe na Mapambo, lakini kodi yake inakusanywa na watu binafsi, kodi hii haiingii serikalini. Kamati yangu inaitaka wizara kuhakikisha kodi ile inalipwa serikalini, ili kudhibiti mapato ya serikali ambayo siku zote tunaiambia serikali kuwa kuna baadhi ya watendaji serikalini huwa wanachukua mapato ya serikali na kuyatumia wao kwa maslahi yao binafsi pamoja na familia zao. Kwa hivyo, suala hili tunamuomba sana Mhe. Waziri alisimamie ili kuhakikisha kwamba fedha zile za serikali zinarudi serikalini.

IDARA YA UPIGAJI CHAPA NA MPIGA CHAPA MKUU WA SERIKALI

Mhe, Spika, kamati yetu inaipongeza sana serikali, kupitia Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kwa kuhamisha Kiwanda cha Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kutoka Saateni kwenda Maruhubi, jambo ambalo kwa miaka mingi Wajumbe wako wa Baraza la Wawakilishi tulikuwa tukilipigia kelele sana. Kwa hivyo, tunaishukuru serikali yetu kwa kuweza kutekeleza ile ahadi yake.

Vile vile Mhe. Spika, tunaipongeza serikali kwa kuweza kuweka mashine mpya za digitali, ili kuendana na hali halisi ya teknolojia za kisasa, kwa ajili ya kuvutia soko la ndani na nje ya Zanzibar na kiwanda hicho tayari kimeanza kazi zake rasmi. Kwa hivyo, tunaiomba sana serikali yetu kukitumia vizuri kiwanda hicho, na wizara zote zitakazopeleka kazi zao pale, basi walipe pesa taslim na waache ile tabia waliyoizowea ya kukikopa kiwanda mpaka wakakifilisi. Kwani ninaamini wakiweza kulipa kwa wakati, kiwanda kile kitakuwa na uwezo mkubwa sana wa kujiendesha chenyewe na pia baadae kuweza kuchangia katika gawio la serikali kwenye faida watakayoipata hapo baadae, lakini pia kuwapeleka vijana au wafanyakazi wa idara ile, pamoja na watumishi wengine wa kiwanda kile kwenda kwenye mafunzo, ili kuendana na hali halisi na mashine za kisasa zilivyo.

Mhe, Spika, kamati yangu inaendelea kuishauri serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kukifanya Kiwanda cha Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kuwa Shirika, ili kiweze kujiendesha wenyewe. Aidha, kamati inaendelea kusisitiza juu ya suala la kuzitunza na kuzihifadhi nyaraka za serikali kwa ajili ya kumbukumbu za baadae.

Mhe, Spika, kamati yangu inashauri kuwa serikali iendelee kuangalia mazingira mazuri na ya kisasa, ili kukipa hadhi kiwanda hicho ndani na nje ya nchi na kwa ajili ya kukipatia soko kubwa la kibiashara kiwanda hicho.

IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI

Mhe, Spika, moja ya malengo yaliyopangwa kutekelezwa katika idara hii kwa mwaka huu wa Fedha 2014 / 2015 ni kama alivyoeleza Mhe. Makamu wa Pili wa Rais. Kamati yetu inaipongeza Idara hii ya Uendeshaji na Utumishi, kwa kazi kubwa wanayoifanya pamoja na kwamba uingizwaji wa fedha umekuwa kidogo ni mgumu, lakini pia tunawashukuru kwa kuweza kujitahidi kusimamia yale majukumu ambayo waliyojipangia.

BARAZA LA WAWAKILISHI

Mhe, Spika, kamati yetu inaipongeza sana Ofisi ya Baraza la Wawakilishi, kwa kutekeleza majukumu yake kama ilivyojipangia kwa mwaka huu wa fedha 2013/ 2014, licha ya baadhi ya changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa majukumu hayo.

Mhe, Spika, aidha kamati tunaipongeza Ofisi ya Baraza la Wawakilishi, kwa maandalizi mazuri ya Wajumbe yaliyofanywa na Ofisi yake kuelekea kwenye Bunge la Katiba. Semina kadhaa zilifanywa kwa ajili ya kuwajengea uwezo Wajumbe hao, na elimu juu ya masuala mazima ya Katiba mpya, ili kuweza kupata katiba bora kwa maslahi ya nchi yetu ya Zanzibar na Tanzania kwa jumla.

Mhe, Spika, kamati inaendelea kusisitiza agizo lake kwa Ofisi ya Baraza la Wawakilishi, katika kuharikisha kukamilika kwa matengenezo ya nyumba ya Spika iliyojengwa maalum kwa ajili yake, ili ahamie katika nyumba hiyo. Kwa kuwa muda umeshakuwa mrefu tokea kukamilika kwa nyumba hiyo, kamati imeona sio busara kwa nyumba hiyo kukaa bila ya kutumiwa, kwani hatutaitendea haki Ofisi ya Baraza la Wawakilishi na wananchi wote wa Zanzibar.

Mhe. Spika, mara ya mwisho kamati yangu ilipotembelea katika jengo lile, tuliambiwa kwamba kulikuwa kuna tatizo la maji. Kwa hivyo, Ofisi ya Baraza la Wawakilishi tunaiomba kuharakisha upatikanaji wa maji katika jengo lile, ili Mhe. Spika wetu aweze kukaa katika jengo lile la kifakhari ambalo linaendana na hadhi yake ya Uspika.

Mhe, Spika, aidha kamati yetu inashauri kutengezwa ubao maalum, kama ilivyoahidiwa na Baraza lako tukufu, na ubao huo uwe na orodha ya majina ya Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi, waliofungua jengo hili jipya. Kwa hivyo, kazi hii mpaka leo bado haijafanyika na sasa hivi tumebakisha mwaka mmoja tu. Tunaomba sana Ofisi yako ya Baraza la Wawakilishi iweze kutekeleza ahadi yake hiyo.

Mhe Spika, kamati inaipongeza Ofisi ya Baraza kwa kukamilisha ukarabati wa vyoo, na hivi sasa jengo limerejesha haiba yake kwa usafi unaofanywa na Kampuni ya Usafi hapa Barazani. Tunaipongeza Kampuni inayofanya usafi hapa Barazani kwa kazi yao nzuri, na tunawaomba waendelee. Lakini kamati yangu bado haikuridhika na ukarabati uliofanywa katika banda la kuegeshea magari, kwani turubali lililotumika halina kiwango. Tunaomba fedha za umma zitumike vizuri, kwani chombo chetu hiki kinatakiwa kiwe ndio mfano.

Mhe, Spika, kamati inaisisitiza serikali katika kuangalia malipo ya mishahara ya watendaji wa Baraza la Wawakilishi, ili ifuate muundo uliopendekezwa na Ofisi ya Baraza la Wawakilishi. Katika hili Mhe Spika, wewe mwenyewe binafsi tunakutaka kuisimamia serikali ili kuhakikisha sheria yetu ya Utumishi wa Baraza inakuja hapa Barazani kwa haraka, kama tulivyokubaliana na serikali. Kwani haiwezekani sisi hapa kila siku, tunatunga na kupitisha sheria wakati sisi wenyewe hatuna sheria yetu wenyewe inayoongoza Utumishi na Utawala wa Baraza. Hii ni sawa sawa na ile hadithi ya ngariba wa Kilwa, ambaye yeye anatahiri wenzake lakini yeye mwenyewe bado yuko vile vile.

OFISI YA FARAGHA

Mhe, Spika, kamati yangu inaipongeza sana Ofisi ya Faragha ya Makamu wa Pili wa Rais, kwa utekelezaji mzuri wa majukumu yake kwa Makamu wa Pili wa Rais, licha ya ufinyu wa bajeti uliokuwanao, lakini bado ipo haja ya kuiangalia vizuri ofisi hii, kwani ikiweza kufanyiwa kazi vizuri basi hata hadhi ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa kweli itaonesha.

Mhe. Spika, aidha kamati yangu inaendelea kuishauri ofisi hii ya faragha, ili kuangalia uwezekano wa kuweza kufunga *camera* za kiusalama yaani *CCTV Camera*, katika Ofisi ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais. Hili si tu kwa ofisi, bali hata kwa usalama wa mwenyewe Mhe. Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe, Spika, kamati yetu bado inasikitishwa sana na gari za *escort* za viongozi wetu. Suala hili ni muhimu sana na bado kamati itaendelea kulisemea, kwani gari za *escort* za viongozi wetu kwa kweli haziko katika kiwango kilicho bora. Kamati inaishauri serikali kuliangalia vizuri sana suala hili kutokana na umuhimu na uzito wake.

Mhe Spika, ingawa tulipata habari kuwa tunategemea kupata msaada wa magari kutoka Serikali ya Oman, lakini hadi hivi sasa hatujaona mafanikio yoyote. Kwa hivyo, tunaitaka serikali kuutumia mfuko wa *MDRI* kuweza kununulia magari hayo, kwani vingozi wetu hao tunawathamini na sio busara kuongozwa na magari ambayo yako chini ya kiwango.

Mhe, Spika**,** kamati yangu inaendelea kuiomba Serikali Kuu kuliangalia suala la ujenzi wa nyumba za viongozi wetu wakuu wa Kitaifa, hasa kule Pemba, kwani nyumba wanazofikia kamati bado haijaridhika nazo. Aidha, kwa upande wa suala la usafiri wa viongozi wetu hawana usafiri wa kutosha na wa uhakika kwa kisiwa cha Pemba, hasa Makamu wa Kwanza wa Rais na Makamu wa Pili wa Rais. Kwa hivyo, tunaiomba sana serikali kupitia Wizara ya Fedha kuweza kuliangalia suala hili la usafiri na makaazi kwa viongozi wetu hawa wakuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

TUME YA UCHAGUZI

Mhe, Spika, kamati yetu inatoa pongezi za dhati, kwa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, kwa kuendesha uchaguzi mdogo katika Jimbo la Kiembe Samaki, uchaguzi ambao umefanyika kwa uhuru na haki. Aidha, kamati inaendelea kuipongeza Tume, kwa kukamilisha zoezi la uandikishaji wa wapiga kura na uendelezaji wa daftari la kudumu la wapiga kura, ambao uliendelea hivi sasa.

Mhe, Spika, kamati pia inasisitiza juu ya kupatiwa vifaa vya kisasa na vya kutosha kwa Tume ya Uchaguzi, ili kutekeleza majukumu yake kwa kuwa na ufanisi zaidi na kuepusha lawama kwa Tume ambazo zinaweza kuepukika.

Mhe, Spika, kamati inaendelea kuishauri Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, kufanya kazi zake kwa mujibu wa sheria za nchi, ili kuepusha vitendo vya uvunjifu wa amani hasa katika vipindi vya uandikishaji na uchaguzi wenyewe utakapofika.

Mhe, Spika, suala la elimu ya uraia na elimu ya uchaguzi ni muhimu sana kwa wananchi wetu. Hivyo basi, kamati inaendelea kusisitiza juu ya suala hili kwa wananchi, ili wapate elimu ya kutosha katika suala zima la uchaguzi na haki zao kwa ujumla. Pia tunaiomba Tume kufanya maandalizi ya kura ya maoni, ili wananchi waje kuitumia vyema haki yao kuja kuipigia kura ya maoni, kura ya ndio ya Katiba ambayo naamini kwa pamoja Wazanzibari, hasa sisi Wajumbe wa Bunge la Katiba, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tunaotoka Zanzibar, tutaweza kushirikiana kwa pamoja na kuweza kuipitisha na kuiridhia kwa pamoja, ili kuja kuletwa kwa wananchi wetu wa Zanzibar kwa ajili ya kuridhiwa.

Mhe, Spika, kwa ujumla kamati inaiomba sana serikali kupitia Wizara ya Fedha, wajitahidi sana kuipatia Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais fedha za kutosha kwenye idara zake zote kwa wakati, ili waweze kufanya kazi zao vizuri, kwani wizara inakuwa na wakati mgumu sana kwa kucheleweshwa fedha zao kwa kutekeleza majukumu yao.

Mhe. Spika, kabla sijamaliza nilikuwa naomba kama nilivyosema kwamba kitabu kilichelewa, kwa hivyo kuna baadhi ya maeneo ambayo katika hotuba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais sikuweza kuyaingiza katika hotuba yangu. Kwa hivyo, naomba na haya nitakayoyasoma vile vile yaingie katika *hansard*.

Mhe. Spika, Mhe. Makamu wa Pili wa Rais alipokuwa akitoa muhtasari wa hotuba yake, lakini vile vile baada ya kupata kitabu nilijaribu kuangalia katika eneo ambalo amezungumzia hali ya kisiasa.

Mhe. Spika, kama alivyoeleza Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, hali ya kisiasa Zanzibar hivi sasa sio mbaya inaendelea vizuri. Kwa hivyo, na mimi kwa kushirikiana na yeye nawaomba wananchi, lakini vile vile na sisi viongozi wa kisiasa tuendeleze umoja wetu na mshikamamo wetu na tuondoe sintofahamu ndogo ndogo ili kuhakikisha kwamba tunawatumikia wananchi na tunawaletea maendeleo.

Vile vile nataka nitoe pongezi kwa uchaguzi wa Jimbo la Kiembe Samaki, lakini vile vile tumpongeze Mhe. Mwakilishi, Mhe. Mahmoud Thabit Kombo ambaye yeye ndiye aliyeibuka mshindi na hivi sasa anawawakilisha wananchi wa Jimbo la Kiembe Samaki.

Vile vile Mhe. Spika, Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwenye hotuba yake alielezea kuhusu suala la Idara inayoshughulikia Uratibu, pia na masuala ya Muungano. Mhe. Spika, suala hili kama alivyoeleza Mhe. Makamu wa

Pili wa Rais, pia katika Idara ya Uratibu ambayo wanashughulikia masuala ya Muungano. Wameeleza pia yale mambo ambayo yamepatiwa ufumbuzi na yale ambayo hayajapatiwa ufumbuzi.

Lakini pamoja na yote hayo Mhe. Spika, nadhani wakati muafaka sasa hivi sisi kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na kwa kumtegemea yeye Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, tunamuomba tena na ninamuomba rasmi kama Mwenyekiti wa Wenyeviti wa Kamati zote za Baraza la Wawakilishi, basi Mhe. Makamu wa Pili wa Rais atuite wenyeviti wake wa kamati zote, ili tukae naye na tuweze kushauriana ni namna gani bora tutakayoweza kufanya tukarudi Bungeni tukawa wamoja, ili kuweza kushikamana na kuweza kuiletea maendeleo nchi yetu. Vile vile kwenda kupitisha katiba ambayo itakayokuwa bora kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wa Zanzibar, vile vile na Watanzania wote kwa jumla. Naamini Mhe. Makamu wa Pili wa Rais hili atalichukua, kwa sababu kama tunavyomjua ni mtu msikivu, na mara nyingi kamati yangu inapokuwa inatoa ushauri ofisini kwake, basi huwa hapuuzi ushauri huo.

Mhe. Spika, pia Mhe. Makamu wa Pili wa Rais alielezea suala la migogoro ya ardhi. Mhe. Spika, tunaishukuru sana serikali yetu kwa kuipokea kwa pamoja na kuiridhia kwa pamoja ripoti ya kamati iliyokuwa inasimamia migogoro ya ardhi, ambayo wewe uliituma. Naamini hivi sasa serikali wanaichambua na wanaendelea kuifanyia kazi. Lakini kama tunavyojua Mhe. Spika, migogoro ya ardhi inagusa sana maisha ya wananchi. Kwa hivyo, tunamuomba Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, kwa yale ambayo yanaweza kutekelezeka kwa haraka, basi yaweze kutekelezwa ili wananchi wetu waweze kupata afueni na maisha yao, na kuweza kuitumia ardhi yao kwa maslahi yao na familia zao.

Mhe. Spika, vile vile tunaipongeza serikali kwa kauli ya Mhe. Makamu wa Pili ya Rais, kwamba Idara ya Uratibu huwa inachukua masuala yote na ahadi zote ambazo serikali inazozitoa hapa Barazani. Kwa hivyo, serikali kwa kweli imeshatoa ahadi nyingi, lakini bado nyingi hazijatekelezwa. Namuomba sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, ahakikishe kwamba anawasimamia watendaji wake ili zile ahadi ambazo zinakuwa ngumu kutekelezeka, wampelekee yeye ili aweze kuzisimamia na kuzipatia ufumbuzi.

Mhe. Spika, Mfuko wa Jimbo. Tunaishukuru sana serikali yetu na tunaishukuru sana Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, lakini vile vile na Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, baada ya kuendelea kututengea fungu la shilingi milioni 750 kwa mwaka uliopita. Vile vile walituwekea kwa mwaka huu wa fedha, lakini baada ya maombi maalum ya Kamati ya wenyeviti, Mhe. Makamu wa Pili wa Rais baada ya kushauriana na Mhe. Rais tunashukuru sana walikubaliana na sisi ili fedha zile zitoke kutoka milioni 750 ili ziwe bilioni moja kwa ajili ya kusogeza huduma za maendeleo ya wananchi wetu.

Mhe. Spika, kwa kuwa muda uliobakia ni mdogo kumaliza bajeti yetu hii na fedha zile mpaka sasa hivi bado hazijatoka. Kwa hivyo, nadhani Mhe. Spika, mimi nikiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti, nitaweza kusaidiana na Mhe. Waziri wa Nchi Katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kuhakikisha kwamba Waheshimiwa wanarudisha haraka zile *return;* na wale ambao watakaochelewa, basi tutaiagiza Ofisi ya Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali, kwa sababu wao ndio hasa wenye majukumu ya kuweza kusimamia na kufuatilia mahesabu haya. Kwa hivyo, fedha hizo Mhe. Spika, naomba chonde chonde Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ziende majimboni ili zikaweze kutusaidia kutatua matatizo ya wananchi wetu.

Mhe. Spika, kwa kumalizia ukurasa wa 71 nilivyojaribu kuangalia nimeona Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Mhe. Spika, kwa mara ya kwanza kitabu hiki kwa kweli kimeripoti vizuri kazi ambazo inazifanya Idara hii ya Uratibu wa Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kule Dar es Salaam. Kwa hivyo, naomba sana nilipoangalia ile ripoti ya kitabu hiki ukurasa wa 71 kwa kweli wamefanya kazi kubwa ya kufuatilia ile mikutano ya mashirikiano baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na nchi wahisani, kwa hivyo tunaomba basi yule Mkurugenzi wa Idara ile aweze kuhakikisha anafuatilia, lakini vile vile katika mwaka ujao tuone basi yale ambayo aliwaeleza katika ile mikutano aliyoifuatilia ambayo tunategemea Zanzibar itaweza kufaidika basi tujue ni lipi na lipi limeweza kutekelezwa.

Lakini mwisho kabisa Mhe. Spika, nataka nimpongeze tena Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais katika bajeti ya mwaka uliopita nilisimama hapa na nikamuomba sana ili kuhakikisha kwamba afanye ile ziara ya Marekani ambayo tungelitegemea ingelileta maendeleo makubwa na msaada mkubwa kwa Zanzibar. Namshukuru sana Mhe. Spika, na kwa bahati nzuri katika ziara ile aliungana nami na ninamshukuru vile vile hivi juzi tu matunda ya ziara yake ile yameonekana kwa sababu tayari amekabidhi kwa Wizara ya elimu kontena la futi ishirini ambalo lilikuwa na

kompyuta 250. Kwa hivyo kompyuta zile tunategemea Wizara ya elimu itaweza kuzisambaza kama walivyoagizwa na Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais ili zile kompyuta nyengine 750 ambazo tunagemea zitakuja baadae basi tuweze kuzipata, kwa sababu bila ya kuweza kutunza vizuri kompyuta zile tusitegemee kama hizo nyengine zilizobakia tutaweza kuzipata.

Lakini vile vile tunashukuru katika kontena lile Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais alipatiwa vile vile msaada wa vitabu zaidi ya 5000, kwa hivyo tunategemea Wizara ya Elimu vitabu vile watavitumia katika *library* mbali mbali za maskuli yetu kwa ajili ya kuleta ufanisi na maendeleo kwa vijana wetu.

Baada ya hayo machache Mhe. Spika, nawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuijadili, kuichambua, kuikosoa pale inapobidi lakini vile vile kuishauri vizuri Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais na baadae kuipitisha kwa pamoja bajeti hii ili kumpa nguvu Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais aweze kusimamia Serikali katika kutekeleza majukumu yake.

Baada ya hayo Mhe. Spika, naunga mkono kwa niaba ya Kamati kwa asilimia mia moja, ahsante sana Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, na mimi namshukuru Mwenyezi Mungu jioni hii kuweza kuwa mtu wa mwanzo kuchangia bajeti ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, kwanza nimshukuru Mwenyewe Mwenyezi Mungu *Subhaanahu Wataala* na mimi kuweza kunipa pumzi saa hizi nikamudu na kuweza kuchangia hotuba ya Makamu wangu wa Pili.

Mhe. Spika, leo niseme kuwa kwangu mimi itakuwa ni maajabu; na maajabu haya ni barka ndani yake sababu mara nyingi huwa namsikia tu Mheshimiwa Makamu wa Pili akitoa hutuba za kufunga, lakini leo nimemsikia mwenyewe kasimama na kakichambua hiki kitabu na kuweza kusoma mwenyewe bajeti yake ili tuweze kuichambua vizuri kama alivyosema Makamu wangu na mimi nitafanya hivyo, mimi leo nitakuwa mtaalamu tu wa mambo madogo madogo sitokuwa na *comment* nyingi sana za kupingapinga.

Mhe. Spika, nianze na ukurasa wa 18 ukurasa huu kuna mambo mawili makubwa; jambo la kwanza suala la sekta ya afya. Ninaomba sana tu, kwa kuwa tunajua tuna upungufu wa madokta bingwa, tuna upungufu wa baadhi ya mambo ambayo kwenye hospitali zetu yanakosekana hasa vifaa vya kisasa.

Mheshimiwa Makamu nakuomba sana jitahidi sana unapokwenda nje mara hii si lazima unichukue mimi lakini ukienda wewe jaribu angalau kutuombea vifaa vya afya, nakuomba ukifika tu jaribu kutafuta au ondoka na *project* labda hapa, mimi nashangaa au nijaribu kuwauliza wataalamu wanapokuwa wanakwenda nje wanakwenda na *briefcase* au wanakwenda na *special project* sasa hili kidogo nalishangaa sana lakini wakirudi wanarudi wao tu hatuoni vitu vyengine, naomba sana ushauri wangu mara hii mkienda nendeni na zile *project* ili tuwaachie vitabu wale wenyewe wataalamu halafu wenyewe waone jinsi gani tunavyofanikiwa. Mara nyingi sana wakubwa mnakwenda lakini tunachukua miaka mingi mpaka tunamaliza uongozi hatuoni kitu kinachoendelea, sasa naomba sana kwa ushauri wajaribu sana kufanya vitu hivyo wachukue wataalamu ambao wanajua ku- *write up* hiyo *project* na unao ofisini kwako nitakuja kukutajia baadae.

Lakini Mheshimiwa masuala ya migogoro kila siku kitabu chako kitakuwa na migogoro ya ardhi; natoa ushauri wa bure tu wala msitafute mtaalamu, ushauri wangu Mheshimiwa unda *task force* kwa nia nzuri tu wanaopata tabu ni wapiga kura wetu katika masuala ya ardhi tena wanakuwa wananyanyasika kwa sababu ardhi ni moja katika njia ya kumgomboa mwananchi aondokane na umasikini, ndio matatizo yanakuwa mengi sana mengine tunayasababisha sisi wenyewe viongozi tuwe wawazi kusema ukweli. Lakini mengine yanatokana na wao wenyewe wananchi wengine kwa tamaa zao wanauza kwa watu mara mbili au mara tatu, sasa hiyo ningeomba sana Mheshimiwa wangu uunde *task force;* unda vikundi ambavyo tukiwemo na sisi tukusaidie, washirikishe Waheshimiwa na wahusika wenye idara maalum za ardhi nao wahusishe ninakuhakikishia kwa muda wa mwaka mmoja tu suala hili litaondoka kabisa, wala bajeti nyengine sitarajii kama litakuja tena suala hili.

Lakini kwa wewe mwenyewe kwa sababu sheria inakupita ndio tatizo lenyewe twende kwenye sheria, sheria Makamu unashindwa kuli-*final* hili suala; sheria haikupi wewe useme ufute huna uwezo huo kwa mujibu wa sheria, lakini tukiunda *task force* tukaifanyia marekebisho ya sheria kwa kupitia ile idara yenyewe ya ardhi nafikiria suala hili Mheshimiwa litakuondoka, sana mimi nilikuwa nataka kuleta hoja kwa Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais

awe na uwezo aidha wa kumuondoa Waziri mara moja nilikuwa nataka alete sheria hiyo, lakini bado ipo kwenye kabati inatengenezwa kwanza ili tumpe meno Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais. Kwa sababu yeye ndio mtendaji mkuu imo labda mwakani nikirudi tena Barazani sheria hiyo itakuja ili tuweze kuona utendaji wake una ufanisi kabisa.

Mhe. Spika, tatizo limekuwa kubwa sana kila siku linakuwa kubwa tu, tunasema yanapungua ni kweli yanapungua lakini na mapya yapo, leo nataka nikwambie namshukuru sana Katibu wangu wa majenzi na ardhi pamoja na Mkurugenzi wake tulikwenda *field* leo kabisa wao wenyewe wameona, tena namshukuru sana Katibu huyo wa majenzi amekwenda ametoa uamuzi hapo hapo, ndio maana nikasema kuwa tukishirikishwa na sisi basi inakuwa afadhali na suala linakuwa zuri sana; ndio maana nikasema Makamu wa Pili wa Rais atutafute na sisi tushirikishwe. Mhe. Spika, limetatuka suala ambalo ni *simple wallahi laadhym* na lilikuwa lina muda mwingi sana lakini leo kwa kuwa mwenyewe nipo pale, na watu wengine wapo pale; wanasheria na mimi nikasaidia vijisheria vidogo vidogo pale Mhe. Spika, Katibu katoa uamuzi keshokutwa wanafunzi wanaondolewa. Sasa hivyo ndio tunavyotaka Mhe. Spika, tunamrahisishia Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais uwe na hiyo kamati *special* ya kuondoa tatizo, si hivyo kila siku tutakuwa na matatizo ya hapa na pale hayeshi.

Mhe. Spika, suala la walemavu namuomba sana Mhe. Makamu wa Pili na wahusika zaidi naomba sana tuwasaidie sana watu wetu hawa tuwasaidie kwa hali na mali, tusifanye mchezo Mheshimiwa tuwasaidie katika mambo yaliyokuwa na umuhimu sana, kwa mfano kuna mambo ambayo wanashindwa kuyapata kwa mujibu wa utaratibu wa ulemavu wao na pamoja na zile sheria zinawakwaza, ninaomba sana tuwape kipaumbele katika ajira, zikija tuwasaidie, ofisi yako Mheshimiwa Makamu wa Pili isimamie, misaada ya hapa na pale kwa walemavu naomba sana tuwasaidie tuwape kipaumbele sasa mimi naomba hasa Mhe. Spika, bora wangekuwa sasa hivi mwanzo wao halafu sisi tuwe nyuma tuliokuwa wazima mimi naomba sana kwa ushauri huo. Kwa sababu asilimia ndogo wamo wanaofanya kazi , ni asilimia ndogo sana, asilimia ndogo wanapata misaada midogo sana kufanya biashara naomba sana, nilisikia leo wenzetu kule Tanzania Bara walemavu walifunga njia kutokana na kuwa hawakupata haki ya eneo la kufanyia biashara Mheshimiwa eneo hatujawatafutia ndugu zetu hawa, naomba sana Mheshimiwa Makamu wa Pili simamia na wao watafutiwe eneo wakafanye biashara, tukawajua hasa wenzetu hawa wako sehemu fulani pahali pazuri mazingira yao wamepewa kwa kufanya biashara ninaomba sana kwa hilo wasaidiwe wapewe kipaumbele, lakini inakuwa kazi yetu kusema tu hapa tatizo lenyewe utekelezaji wake unakuwa mdogo.

Mhe. Makamu wa Pili Katibu wangu mpendwa kabisa naomba sana Mhe. Spika, nikupe hadithi ndogo ya Katibu wa Wizara hii Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, huyu ni dokta sifa yake moja anapokaa pahali basi yeye akiondoka anaacha jina, alikuwa Katibu wa kilimo watu wamenufaika wengi wamepata ardhi za kulima, aliyekuwa hakupata ardhi bahati mbaya mpaka leo wanasema *alhamdulillah* watu wanashukuru wanapanda mihogo na minazi kutokana na yeye, na vile ndio inavyotakiwa dokta sio ndani ya *briefcase;* dokta vitendo, ninaamini kwa hili dokta huyu ataifanya kazi ataondoka hapo na jina atakwenda kwengine sio aondoke ndio mwisho wa kazi bado Mwenyezi Mungu anamjaalia uhai anao, uzima anao, uzuri ataendelea kufanya kazi na kwengine kwa baraka za Mwenyezi Mungu mwenyewe.

Naamini dokta huyu atakapokwenda pengine na hapo ataacha jina kuwa ameshawapatia eneo ndugu zetu wenye ulemavu ili waweze kufanya biashara za kisasa, naamini hilo na ndio kazi ya dokta, sio dokta ndani ya *briefcase.* Mimi naamini hiyo na atafanya kazi hiyo, namshukuru sana na tunaona neema zake, *inshaallah* Mwenyezi Mungu azibariki.

Mhe. Suala la madawa ya kulevya Mheshimiwa Makamu hapa ndio kunapo utata. Nakumbuka siku moja kulitokea tatizo Uwanja wa Ndege CCTV zikaambiwa hazifanyi kazi, lakini CCTV ile ile kuna mtu imeonesha mkono, mimi nasema hatujawa *serious,* hili suala tunafanya mzaha mzaha kwa kutaka kulindana tu, hatujawa wakweli katika suala hilo Mheshimiwa, lakini la kusikitisha Makamu wa Pili kuna watu mpaka leo wamenyang'anywa vitambulisho wasifanye kazi sio wahusika, waliokuwa wahusika jamani yale mambo tumewaachia mpaka leo hii Mheshimiwa Makamu bado fuatilia suala hilo mimi sijaridhika nalo. Mhe. Haji Omar Kheri Mheshimiwa Waziri alilifuatilia lakini mwishowe sijui limefikia wapi, sasa namwambia Mheshimiwa nenda wapo watu waliokuwa wafanyakazi wa mule ndani waliohusika na mabegi yale, nitafute nitakwambia!

Mhe. Spika, kwa kweli hili suala linasikitisha sana; kuna vijana ambao wanafanya kazi pale ZAT hawahusiani na masuala kama hayo wamedhalilishwa kupelekwa polisi, lakini kuna wenyewe wahusika hawa wameachiwa huru. Leo mimi nashangaa CCTV ikaharibike ina maana gani kuwekwa pale Uwanja wa Ndege, lakini CCTV ile inafanya

kazi kwa kuonesha mkono mmoja tu tena huyo mtu alikuwa akionesha jamani mbona yale mabegi yapo pale kwa muda mrefu, yamekaa muda mwingi, kuna mtu kenda kuweka na huyo mtu anajulikana kusema la ukweli ulivyo, na vijana wako tayari kutoa hiyo siri.

Naomba sana Mhe. Spika, naomba Mheshimiwa Makamu wa Pili tekeleza wajibu wako, lifuatilie na hao vijana warejeshwe Uwanjani wapewe vitambulisho waendelee na kazi zao kwenye Idara nyengine ya ZAT, ninaomba sana Mheshimiwa kwa hilo iwe mfano, Mheshimiwa onesha mfano kwa sababu hao waliozuiliwa ni masikini ndio rizki yao wanapata pale, na kwa sababu Polisi wamewaambia endeleeni kufanya kazi, kwa sababu Polisi ndio muamuzi wa mwisho.

Keshaona huyu hana hatia kwa nini tunazuia vitambulisho? Naomba sana Mheshimiwa hebu tuwe na imani na hawa wanyonge jamani, turidhike na sisi na hicho tunachokipata, kazi yetu jamani msifikiri ukubwa huu tunauona hapa duniani, ukubwa huu hata kwa Mungu unakwenda kuulizwa tusifanye mchezo, hichi sio kiti cha mchezo kusema mimi kiongozi, mimi mkurugenzi, mimi katibu mimi nani.

Mhe. Spika, Wakurugenzi wengine hasa mizigo kuwekwa kwenye Serikali niseme ukweli ulivyo; ni mzigo kwenye serikali. Unaweka mtu ambaye haelewi nini madhumuni ya kazi yake, tena mzigo wa kuni, hebu nambieni kwa nini nisiseme ni mzigo hichi kitu kinaumiza sana Mhe, Spika, kwa hivyo mimi naomba sana Mheshimiwa Makamu wa Pili ninavyokujua wewe utaifanya hii kazi na nenda wamefukuzwa mpaka kwenye mafuta watu kwenye Shirika la Orange wamefukuzwa, vijana wamefukuzwa bure waletaji unga hawakufukuzwa haki ya Mungu nakwambia, wamefukuzwa bure, uonevu tu basi, haiwezekani! Mimi hilo suala linaniuma sana, tumuogope Mwenyezi Mungu jamani hii kupita *luxury* tu; tuogope Mwenyezi Mungu, tusichukue madaraka kwa kudhalilisha masikini ya Mungu, ni hatari, mimi naogopa sana ndio maana nawatetea hapa.

Mhe. Spika, nikiingia ukurasa wa 22 Mazingira. Nilisema sana kuhusu mazingira hali halisi tunayokwenda nayo vizuri sana, na nijaribu kusema sana Mheshimiwa kuwa tujaribu kuleta *modality* ya sheria sasa hivi ya mazingira au sera.

Mhe. Spika. Unazo dakika tano.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Zinanitosha hizo.

Mhe. Spika, nimshukuru sana Mkurugenzi kwa kutaka kutuletea sasa hivi sheria, nafikiri itakuja wakati wowote ambayo inaonesha jinsi gani sasa tunasimamia sheria ya mazingira kihaki *lillahi taala*. Mazingira sasa hivi yanaharibiwa kwa nguvu sana, lakini *inshaallah* kheri na nikaomba sana Mkurugenzi huyu awe kila baada ya muda anatoka *out* anakwenda nchi za nje kuangalia hali halisi ya wenzetu jinsi gani wanavyoweka nchi zao kwa mujibu wa sheria za kimazingira, nimeomba sana suala hilo na naamini hilo suala litakuwepo na ataweza kusaidiwa kabisa.

Mhe. Spika, kwa kutaka kumalizia muda wangu huo niko kwenye Idara ya Maafa, hapa ndipo kwenye hali halisi ya nchi hawa ndio roho, nimeomba sana tuwatafutie vifaa ambavyo vinakwenda na wakati nikaambiwa *radio call* zipo, gari kama hakuna itakuwa wapatiwe hichi kitengo ni muhimu sana, hali halisi mnaona yanavyotokezea majanga hapa, tuwape kila aina ya vifaa, tukate kama tulivyofanya harambee ya meli, dokoa dokoa kwenye bajeti humo Mhe. Waziri wa Fedha dokoa bajeti humo ili zipatikane fedha za kuweza kuwapatia vifaa vya kisasa; hawana hawa vifaa vya kisasa Mheshimiwa. Wataalamu wanao lakini bure tu kwa sababu mtaalamu hana kitu cha kutengenezea, ninaomba sana wapatiwe hivyo vitu ili kuweza kufanikiwa.

Mhe. Spika, nikimalizia nirudi tena hapo nimshukuru sana Katibu kwa jitihada zake za kufanikisha sherehe za kutimia miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar hali kadhalika na ya Muungano; nishukuru sana amejitahidi sana sijui kama usingizi mpaka leo kama amekwisha kuulala, amefanya shughuli imekuwa vizuri tumependa sote, na tumeona jinsi gani ambavyo sherehe ilivyokuwa kubwa na ya aina yake sijapata kuona mpaka leo mwemvuli ninao ndani nimeweka na sikutegemea kama ningepata katika sherehe hii kutokana na ile hali halisi, nimshukuru sana sana.

Na mimi naungana Mheshimiwa Mwenyekiti fedha zile ziwekwe katika fungu ambalo litakuwa linaonekana pale ili kuweza kusaidia sherehe hiyo kwa kupitia Wizara hii, kwa sababu fungu hilo tukilitia mule tunamnyima yule haki Mheshimiwa Waziri, inakuwa tunamwambia *other charges* akishapata kumbe lile fungu sio lake tunakwenda

kumuongezea mzigo wa bure, lakini likikaa pembeni baadae zile *other charges* ili aweze kufanya shughuli zake kumalizia.

Mhe. Spika, nimalizie suala la visakina nimeshasema sana suala la kisakina siku moja nilikuwa katika kamati ya Katiba na Sheria tulikuwa na Mhe. Ali Mzee, tulikuwa mimi na wengine, Mheshimiwa tulikwenda kwa Waziri wa Mambo ya Ndani tulikuwa majabari kweli, sisemi uongo tulikuwa mimi na Mhe. Ali Mzee nilianza *issue* ya kusema jamani ee visakina vinasukumwa. Mhe. Ali Mzee na yeye akalikamata hilo suala akasema hii ni aibu. Lakini *wallahi* Mhe. Spika, huwezi kuamini, wakati ule alikuwa Waziri gani yule Rolase Gama, kufika jioni tunapigiwa simu kwa jina jengine Masha; tunaambiwa tayari visakina vishapelekwa Zanzibar haki ya Mungu ninakwambia Mheshimiwa!

Lakini leo Mhe. Makamu wa Kwanza, Mhe. Rais anatembea na gari nzuri kisakina kibovu, haki ya Mungu nakwambia ni kitu cha kuchekesha kikubwa sana Mhe. Spika, mimi nashangaa. Ukiliona gari la Mhe. Makamu wa Pili ni zuri; *fantastic* nakwambia Mhe. Spika, lakini leo ukija kuangalia Mhe. Makamu wa Kwanza gari yake ni nzuri kisakina kibovu, lakini Mhe. Rais na yeye gari lake zuri ukiangalia kisakina ndio kile kile cha miaka 20 ya nyuma huku kibovu ndio unaambiwa *escort*, lakini ki-*escort* ndio hicho kisakina hamjui. Mheshimiwa hiyo hiyo kisakina ndio nilivyozoea mimi hicho.

Sasa naomba sana Mheshimiwa kama huyo Omar sasa hivi mwambie haraka ni aibu. Mheshimiwa ni aibu kubwa sana. Mimi leo ninavaa koti zuri tai mbovu haiwezekani Mhe. Spika, ni aibu! Ninaomba sana Mheshimiwa wangu tuwaletee visakina viwe vizuri vyende kwa wakati kama wenzetu wanavyokwenda na zile honi zao za kutisha zile hooo viletwe vile tuvione, lakini hata leo ninakwambia Mhe. Spika, hata ile honi husikii. Kwa hivyo Mhe. Spika, mimi naomba nimshukuru sana Mhe. Waziri wangu Mhe. Mohamed Aboud, nimshukuru Makamu wa Pili, nimshukuru Katibu pamoja na Naibu Katibu, watendaji wake na Wakurugenzi.

La mwisho Mheshimiwa kama tulivyosema Tume ya Uchaguzi nayo Mheshimiwa ipewe vitu vya kisasa ili ifanye kazi zake kwa uhuru na wapewe safari za kuangalia chaguzi za wenzetu zinavyokwenda. Kwa hayo machache Mheshimiwa ninaunga mkono mia kwa mia.

Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali: Mhe. Spika, kwanza tupongezane sote Wazanzibari kwa sherehe zetu ambazo zilizofanyika kutimiza miaka 50 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar, napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais akiwa Mwenyekiti wa Kamati ya sherehe zetu hizi za Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar.

Mhe. Spika, bila ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar leo tusingelikuwa hapa tuliposimama na kujadili na kuongea nafasi yetu ya kujitanua kabisa katika ardhi yetu ya Zanzibar. Na niipongeze serikali kwamba ukumbi huu umechanganyika rika mbali mbali, kabila mbali mbali. Hii inaonesha uimara na usimamiaji wa Mapinduzi yetu Matukufu ya Zanzibar.

Mhe. Spika, mimi naipenda nchi yangu na nina uchungu na nchi yangu, nataka nimuhakikishie Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na viongozi wote wa kitaifa kwamba sitovunjika moyo, nitaendelea kwa hali na mali kuisaidia Zanzibar yangu kwa sababu nina uchungu wa Zanzibar bila kujali kabila, rangi, dini na mambo mengineyo. Kila nitakapokuwa na uwezo Mwenyezi Mungu akinijaalia basi nitatizama watu wangu wa chini na pale panapohitajika kuisaidia nchi yangu.

Mhe. Spika, jambo lililokuwa limenisikitisha sana, na kama nilivyosema sitovunjika moyo nitaendelea ninajua hii ni wachache tu kwamba tulipofikwa na sherehe zetu za Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar Serikali iliunda Kamati ambayo Wajumbe wake wote ni wateuliwa wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya *Mapinduzi Cup* ni dada yangu Sherry ambaye vile vile ni Mwenyekiti wa Baraza la Michezo Zanzibar. Katibu Mkuu Wizara ya Habari Dr. Mwinyikai yeye ni Mjumbe katika kamati hiyo ya *Mapinduzi Cup*. Naibu Katibu Mkuu na viongozi wengine Mhe. Nassor Salim Ali, Ali Khalil pamoja na Makatibu wote.

Mhe. Spika, wakati tunajiandaa kwenye sherehe hizi; hizi sherehe ni zetu na shughuli hii ilikuwa ni yetu, kwa hivyo tulikuwa tunasimamia kwa hali na mali sherehe hizi zifane ili tuwe na makumbusho makubwa ya Mapinduzi ya miaka 50.

Mhe. Spika, kamati hii ambayo inasimamiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar sisi kama wafanyabiashara na wadau tulitoa michango mbali mbali, kampuni mbali mbali, ikiwemo Kampuni yangu ya *Hassan & Sons* pamoja na Kampuni ya *Airport Ground Handling* tulitoa karibu milioni 10 kuzipa sherehe za Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar.

Mhe. Spika, kinachonisikitisha Mhe. Spika kwa sababu nina vielelezo, Mhe. Spika, tokea nilipoteuliwa ninamshukuru Mwenyezi Mungu na Mtume kila nilipokuwa ninasimama basi nina vielelezo na nina ushahidi wa kutosha, tokea siku niliyoteuliwa na wananchi wa Jimbo la Uzini.

Mhe. Spika, wenzetu walipozidiwa walifanya *booking* karibu hoteli 13 na zilikuwa zinahitajika pesa kwa sababu ya kuweza kufanikisha Mapinduzi yetu Matukufu katika suala la Michezo kwa jumla. Basi Mhe. Spika, baada ya kukaa viongozi wenzangu nilitakiwa kuisaidia Kamati hii ya *Mapinduzi Cup* ambayo inasimamiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mlezi wa Kamati hii ni Mhe. Makamu wa Pili wa Rais; hoteli 15 Mheshimiwa zilitakiwa milioni 71,410,000 sawa na dola 45,629.

Mhe. Spika, kwa sababu nina uchungu na nchi, heshima ya nchi yangu, heshima ya Rais wangu pamoja na Wazanzibari, wenzangu hawa walinifuata kiwandani, alikuja Mwenyekiti wa Baraza la Michezo ambaye vile vile ni Kaimu Mwenyekiti wa *Mapinduzi Cup*. Alipokuja Kiwandani na maelekezo ya kutaka pesa hizi ili nchi yetu isipate aibu, ili hizi pesa zinazohitajika zikalipwe kwenye hoteli hizo. Na ilikuwa *deadline* siku moja.

Mhe. Spika, kwa sababu nina uchungu na nchi na wenzangu hawa niliotoka nao na wazanzibari ndio walionifikisha mimi nilipofika. Mhe. Spika, nilikwenda baada ya kunitaka Mwenyekiti alipokuja Kiwandani nikaingia kwenye gari yake kwa makubaliano kwamba zikimaliza sherehe za Mapinduzi kwa sababu ahadi zilikuwa nyingi zaidi ya milioni 200. Lakini unajua wafadhili si rahisi pale kwa pale kutoa pesa, kwa hivyo zilihitajika pesa hizi zikalipwe hoteli baada ya siku mbili, hizi zilizohitajika milioni 71 zikalipwe hoteli 15 ili hoteli zile zisifute timu zile zilizokuja hapa Zanzibar ndio lengo moja.

Mhe. Spika, mimi si benki wala sina kazi ya kukopesha na laiti hizi pesa milioni 71 wangelitaka kwa ajili ya matumizi ya *Mapinduzi Cup* au ya sherehe mimi nisingelitoa. Lakini pesa hizi zilihitajika kwa makhsusi kama zikalipwe hizo hoteli 15 ili tusiathirike na Mapinduzi.

Mheshimiwa nilipanda kwenye gari na nilipofika benki pamoja na Mwenyekiti wangu dada yangu Sherry, nilipofika benki MD alinambia Raza kuna mapungufu kidogo ya pesa hazitimii kwenye *account* yako milioni 71 na hizi pesa nilimwambia zinahitajika leo. Mhe. Spika, niliweka rehani mimi nyumba yangu pale pale kwa kuona, kwa sababu nina uchungu na nchi, nina uchungu na Mapinduzi matukufu ya Zanzibar. Nikapewa milioni 71 nikaingiza kwenye *account* ya Mapinduzi Cup ambapo Mhasibu ni wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, nikaziingiza hizo pesa milioni 71,400,000 na makubaliano kwa siku ile kwa sababu *rate* ya dola ilikuwa 1565. Tukakubalina watapokuja kunirejeshea kuna dola kupanda na kushuka basi nije kulipwa dola 45,629 kwa mujibu wa *rate* ile ya benki iliyokuwepo pale.

Mhe. Spika, baada ya kukabidhi pesa hizi kwa sababu nimeendelea, ilipofika Januari kimya, ilipofika mwezi wa Februari nikaulizia na nilipoandika barua Mhe. Spika, sikujibiwa. Sasa kutokana na wasiwasi wangu Mheshimiwa Spika, ikabidi zile hoteli zote nikazifuate nizitizame kweli hizi pesa hazikuchakachuliwa. Kwa hivyo Mheshimiwa nikaenda kwenye hoteli ile kwa mfano, kuna hoteli ya Kilimani ilikuwa walipwe milioni 11,700,000. Sasa nilipokwenda nikawaambia jamani hapa mimi naomba nikusaidieni, wakasema loo Raza sisi hatukupata hizi pesa, tulipata *cheque* ya 3,000,000 hii. Nikawaambia nitoleeni kopi. *(Makofi).*

Nikaenda hoteli nyengine walikuwa walipwe 5,000,000, milioni mbili nikawaambia nitoleeni kopi, kwa sababu Mheshimiwa pesa nilizotoa na serikali ikaamua kutoa hizi ili kuondoa aibu kwamba hizi hoteli zikalipwe. Kwa hivyo mimi Mheshimiwa tatizo langu moja kwamba zile pesa nilizotoa kwa madhumuni zikalipwe hoteli hazikulipwa kwa kipindi kile.

Sasa Mhe. Spika, baada ya yote hayo nilipozungumza na wenzangu hawa ambaye Katibu Mkuu Dr. Ali Mwinyikai ndiye mjumbe ndie aliyesimamia. Sasa wenzangu Mhe. Nassor Salim alikuwemo kwenye kamati, Katibu Mkuu Ali Khalil alikuwemo ndani ya kamati, Farouk Karim alikuwemo ndani ya kamati na hii kamati ndio ya watu saba hii. Sasa Mhe. Nassor Salim akanambia Raza mbona umetuacha, nikamwambia lakini si nimetoa mchango wangu wa

10,000,000 kama Kampuni, lakini isitoshe haya Mhe. Nassor Salim na Farouk mbona nimekukopesheni bila ya riba, bila ya faida nimetoa 71,000,000 *cash*. Mhe. Nassor Salim wakasema sisi mbona hatuna taarifa, Mheshimiwa sukari yangu ilizidi kupanda badala ya kushuka.

Maana yake Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi yumo ndani ya Kamati, Katibu Mkuu Ali Khalil yumo ndani ya Kamati hawajui kama zile pesa wametoa. Sasa Mhe. Spika, inaonekana watu wanne tu hao. Katibu wa Baraza la Michezo ndiyo Katibu wa Mapinduzi Cup, Mwenyekiti wa Baraza la Michezo ndiye Mwenyekiti wa Mapinduzi Cup, Katibu Mkuu Wizara ya Habari ndiye Katibu wa Mapinduzi Cup. Kwa hivyo Mheshimiwa hawa watu wanne mpaka wale wenzao waliokuwa pamoja wamewatenga.

Sasa kwa bahati Mhe. Nassor Salim alipokwenda sasa kwenye Kamati akasema jamani kuna taarifa kwamba Raza ametukopesha 71,000,000 na hii Kamati tumeshakutana zaidi ya mara kumi wale wakasema ee ndio kweli kweli. Akawaambia lakini tulikutana zaidi ya mara kumi hizi pesa zimeshatoka zaidi ya mwezi mmoja, ZFA na wao walikuwa hawajui.

Kwa hivyo Mhe. Spika, kitu kilichokuwa kimeniumiza zaidi kwenye Kamati ya Baraza la Wawakilishi kwa bahati mimi ni Mjumbe ndani ya Baraza, mama yangu Mhe. Asha Bakari ndani ya Kamati ambayo Waziri muhusika mzee wangu ninamuheshimu sana Waziri wa Habari, Naibu Waziri alikuwepo, Katibu Mkuu Dr. Mwinyikai alikuwepo, basi mama Asha aliuliza hizo pesa Raza mtamlipa lini. Mhe. Waziri ninamuheshimu sana pale alitamka hivi.

Alisema hivi, alisema mimi sitambui wala huna pesa hapa wala sikulipi, yule pale. Kwa hivyo inawezekana Mhe. Waziri na yeye kaliwa kivuli. Lakini Katibu Mkuu ndiye aliyepokea pesa alikuwepo na akasema hajapokea Katibu Mkuu. Inaweza kuwa Mhe. Waziri kaliwa kivuli hajui.

Sasa Mhe. Spika, ninamuomba Mhe. Waziri, mimi naipenda nchi yangu, ninachotaka mimi hizi pesa zangu kulipwa, maana nimetoa na mimi ni mfanyabiashara. Mimi sikufanya biashara kwa kuleta mazao; nimetoa *cash*, na mimi nina zaidi ya miezi sita nasema sitovunjwa moyo, nitaendelea kusaidia nchi yangu pale popote panapohitajika kusaidia. Lakini Mhe. Waziri ninakuomba hizi ni haki yangu.

Mheshimiwa isitoshe hapo, kocha wa Simba alikuja pale alikaa hotelini kwa Makungu nikaambiwa nichukue dhamana. Mheshimiwa kaja kocha wa Simba nikachukua dhamana, hawa jamaa hawakuwepo. Kocha wa Simba alizuiliwa matokeo yake Mheshimiwa nilikwenda mimi kulipa hizo pesa nyengine kwa ajili ya huyo kocha wa Simba ili sherehe zetu za Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar zisipate aibu nikalipa dola 1,180. Mheshimiwa nyaraka zote zimo humu ndani.

Kwa hivyo Mhe. Spika, mimi ninamuomba Mhe. Waziri na ninaheshimu Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, ninamuheshimu mzee wangu, lakini ninachosema kwamba hii inaweza kuvunja moyo kwa wazanzibari Mhe. Spika. Inaweza kutuvunja moyo sote sisi tuliokuwepo. Kwa hivyo Mhe. Spika, mimi ninachoomba ni kupata haki yangu kama ipo, kama haipo basi nitamuachia Mwenyezi Mungu. Nikiambiwa haipo nitamuachia Mwenyezi Mungu, lakini pesa nimetoa nimezitia kwenye *account* ninamuomba Mhe. Waziri anisaidie hili mimi pesa nilizotoa kwa kuisaidia nchi yangu, kwa heshima ya nchi yangu basi nirejeshewe. Maana wenzangu wameshasema hawaitambui, Kamati ya Mapinduzi na hao hao ndio viongozi wa Wizara waliohusika.

Mhe. Spika, baada ya hapo ninakuja katika Makadirio ya Wizara inayohusika. Mhe. Spika, ninachosema tuna mapungufu mengi Mhe. Spika, katika utekelezaji wetu wa Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Mhe. Spika, kuna vitu vingi katika ukumbi huu tunazungumza na kila Wizara zinazohusika zinaji-*commit* na kusema hili nitafanya, hili nitafanya. Mhe. Spika, jambo linaloniumiza sana mapungufu ya maadili, mapungufu waliyokuwa nayo watendaji. Mhe. Spika, hichi kitu kitatuumiza sana ndani ya Baraza la Wawakilishi la Zanzibar. Kwa sababu Mhe. Spika, maporomoko ya maadili na watendaji wakati mwengine kujiona umimi, umimi, umimi kwa kweli tunaathirika sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe unazo dakika 5 kumaliza hotuba.

Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali: Mimi ningeliomba Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwamba tuwe *serious* katika utekelezaji mzima wa ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi chini ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Mhe. Spika, hapo tulipokutana sote tunatekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Sasa ningeliomba vile vile Mhe. Spika, mawaziri wetu, ningeliomba wakati tunapokwenda katika bajeti hii, ningeliwaomba wasiwe wavumilivu kwa wale ambao wanaleta kero na kuwatesa wananchi wetu katika maendeleo kwa ujumla. Mimi ningetoa wito kwa Mawaziri huko tunakokwenda kwa kweli, kama mawaziri wetu wataendelea na kuwabeba watendaji kwa sababu tu ya kutaka kuridhika, mimi naona kutakuwa na Kamati Teule nyingi sana humu ndani.

Mhe. Spika, tumekuja hapa sisi kuwatumikia wananchi, wananchi wana shida, ningeliiomba Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais walione hili. Jana kulikuwa na upungufu wa maji katika kijiji cha Umbuji kwa muda wa miezi mitatu, basi nikaenda Idara ya Maji, nilipokwenda kule kwa bahati alikuwa Mkuu wa Wilaya ya Mjini, Mhe. Abdi Mahmoud pamoja na Mkurugenzi. Nikaambiwa Mhe. Mohamedraza sio mota yako tu, kuna mota zaidi ya 20 kwa majimbo mbali mbali zaidi ya miezi miwili maji hawana. Sasa nikamwambia Mkurugenzi na Mhe. Mkuu wa Wilaya ya Mjini yupo, tatizo nini? Mwezi wa Ramadhani unakuja hawa wenzetu waliokuwa chini ndio waliotufikisha hapa tuwasaidie hawana sauti, sisi ndio wenye sauti humu ndani. Akanambia tumeomba pesa kwenye Wizara ya Fedha na sasa hivi kuna bajeti huenda hizo fedha zikachelewa.

Mhe. Spika, kwa sababu ya heshima na naipenda nchi yangu nikamwambia kwani tatizo nini, dola elfu 50, 100,000 au ngapi, hebu niambie mashine hizi za watu wote hao kama mashine 20, 30 kwa sehemu mbali mbali, kaa na mwenzako uniambie kunahitajika dola laki moja au ngapi, bajeti hii kwa pesa leo na kesho hutopata na Mwezi wa Ramadhani unakuja wananchi wetu angalau tuwasaidie ili kuondosha tatizo la maji katika visiwa vya Unguja na Pemba. Nikamwambia kama kuna bajeti na Waziri anaijua bajeti hii na kama kutahitajika dola elfu 50 au 100,000 kwa kuagiza mashine hizi mimi sitaki riba, sitaki faida, niko tayari kukupeni angalau hao wananchi wa visiwa vya Unguja na Pemba wakasaidiwe maji.

Kwa hivyo, nataka kumwambia Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwamba hizi kero ndogo ambazo wala si kubwa tungelisimamia na kuziondosha kero hizi, kwa sababu kero hizo ziko nyingi sana, na kwa sababu Makamu wa Pili wa Rais ndiye Mtendaji Mkuu hapa.

Mhe. Waziri hapa tulipopitisha bajeti ya Wizara ya Miundombinu mimi ningeliomba wenzangu wasinitizame kama Mohamedraza, mimi hapa nipo kama Mwakilishi wa Jimbo la Uzini, sitaki nionekane kama ni Mohamedraza. Nimesimama hapa kwa kiti cha Chama cha Mapinduzi basi ndio ninachokijua, lakini nimekuja hapa kwa niaba ya wananchi kuwaondoshea kero.

Mhe. Spika, nataka kulitolea taarifa kabisa ndio maana nikasema Kamati Teule hapa zitakuwa nyingi, na siku nyengine Mhe. Spika, inawezekana ukanambia kiti hiki Mhe. Mohamedraza Hassanali kwa lugha unazokwendanazo bora tusamehe, na mimi nitakubali kuisamehe mbele ya Mwenyezi Mungu.

Mhe. Spika, tulipitisha bajeti hapa Mhe. Waziri wa Fedha akanambia Mhe. Mohammedraza Hassanali pesa tunazopitisha hii buti usigonge. Mimi nikasema bado, Mhe. Spika wewe ndiye baba yangu, wewe ndiye kiongozi wetu, wewe ndiye mtu mzima wetu, umesimama ukamuomba Mwenyezi Mungu ukanambia mimi mwanao, mwanangu Raza basi madhali pesa zipo zishapatikana pitisha bajeti. Mheshimiwa nilikuheshimu sana kwa Mwenyezi Mungu na Mtume, matokeo yake tunaingia kwenye bajeti ya pili wala hakikuguswa kitu, halafu Mheshimiwa tuje tena hapa utwambie kwamba tukae tukusanyike tupitishe bajeti au tusipige mabuti?

Mhe. Spika, mimi sikufichi nimekuja hapa kwa niaba ya wananchi, ninaringa na pumzi za Mwenyezi Mungu, ikiwa wewe Mhe. Spika, umetoa kauli yako kwenye *hansard* ninayo, umesema Mhe Mohammedraza Hassanali pitisha bajeti na mimi pesa nimechangia, Waziri wa Fedha akasema pitisha bajeti.

Mhe. Spika: Mheshimiwa muda wako umemalizika.

Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohamedali: Mhe. Spika, nakubali lakini nataka kusema kwamba nitaendelea kuipenda nchi yangu. Ahsante sana.

UTARATIBU

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Spika, Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali ambaye amemaliza hivi sasa kuchangia alizungumza suala hili la fedha ambazo alitoa shilingi 71 milioni. Nataka niweke sawa tu, kwamba ni kweli zilipotoka hizi fedha mimi nikiwa kama Mjumbe, Katibu Mkuu; Ali-Khalil Mirza, Farouk…

Mhe. Spika: Uliomba utaratibu.

Mhe. Nassor Salim Ali: Nataka kuweka sawa hiyo taarifa, utaratibu kidogo.

Mhe. Spika: Nafasi nilimpa Mhe. Subeit Khamis Faki, sasa nafikiri ungojee nafasi nyengine.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Spika, jioni hii ya leo kunipa fursa na mimi kuchangia hotuba hii ya Makadirio ya Mapato ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Ofisi hii ya Makamu wa Pili wa Rais kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mhe. Spika, kwanza kabisa napenda nianze kuchangia kwenye Idara ya Maafa. Napenda nichangie hapa kwa sababu maalum. Kwanza kabisa katika mwaka huu wa fedha 2014 katika Jimbo langu la Micheweni lilipata matatizo ya maafa ya kuungua nyumba moto ambapo Kijiji cha Shumba Mjini ziliungua nyumba zisizopungua 26 na Maziwang'ombe nyumba zisizopungua 7, lakini kwa kweli maafa haya yalikuwa ni makubwa na mimi Mjumbe wako nilikuwa hapa tuna kikao, nikapata taarifa hiyo, siku ile ile nikasafiri nikaenda Micheweni kwa ajili ya kushirikiana na wananchi kwa maafa hayo yaliyotokea.

Mhe. Spika, kwa maana hiyo, napenda niishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuwa baada ya kutokea tukio hili Mhe. Makamu wa Pili wa Rais alikuweko kule Pemba kwenye ziara basi alikatisha safari zake akaenda Micheweni kuwafariji watu wa Jimbo langu la Micheweni. Kwanza namshukuru sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa hilo. *(Makofi)*

Jambo la pili, napenda nishukuru kwa sababu Waswahili wanasema linapotokea tatizo mzee akianza kufika kwanza basi na watoto nao hukimbilia kufika. Kwa hiyo, baada ya serikali kufika pale basi nawashukuru sana wananchi pamoja na wafanyabiashara mbali mbali walijitokeza kwa wingi, na kwa kweli tulifarijika sana wananchi wa Jimbo la Micheweni kwa misaada mingi tuliyoipata.

Mhe. Spika, Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ilikuweko Pemba na wao pia walikimbilia wakaenda kuwafariji wananchi wa Micheweni. Kwa hiyo, natoa shukurani sana Mheshimiwa kwa wananchi pamoja na serikali kwa suala hili. Kwa sababu ni suala zuri na hakuna anayeomba kuwa nyumba yake iungue lakini wale wengine ambao nyumba zao hazikuungua basi walipata hofu, waliona kama wameonewa wao.

Kwa hivyo, nashukuru sana kwa hilo na napenda niseme kuwa zile nyumba tayari zimejengwa lakini kuna vitu vidogo vidogo ambavyo bado havijakamilika. Sasa kama kuna mfanyabiashara yeyote au muhisani atakayekwenda kusaidia ili zile nyumba zikamilike ziwe vizuri, basi tunamkaribisha sana na tutashukuru sana kama atafanya hivyo.

Mhe. Spika, nikizungumza kuhusu suala hilo, pia napenda niseme kwamba Idara hii ya Maafa ni muhimu sana. Kwa sababu sisi tumepata mafunzo zaidi baada ya matokeo zaidi ya matatu yaliyotokea kwenye ajali za meli. Kwa hiyo, hiki kitengo ni muhimu, naiomba sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuwa hiki kitengo kiimarishwe na kuona kuwa kina umuhimu. Kwa sababu sisi kamati yetu tulikwenda kutembelea ghala ya vifaa vya maafa, kwa kweli tuliona bado vifaa vilivyoko ni vichache na havikidhi haja. Sasa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imetenga hizi shilingi 40 milioni kwa ajili ya kukuza hii Idara ya Maafa, lakini mimi naziona ni chache sana. Bajeti hii tayari ishapita lakini naomba sana Ofisi hii ya Makamu wa Pili wa Rais kupitia kitengo hiki ionekane kwamba maafa hayana muda wala wakati, kwa hiyo ni wajibu kujitayarisha kikamilifu, hiki kitengo kitayarishwe kiwe na uwezo likitokea tatizo lolote lile isiwe tunahangaika kuchawachawa. Kwa hiyo, kitengo kiimarishwe sana.

Namuomba sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais apeleke serikalini suala hili, yeye ni mtendaji mkuu wa serikali aone kama hiki kitengo ni muhimu sana na kiimarishwe kikamilifu.

Suala la pili nataka nizungumze suala la Uratibu wa Muungano. Kwa kweli pamoja na maelezo mengi aliyoyaeleza Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kama kuna changamoto nyingi za Muungano ambazo zina utaratibu wa kutatuliwa, lakini bado tuna changamoto nyingi za Muungano ambazo hazijatatuliwa, na mara nyingi sana tunakuwa tunahoji fedha ambazo zinaingia kutokana na Serikali ya Muungano kuchangia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Lakini kila tukihoji jibu lake tunaambiwa tu kama zinapatikana. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Ofisi hii ya Makamu wa Pili wa Rais hizi fedha zinazoingia kwenye michango ya Muungano kupitia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tufanyiwe semina Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ili tupewe changamoto, tuelezwe kwa utaratibu mkamilifu, hizi fedha zinavyoingia. Kwa sababu sisi katika kuambiwa kwetu zinaingia hatujui zinaingia vipi na zinatokea vipi. Kwa hiyo, naomba Ofisi hii iandae semina maalum kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ili kuelezwa zinaingiaje na zinatokaje hizi fedha.

Suala la pili kuhusu Muungano, amezungumza Mhe. Makame Mshimba Mbarouk hapa kuhusu gari za *escort* za viongozi. Sisi kamati yetu tulikwenda Dar es Salaam na tulikwenda moja kwa moja katika Wizara ya Mambo ya Ndani tukaenda kuonana na Ofisi ya *IGP*, yeye mwenyewe alikuwa hayupo lakini watendaji wake walikuwepo, tukazungumza nao kuhusu *escort* za viongozi na tukaambiwa kuwa tutafanyiwa maarifa ziletwe. Kwa sababu mimi ninavyoelewa *escort* ni suala la Muungano; maana Ofisi ya Mambo ya Ndani ni ya Muungano, pamoja na kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina uwezo wa kutafuta *escort*, lakini sasa haya ni masuala ya Muungano, leo kama haya ni masuala ya Muungano mpaka leo kwa nini kule *escort* za viongozi ziko na za kutosha, tena nzima sisi mpaka leo tuna vigari vibovu huku. Tushakwenda kupeleka maoni mpaka kamati yetu imekwenda lakini mpaka leo jibu halipatikani.

Naomba sana Mheshimiwa na suala hili liangaliwe kwa sababu ni suala la Muungano basi tutekelezewe. Pamoja na matatizo kusema kwamba kuna mengi yanayotatuliwa, lakini bado narudia kwamba kuna matatizo mengi ambayo hayajatatuliwa.

Suala la pili limezungumzwa hapa kuwa sasa hivi tayari tusharuhusiwa au tuna nafasi ya kuwa mafuta na gesi yatakuwa ni ya Wazanzibari, tutachimba kwa niaba ya kuwa ni ya Wazanzibari pekee. Lakini huku nyuma ilikuwa ni suala la Muungano na kuna fedha nyingi ambazo zimekusanywa kule Bara kuhusu suala hili la mafuta na gesi, kwa nini hatupewi hizi fedha ambazo ilikuwa bado ni suala la Muungano na hatujaambiwa kuwa ni kiasi gani cha fedha kilikusanywa tukapewa. Kwa hiyo, kama linataka kutolewa lakini halijatolewa, sasa huku nyuma ambako lilikuwa ni suala la Muungano, kwa nini hizi fedha tusipewe wakati ni haki yetu kupewa, hatuombi ni haki yetu. Kwa sababu suala ni la Muungano na mpaka sasa halijatolewa, kwa nini tusijue hizi fedha kama ni kiasi gani kilichokuwa chetu ni haki yetu tupewe. Tunaiomba sana Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais itudaie fedha hizi ni haki yetu, na itudaie tujue kama tumepewa na tuambiwe tumepata kiasi fulani cha fedha hizo.

Jengine ninalotaka kulizungumza ni suala ambalo sasa hivi linazungumzwa kwenye vitabu vyote, kila kitabu kinachokuja kinasisitiza amani, utulivu na mshikamano wa nchi yetu. Lakini kwa nini tunasema midomoni tu kwenye vitendo hatusemi. Sisi tunasema amani kwa midomo tu hatutekelezi kwa vitendo.

Mhe. Spika, leo watu wanathubutu kusimama hadharani wakisema Wapemba wendezao kwao hii ni amani na utulivu au inaashiria nini? Hili si suala la amani na utulivu. Mwisho sasa hivi kwa kweli tumelewa na shuwari *madabe* yamekuja juu yanaelea. Mheshimiwa tunachezea shilingi kwenye shimo la choo. Huku nyuma tusisahau haraka tulivyokuwa, nyuma tulivyokuwa hapana asiyejua hapa, nchi hii ilikuwa misaada haiendi, serikali haiendi, mishahara ya wafanyakazi hailipwi, leo kwa sababu tuna amani na utulivu kuna watu wanachokora. Mheshimiwa nawaambia tusichezee shilingi katika shimo la choo, ikiwa wamesahau haraka kwa shuwari iliyopo wasisahau.

Leo kuna watu wanasema walete mswada tuondoe Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Mimi nasema basi uletwe haraka huo mswada tusiucheleweshe, kwa sababu tukiucheleweshe hatutopata kuuchangia, uje haraka sana tupate kuuchangia, ikiwa shuwari tuliyonayo tushalewa tunataka turudi tena kule tulikokuwa basi tayari na turudi. Lakini mimi nawambia tusichezee shilingi katika choo, tusione kwa sababu sasa hivi tunakusanya mapato serikali inakwenda, tunataka turudi tena kule nyuma tulikokuwa. Nawasihi sana msichezee shilingi katika shimo la choo, sisi Wazanzibari maana ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuleta umoja na mshikamano wa nchi hii.

Leo kuna watu huu mshikamano uliopo wanauchezea washaona *waroba*, kwa sababu kuna watu kama hakuna ugomvi hawaneemeki, kuna watu wanachochea ugomvi ili waneemeke kwa ule ugomvi, tunaelekea wapi? Badala ya kuleta maendeleo kwenye nchi yetu mnaturudisha nyuma, haya tuendeleeni turudini nyuma. Nakuomba

Mheshimiwa wewe ndiye mratibu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar unaona watu wakifanya uchochezi serikali ndio yenye uwezo wa kuwakemea watu hao, leo ukipita Kisonge kumeandikwa matusi ya Wapemba na hakuna mtu anayekemea, serikali kama iliyolala, haiwezi kukemea, kwa nini jamani tunakwenda hivi?

Nakumbuka wakati wa Karume mtu akija na manywele mabaya tu ananyolewa, kaja na suruali mbaya ilikuwa ikichanwa, leo serikali kama iliyolala haipo, kwa nini tunakwenda hivi jamani? Viongozi wapo watu wanafanya uchochezi, watu wanafanya mabaya wanatizamwa tu, serikali haikemei wakati serikali ndio baba, serikali ndio mama katika nchi, mwenye uwezo mwengine ni nani kama si serikali. Wale watu wanachochea nchi, wanatia ugomvi katika nchi wanatizamwa tu, hivi kama viongozi hawapo! Mimi nasema tusifanye masihara na amani, amani ikiwepo ikiondoka kuirudisha ni kazi, wenzetu wameanza hivi hivi, wenzetu wameanza matatizo kidogo kidogo lakini wakishaanza matatizo kidogo kidogo baadae yanakuwa makubwa. Mtu atizame akiwa na chungu akiikuna halafu likiwa donda, likiambuka donda kulirudisha ni kazi, kutia dawa mpaka ukapoa. Leo watu wanafanya masihara na amani.

Tutizame hapo Sudan wamegawika sehemu mbili sasa hivi, kuna Bokoharamu na nini sijui, jamani mnatupeleka wapi. Leo serikali tumekaa tumetulia tunakusanya mapato tunajisifu halafu mnaturudisha. Mheshimiwa mimi naunga mkono hotuba hii lakini nawaambia msicheze na shilingi katika choo. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Nakushukuruni Waheshimiwa Wajumbe kwa mashirikiano makubwa ambayo tumeonesha hadi sasa hivi. Niwaombe kwamba tuendelee na mashirikiano hayo.Suala la amani na utulivu ni jukumu letu sote, viongozi tuliomo humu tusisitize amani hiyo iendelee kudumu, na tusioneshe kwa namna yoyote ile kama vile kwamba amani hiyo tunataka itoweke. Amani iendelee kudumu; mshikamano uendelee kuwepo na mashirikiano yaendelee kujenga nchi yetu kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wetu.

Naomba sana Waheshimiwa Wajumbe; chombo hiki ni chombo kikubwa, ni chombo muhimu. Chombo hiki kinategemewa na wananchi ili kiweze kutoa uongozi kwa wananchi wetu, lakini hatimaye kuleta maendeleo ya wananchi hao. Tujitahidi tusichoke na tuhimizane kwamba amani iendelee kudumu kwa ajili ya maisha ya wananchi wetu.

Waheshimiwa Wajumbe nilitaka niseme maneno hayo. Unajua kawaida ya binadamu ile mtu kusema tu kwa sauti kali, basi huko wananchi tayari wanapokea kwamba kule sasa watu wameanza kutofautiana; yaani viongozi sisi tumeanza kutofautiana. Tujitahidi sana kuwa wamoja na tufanye kazi ya wananchi Waheshimiwa Wajumbe.

Baada ya maneno hayo machache sasa niakhirishe kikao hiki hadi kesho tarehe 22/05/2014 saa tatu barabara za asubuhi.

(Saa 1:43 usiku Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 22/05/2014 saa 3:00 asubuhi)